

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 18 Julai, 2009

(Mkutano Ulianze Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 (*The Annual Report and Accounts of Arusha International Conference Center for the Year 2007/2008*)

MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka 2008/2009, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

MHE. HEMED MOHAMMED HEMED (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):

Taarifa kwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Randama za Makadirio ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010 – Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia Taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (NUU), naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu, likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii, kukupongeza wewe binafsi, Wenyeviti na Mheshimiwa Spika, kwa uongozi thabiti na kwa kuongoza Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge hili la Awamu ya Nne, kwa umahiri mkubwa na hivyo kuliwezesha kutekeleza ipasavyo, majukumu yake yenye kukidhi matarajio ya wananchi. Vile vile, natoa pongezi zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kusimama imara katika kutetea maslahi ya wananchi wetu na kusaidiana na Serikali katika kuchukua hatua juu ya changamoto mbalimbali zinazoikabili nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa namna ya pekee, niwashukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda na Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, ambao Hotuba zao zimetoa dira ya Taifa letu katika mwaka huu wa fedha. Hotuba zao zimegusia mambo ya kimsingi yanayohusu Wizara yangu katika mwaka huu wa fedha. Hivyo, sina budi kuwashukuru kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa maana wameifanya kazi yangu kuwa nyepesi zaidi. Naomba pia nitoe shukrani zangu za dhati, kwa Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote walionitangulia katika kuwasilisha Hotuba zao, kwa kuzungumzia kwa ufasaha baadhi ya masuala ya Ushirikiano wa Kimataifa, wanayoyashughulikia katika Wizara zao. Wizara yangu imekuwa ikishirikiana vyema na kwa karibu sana na Wizara hizi na mara zote imekuwa ikizingatia ushauri wao kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (NUU), chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Wilson Masilingi, kwa ushauri wao ambao umekuwa wa msaada mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu kwa mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, ambaye tumeshirikiana vyema katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, namshukuru Kaimu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Mabalozi wetu, pamoja na Wafanyakazi wenzangu wote Wizarani na katika Balozi zetu, kwa kuwezesha kukamilisha bajeti hii kwa wakati na kwa mafanikio. Zaidi ya hapo, nawashukuru na kuwapongeza kwa uchapakazi wao mzuri, unaowezesha Taifa letu kutetea ipasavyo maslahi yake nje na ndani ya nchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru wapiga kura wangu na Wananchi wa Jimbo la Mtama, kwa upendo wao na kutotetereka kwa imani yao kwangu. Napenda pia niwashukuru Viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi na Serikali

wa Mkoa wa Lindi, kwa uongozi uliotukuka na kwa ushirikiano wao mkubwa. Kwa upande wa familia yangu, ningependa kumshukuru sana mke wangu Dorcas Membe, pamoja na watoto wangu, kwa kusimama kidete kunitia moyo na nguvu katika shughuli zangu za kila siku. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii, kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya wa Chama cha Mapinduzi, waliokitoa kimasomaso chama chetu katika chaguzi ndogo na hivyo kudhihirisha msemo wa wahenga unaosema *isiyo kongwe haivushi*.

Nawapongeza Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kwa kushinda chaguzi ndogo katika Majimbo yao. Ushindi wao ni heshima kubwa kwa Chama cha Mapinduzi na ishara ya imani kubwa waliyonayo wananchi kwa Chama Tawala cha CCM. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane pia na Wabunge wenzangu, kutoa mkono wa pole kwako Mheshimiwa Naibu Spika na kwa familia za Wabunge wenzetu, waliofariki dunia katika mwaka wa fedha uliopita. Naomba kuwataja kwa heshima, Marehemu Richard Said Nyaulawa, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Marehemu Phares Kabuye, aliyekuwa Mbunge wa Biharamulo Magharibi na Marehemu Faustine Kabuzi Rwlomba, aliyekuwa Mbunge wa Busanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kuwapa mkono wa pole, wahanga na waathirika wa milipuko ya mabomu iliyotokea katika eneo la Mbagala Kuu, Jijini Dar es Salaam na majanga mengine yaliyotokea nchini mwetu. Nawaombea faraja walioathirika na majanga haya na kwa wale waliopoteza maisha, tuendelee kumwomba Mwenyezi Mungu, azipumzishe roho zao mahala pema peponi. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya kiuchumi duniani imeendelea kuzorota toka nilihutubie Bunge lako Tukufu katika Hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka jana. Changamoto mpya zinazidi kujitokeza na kutishia mustakabali wa dunia hasa katika nchi maskini. Wakati ambapo bei za mafuta na chakula zikionekana kupatiwa ufumbuzi, dunia imekumbwa na mgogoro wa kiuchumi ambaa umetikisa nchi zote, tajiri na maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro wa uchumi ulioanzia nchi zilizoendelea kutohana na upungufu katika mifumo ya udhibiti wa uchumi wa soko, ulifafanuliwa kwa ufasaha na ufanisi mkubwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alipozungumza na Wananchi wa Dodoma na Wabunge tarehe 10 Juni, 2009 katika Ukumbi wa Kilimani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza na katika tukio la kihistoria, Shirika la Fedha Duniani (IMF), likishirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lilifanya mukutano na Mawaziri wa Fedha pamoja na Magavana wa Benki Kuu wa nchi za Afrika Mjini Dar es Salaam. Mukutano huo uliofunguliwa na Mheshimiwa Rais Kikwete hapo mwanzoni mwa mwezi Machi 2009, uliipa Tanzania heshima kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya mukutano huo yalikuwa ni kujadili hoja na kutoa mapendekezo ya nchi za Afrika, juu ya namna ya kukabiliana na athari za mgogoro wa uchumi duniani ili hoja na mapendekezo hayo yawasilishwe katika mukutano wa nchi tajiri duniani (G20), uliofanyika mwezi Aprili 2009 huko London.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Mkutano wa IMF na Mawaziri wa Fedha, pamoja na Magavana wa Benki Kuu wa Nchi za Afrika, Mheshimiwa Rais Kikwete, alipewa heshima kubwa ya kuwasilisha hoja na mapendekezo yaliyotokana na mkutano huo katika mkutano wa maandalizi wa G20. Pamoja na Tanzania, nchi za Ethiopia na Afrika ya Kusini, ziliajwa katika mkutano huo, kueleza athari za mgogoro wa uchumi kwa Bara la Afrika mbele ya nchi tajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imebaini maeneo yaliyoathirika na mgogoro wa uchumi nchini. Baadhi ya maeneo hayo ni kuperomoka kwa bei za mazao yanayouzwa nchi za nje kwa kati ya asilimia ishirini na hamsini, sekta ya utalii iliypungua kwa asilimia kumi na nane; na madini, isipokuwa dhahabu kwa asilimia hamsini. Aidha, makampuni yaliyokuwa yanaendesa shughuli zao katika maeneo hayo, nayo yameathirika sana na kupungua kwa uwekezaji na utalii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na athari hizi, Serikali ya Tanzania iliona na kutambua ulazima wa kuchukua hatua (*rescue package*) za kupambana na hali hii. Kiasi cha shilingi trilioni 1.7 zimetengwa ili kunusuru uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu mkubwa, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa hotuba yake nzuri, aliyoitao tarehe 10 Juni 2009, kuhusu hatua zilizochukuliwa na Serikali ili kukabili mgogoro wa uchumi nchini, wakati akiwahutubia Wananchi wa Dodoma na Wabunge kwenye Ukumbi wa Kilimani. Hotuba yake, ambayo imesambazwa kwa Balozi zote, imetoa dira kwangu na Wanadiplomasia wenzangu, kuhusu namna ya kuelezea suala hili wakati wa kuzungumza na mataifa tajiri ya Marekani, Ulaya na Asia, hasa ikizingatiwa kwamba masoko ya bidhaa zetu nje kwa kiasi kikubwa yako kwenye mataifa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizochukuliwa na Mheshimiwa Rais ni za kijasiri, hivyo sielewi kama kuna nchi nyingine hapa Afrika, iliyochukua hatua za kukabiliana na athari za mgogoro wa uchumi duniani kama Tanzania ilivyofanya. Ni mategemo yangu kwamba, nchi nyingine zitaiga mfano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bara letu limekabiliwa na jinamizi la Mapinduzi ya Kijeshi, ambalo limerejea kwa kasi baada ya kutulia kwa muda. Wimbi la sasa lilianzia Mauritania na kufuatiwa na Madagascar. Mabadiliko yasiyofuata misingi ya demokrasia yalitokea pia Guinea, kufuatia kifo cha Rais wa nchi hiyo, Jenerali Lansana Conteh. Aidha, Mheshimiwa Joao Bernardo “Nino” Viera, Rais wa Guinea Bissau, aliuawa kikatili na askari waasi, kufuatia mauaji ya Mkuu wa Majeshi ya nchi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Umoja wa Afrika umelaani vikali mapinduzi na mauaji hayo, kwa sababu yanakiuka demokrasia na Utawala Bora, misingi ambayo tumejiwekea kwenye Katiba ya Umoja wa Afrika, Mkataba wa Kuanzisha Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika, pamoja na Tamko la Lome la Mwaka 2000, kuhusu Mabadiliko ya Serikali yasiyozingatia Misingi ya Demokrasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeungana na Umoja wa Afrika na Jumuiya ya Kimataifa, kulaani matukio hayo, kwa sababu yanaturudisha nyuma. Naomba kuchukua fursa hii, kuzitaka nchi hizo, kurejea kwenye misingi ya demokrasia na utawala wa sheria, kama njia ya kubadilisha uongozi, kutatua matatizo yao na kuleta maendeleo. Kamwe, Tanzania haiwezi kuziunga mkono wala kuzikumbatia Serikali zinazoingia madarakani kwa njia za mabavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2008/2009, Bara la Afrika liliendelea kukabiliwa na changamoto za kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Darfur, Somalia na Zimbabwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuzorota kwa amani katika Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu, kuliathiri usalama na shughuli za kijamii katika mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Hali hii ilisababisha kuitishwa Kikao cha Dharura cha Wakuu wa Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu, Umoja wa Afrika, Umoja wa Mataifa, Umoja wa Ulaya na Jamii za Kimataifa ili kutafuta ufumbuzi wa mgogoro huo. Mkutano huu ulifanyika mwezi Novemba 2008, Mjini Nairobi Kenya, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa mkutano wa Nairobi ulikuwa ni kuunda timu ya usuluhishi wa mgogoro huo. Kwa upande wa Umoja wa Mataifa, Rais Mstaafu wa Nigeria aliteuliwa kuwa mwakilishi mahususi wa Katibu Mkuu. Kwa upande wa Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu, aliteuliwa Rais Mstaafu wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, hasa ikizingatiwa kuwa ni kiongozi shupavu, mwenye uelewa mpana wa masuala ya kisiasa, kiulinzi na usalama ya Kanda hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Mkapa, kwa kazi nzuri aliyoifanya ndani ya muda mfupi hadi kufikia makubaliano ya kuleta amani Mashariki mwa Kongo. Makubaliano hayo, yalitiwa saini mwezi Machi 2009, Mjini Goma na kushuhudiwa na Timu ya Usuluhishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichobaki sasa ni kuisaidia Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo katika kufanikisha utekelezaji wa makubaliano hayo. Kwa mantiki hiyo, Tanzania imepokea ombi kutoka Umoja wa Mataifa la kutoa mchango wa wakufunzi wa masuala ya kijeshi mia mbili kwenda kufundisha Askari wa Jeshi la Ulinzi na Usalama la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ili kusaidia kuliunda upya Jeshi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro wa Darfur nao bado unaendelea. Suala la kurejesha amani na usalama Darfur ni mionganoni mwa ajenda kuu katika Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa. Mwezi Machi, 2009, Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai (ICC), ilitoa hati ya kumfungulia mashtaka Mheshimiwa Omar El Bashir, Rais wa Sudan, kwa makosa ya kivita, makosa dhidi ya ubinadamu na mauaji ya Kimbari na hivyo kupuuza ombi la Umoja wa Afrika kuwa utoaji wa hati ya mashtaka usimamishwe hadi wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Umoja wa Afrika ulilaani kitendo hicho, kwa sababu hakisaiddii kutatua tatizo la janga la kibinadamu linaloikabili Darfur. Kinyume chake, kumkamata Rais Bashir ambaye ni mdau muhimu katika amani ya Darfur, kunahatarisha utekelezaji wa Mkataba wa Amani ya Sudan ya Kusini, ambayo inajiandaa kwa uchaguzi mwezi Julai 2009 na kupiga kura ya maoni mwaka 2011 kuhusu hatima ya eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi mwishoni mwa mwezi Machi mwaka huu, walinda amani wapatao 15,751 wakiwemo wanajeshi 12,925, polisi 2,426 na watumishi wengine 2,669, walishapelekwa Darfur kuunga mkono juhudhi za kulinda amani. Tanzania imepeleka batalioni moja kutoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) mwezi Julai, 2009, itakayoungana na vikosi vya pamoja vya Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa (UNAMID).

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi ya Somalia inakabiliwa na changamoto kubwa tatu, ikiwa ni pamoja na kuporomoka kwa mihimili ya dola, uharamia na uhaba wa chakula. Hali ya usalama nchini Somalia inazidi kuzorota. Kuondoka kwa vikosi nya Ethiopia, kuliacha pengo la kiusalama na kudhoofisha Serikali ya Mpito, hivyo kutoa mwanya kwa kikundi cha Al Shabab kufanya mashambulizi dhidi ya Serikali hiyo. Ni hofu ya Tanzania kwamba, iwapo Jumuiya ya Kimataifa na hasa nchi za Afrika zilizoahidi kupeleka majeshi yao kusaidia Serikali ya Somalia hazitatekeleza ahadi zao, kuna hatari kubwa ya kuangushwa kwa Serikali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na vita nya wenyewe kwa wenyewe vinavyoendelea, tatizo la uharamia pia limeshika kasi kwenye Pwani ya Somalia. Hali hii inatishia kukua kwa biashara za kimataifa kati ya Bara la Afrika na Mabara mengine, hasa ikizingatiwa kuwa mwaka 2008 pekee, zaidi ya meli 42 zilitekwa nyara na mabaharia 815 kushikiliwa kama mateka. Uharamia huu unaongeza gharama za bima na usafirishaji na hivyo kuathiri biashara. Napenda kuchukua nafasi hii, kuzishukuru Serikali zinazoshiriki kutafuta ufumbuzi wa tatizo la uharamia zikiwemo Marekani, Ujeruman, Uingereza, Denmark na Australia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mvutano na tofauti za kisiasa nchini Zimbabwe, zimeanza kupungua baada ya Serikali ya Umoja kuanzishwa mwezi Februari 2009. Napenda kuchukua nafasi hii, kuwapongeza wananchi na wadau wote wa siasa wa Zimbabwe, kwa uvumilivu wao na hatua walizochukua kurejesha amani na utulivu. Aidha, tunaiomba Jumuiya ya Kimataifa, iunge mkono Serikali ya Umoja ya Zimbabwe na mpango wake wa Dharura wa Kufufua Uchumi, pamoja na kuiondolea nchi hiyo vikwazo nya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuleta mageuzi ya mfumo wa utendaji wa Umoja wa Mataifa na shughuli zake, Tanzania ni moja ya nchi nane zinazotekeliza Mradi wa Majaribio wa Umoja wa Mataifa wa *One UN* unaotarajiwa kukamilika Desemba 2009. Mradi huo unatarajiwa kuongeza ufanisi na kuboresha utendaji wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa yaliyopo hapa nchini katika miradi wanayoitekeliza kwa pamoja. Aidha, Mradi huo utasaidia kupunguza gharama za uendeshaji na urasimu usio wa lazima. Faida ya Mradi huo ni kusaidia kuongeza ushiriki na sauti (*National Ownership*) ya Serikali katika uendeshaji wa miradi ya pamoja iliyo chini ya *One UN*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tarehe 15 Juni, 2009, Mradi wa kusaidia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 ulizinduliwa Mjini Dar es Salaam. Mradi huu, unaosimamiwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), una malengo makuu yafuatayo:-

Moja; kuimarisha uwezo wa kitaasisi, kiutawala na kiutendaji wa Tume za Uchaguzi za Tanzania na Zanzibar (NEC/ZEC) ili kuziwezesha kupanga shughuli za kuandaa, kuendesha na kusimamia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010;

Mbili; kusaidia utoaji wa elimu kwa wapiga kura ili kuhakikisha kwamba wapiga kura, hasa wanawake, vijana, walemau na makundi mengine yaliyotengwa na jamii, yanapata haki zao za kupiga kura;

Tatu; kuvisaidia Vyama nya Siasa nchini na asasi zisizo za kiserikali kuchangia katika uandikishaji wa wapiga kura, usimamizi madhubuti na utatuzi wa migogoro baada ya uchaguzi;

Nne; kutoa mafunzo ya kuratibu shughuli za wasimamizi wa kimataifa wa uchaguzi hususan kwa kuhakikisha kuwa hawapati vizuizi vyovoyote katika kutekeleza majukumu yao ya usimamizi; na

Tano; kuimarisha uwezo wa vyombo vya habari vya kitaifa na kimataifa wa kutoa habari za uchaguzi kwa uwazi na kwa uwiano chanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha dola za Kimarekani milioni ishirini na tatu zimetolewa na nchi wahisani, kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu. Napenda kutumia nafasi hii, kuzishukuru nchi za Denmark, Finland, Norway, Sweden, Uswisi, Uingereza, Uhlanzi na Umoja wa Ulaya, kwa ufadhili wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haikatazi Jumuiya ya Kimataifa kutoa misaada, lakini misaada inayotolewa ama kwa vyama vya siasa au shughuli nyininge ni muhimu iwe ya uwazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu iko katika maandalizi ya kushiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Madola, utakaofanyika Port of Spain, nchini Trinidad and Tobago, tarehe 27 hadi 29 Novemba 2009. Kaulimbiu ya mkutano huo ni Ushirikishi kwa ajili ya Maendeleo Endelevu yenye Usawa (*Partnering for a more equitable and sustainable future*). Mkutano huo utatoa fursa muhimu ya kujadili mikakati ya kuhakikisha ushiriki sawa katika uchumi wa dunia hasa katika kipindi hiki cha mgogoro wa uchumi. Hili litakwenda sambamba na kujadili njia bora ya kufanya mageuzi katika mifumo na taasisi za fedha za kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitakuwa nimetenda haki, nisipotambua na kukupongeza wewe Mheshimiwa Naibu Spika na Bunge lako Tukufu, kwa kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Jumuiya ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola, utakaofanyika Mjini Arusha, mwezi Septemba 2009. Sina shaka hata kidogo, juu ya kufanikiwa kwa Mkutano huo chini ya Uenyekiti wako. Bila shaka Mkutano huo utaitangaza nchi yetu na kuchochea Sekta ya Utalii na huduma hasa katika kipindi hiki cha mgogoro wa uchumi. Wizara yangu inakuahakikisha ushirikiano katika kufanikisha mkutano huo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Februari, 2009, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alimaliza muhula wake kama Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika. Nafasi hiyo sasa imechukuliwa na Kiongozi wa Libya, Kanali Muammar Gaddafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uenyekiti wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwenye Umoja wa Afrika, ulikuwa na mafanikio makubwa sana. Mheshimiwa Rais, amelitangaza vyema jina la Tanzania na kuiletea nchi yetu heshima kubwa mionganoni mwa mataifa, pamoja na kuimarisha Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nafasi hiyo, Tanzania iliongoza Bara la Afrika kwenye mikutano ya ushirikiano baina ya Afrika na Japan (TICAD IV), India na Uturuki, kwa nyakati tofauti. Aidha, kwa nafasi yake ya Uenyekiti, Tanzania iliwalilisha Bara la Afrika katika Mkutano wa G8 uliofanyika Hokkaido, Japan mwezi Julai 2008. Mikutano hii ililetia tija kwa Bara la Afrika na Taifa letu. Aidha, Mheshimiwa Rais alihudhuria Mikutano kadhaa ya Kimataifa kama Mwenyekiti wa AU.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mafanikio ya mikutano hiyo ni ahadi ya mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Japan, kwa ajili ya ukarabati wa Bandari ya Mtwara na

ujenzi wa barabara kutoka Tunduru - Matemanga hadi Namtumbo na msaada wa upanuzi wa Barabara ya Ali Hassan Mwinyi kuanzia Morocco hadi Tegeta, Jijini Dar es Salaam. Aidha, tumepata mkopo wa dola milioni 40 kutoka Serikali ya India, kugharamia pembejeo za kilimo, hususan matrekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alisimamia pia mjadala muhimu kuhusu kuanzishwa kwa Serikali ya Afrika, uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia, Februari 2009. Mjadala huu ulikuwa mgumu sana na ultishia kuugawa Umoja wa Afrika, kwa sababu baadhi ya nchi wanachama zilitishia kujiondoa kutoka kwenye Umoja huo kama Serikali ya Afrika isingeanzishwa mara moja. Baada ya mjadala mrefu, Viongozi wa Afrika walifika muafaka na kuamua kuimarisha Kamisheni ya Umoja wa Afrika (*AU Commission*), kwa kuibadili na kuunda Mamlaka ya Umoja wa Afrika (*AU Authority*), itakayokuwa na majukumu makubwa zaidi ya kujenga utangamano Barani Afrika. Kwa kiasi kikubwa, matokeo haya ni matunda ya busara, hekima na juhudni za Mheshimiwa Rais katika kujenga maridhiano. Majadiliano haya ni magumu na bado yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 18 Machi, 2004 huko Midrand, Afrika Kusini, Bunge la Afrika liliasisiwa kwa mujibu wa Kifungu Namba 17 cha Mkataba wa Abuja wa Mwaka 1991. Kuanzishwa kwa Bunge hili kulikuwa na lengo la kuliunganisha Bara la Afrika ili kuwa na jukwaa la kuzungumzia matatizo na changamoto zinazokabili Bara letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dakta Getrude Ibengwe Mongella, Mbunge wa Ukerewe (CCM), alichaguliwa kuwa Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika. Alishika wadhifa huo tangu tarehe 18 Machi, 2004 hadi tarehe 28 Mei, 2009 walipofanya uchaguzi wa Rais mpya wa Bunge hilo. Rais aliyechaguliwa ni Dakta Idriss Ndele Moussa, Mbunge kutoka Jamhuri ya Chad.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mabadiliko hayo, napenda kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Mongella, kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa kipindi chote cha Urais wa Bunge hilo. Aidha, uongozi wake umeweza kuweka misingi imara na kulifanya Bunge hilo kutimiza majukumu yake ipasavyo. Namtakia afya njema ili aendelee kutimiza wajibu wake kama Mbunge wa Jimbo la Ukerewe na mmoja wa wawakilishi wetu katika Bunge la Afrika. Pamoja na Mheshimiwa Mongella kumaliza muda wake, Tanzania bado inaendelea kung'ara katika medani za uongozi katika Jumuiya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za jumuiya za kikanda zinaendelea kupanuka na kuimarika. Aidha, kumekuwa na juhudni za kuziunganisha Jumuiya za EAC, SADC na COMESA ili kuweza kupata soko kubwa zaidi, kwani litahusisha asilimia 50 ya nchi za Afrika, pato la dola bilioni 624 na watu kiasi cha milioni 527; sawa na zaidi ya asilimia 57 ya pato na watu wa Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakuu wa Nchi na Serikali wa EAC, SADC na COMESA, walikutana mwezi Oktoba 2008 Mjini Kampala, Uganda, kujadili mikakati ya kuimarisha ushirikiano wa kanda zote tatu. Katika mkutano huo, Viongozi hao walikubaliana kuanzisha Soko Huru la Pamoja ambalo litaifanya kanda kuwa na uwezo mkubwa zaidi katika kuvutia uwekezaji na kushindana kibiashara. Kwa sasa, Sekretarieti za Jumuiya hizi zinaendelea na matayarisho ya zoezi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakuu wa Nchi na Serikali wa EAC, SADC na COMESA, walitilia mkazo maendeleo ya miundombinu. Halikadhalika, walielekeza

kwamba, ndani ya kipindi cha mwaka mmoja, Jumuiya zote tatu ziwe na programu za kuimarisha na kuratibu mipango ya kuendeleza usafiri na sekta ya nishati na kubuni njia za kugharlamia kwa pamoja miradi ya miundombinu. Kazi hii ifanyike katika kipindi cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, programu nyingi zinatekelezwa na maandalizi ya Soko la Pamoja yanaendelea kama itakavyoolezwa na Waziri mwenye dhamana hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii, kumpongeza kwa dhati na pia kumshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa juhudi na mchango wake mkubwa katika kuimarisha ushirikiano wa Kanda na Bara la Afrika. Misimamo na miongozo ya Mheshimiwa Rais, imekuwa chachu muhimu katika kutatua migogoro ya kisiasa na kuimarisha mikakati ya kukuza uchumi na maendeleo ya Kanda na Afrika kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzhishwa kwa Idara ya Diaspora, wapo Watanzania wengi wenye uwezo waishio ughaibuni. Ili washiriki katika maendeleo ya nchi yao, kama Ilani ya Uchaguzi ya CCM inavyoolekeza, Wizara yangu inaendelea na mchakato wa kuanzhisha Idara itakayoshughulikia masuala ya Watanzania wanaoishi ughaibuni. Jukumu kubwa la Idara hii ni kuandaa sera itakayosimamia masuala yote yanayohusu Watanzania wanaoishi ughaibuni ili kuwashirikisha katika mfumo rasmi wa ujenzi wa nchi yetu na kusimamia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza azma hii, zipo changamoto nyingi zitakazojitekeza ikiwa ni pamoja na upungufu wa kisheria katika nyanja mbalimbali. Kwa mfano, mfumo wa sheria katika masuala ya uraia, kazi, fedha, ardhi na uwekezaji na mengine mengi yatahitaji marekebisho kwa lengo la kuweka mazingira mazuri, ambayo yatawawutia Watanzania wanaoishi ughaibuni kuwekeza nyumbani ili kujenga nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja za kisheria kama vile uraia wa nchi mbili (*Dual Nationality*) na upendeleo kwa wawekezaji wa Kitanzania wanaoishi ughaibuni wanaotaka kuwekeza hapa nchini, zinahitaji kupitiwa upya ili kuwawutia Watanzania hao kushiriki nasi katika juhudi za kujengwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009, Wakuu wa Nchi na Serikali kutoka nchi mbalimbali walizuru nchi yetu kwa ziara za kitaifa na kikazi. Viongozi wa Kitaifa waliofanya ziara Tanzania ni kutoka Jamhuri ya Watu wa China, Comoro, Uturuki, Qatar, Uganda, Kenya, Ireland, Rwanda, Madagascar, Zambia, Botswana, Denmark, Msumbiji, Swaziland, Malawi, Australia, Iran na Cuba. Vilevile tulitembelewa na Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa wakiwemo Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na Naibu wake, Mkurugenzi Mkuu wa IMF na Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB).

Mheshimiwa Naibu Spika, mionganoni mwa mafanikio yaliyotokana na ziara za viongozi hao ni kuimarika kwa ushirikiano kwenye masuala ya kisiasa, kijamii na kiuchumi hususan uimarishaji wa huduma za afya, utalii, kilimo, biashara, miundombinu na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoptaka na nchi yetu kusifika kwa uongozi bora, unaofuata utawala wa sheria na misingi ya haki za binadamu, pamoja na usimamizi mzuri wa misaada ya kimaendeleo, viongozi wetu pia wamepewa heshima kubwa na kualikwa kufanya ziara katika nchi mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viongozi wetu ambaeo ni Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika kutekeleza shughuli za Kitaifa na Kikanda, Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa, walifanya ziara katika nchi za Marekani, China, Japan, Namibia, Afrika Kusini, Ethiopia, Uganda, Qatar, Msumbiji, Zimbabwe, Kenya, Zambia, Uingereza, Comoro, Saudi Arabia, Swaziland, Botswana, Denmark, Malawi, Rwanda, Libya, Sudan, Ireland, Ujerumani, Italia, India na Iran.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziara hizi zililenga kukuza uhusiano kati ya nchi yetu na nchi hizo, kuimarisha ujirani mwema na masuala ya usalama wa nchi yetu na Bara la Afrika kwa ujumla. Aidha, ziara hizi zimeiletea nchi yetu mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali, zikiwemo kutangaza fursa za uwekezaji zinazopatikana Tanzania, vivutio vya watalii, biashara na uimarishaji wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika ziara nchini Marekani, mwezi Mei 2009, Mheshimiwa Rais Kikwete alikuwa kiongozi wa kwanza kutoka Afrika kukutana na Rais mpya wa Marekani, Mheshimiwa Barack Obama. Katika mazungumzo yao, Marekani iliahidi kuendelea kuisaidia Tanzania kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Milenia (MCC). Aidha, Mheshimiwa Rais, alitembelea Chuo Kikuu cha Stanford, kitovu cha makampuni makubwa ya Silicon Valley yakiwemo IBM, CISCO na GOOGLE. Makampuni haya yaliahidi kuisaidia Tanzania katika mpango wake wa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano kama mhimili wa maendeleo, hasa katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Aidha, Mheshimiwa Rais Obama, ameahidi kutembelea Tanzania katika muda ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara ya Mheshimiwa Rais Kikwete nchini Saudi Arabia, Serikali ya nchi hiyo iliahidi kuongeza ushirikiano na Tanzania katika Sekta ya Kilimo ikiwemo uzalishaji wa chakula na miradi ya ujenzi wa miundombinu nchini Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Machi mwaka huu, Mheshimiwa Rais Kikwete, alifanya ziara rasmi nchini Comoro na kushiriki katika sherehe za maadhimisho ya mwaka mmoja tangu kukombolewa kwa Kisiwa cha Anjouan. Kama Waheshimiwa Wabunge watakavyokumbuka, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, liliongoza Operesheni ya Umoja wa Afrika na kumaliza uasi wa Kanali Mohammed Bacar katika Kisiwa cha Anjouan.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na sherehe hizo, Mheshimiwa Rais, alizindua kisiwani humo Tawi la Exim Bank kutoka Tanzania na kufanya Benki hiyo kuwa na matawi mawili nchini humo, ikiwa ni pamoja na lile lilofunguliwa na Mheshimiwa Rais Sambi katika Kisiwa cha Ngazija, mwezi Juni 2008. Napenda kuchukua fursa hii, kuupongeza Uongozi wa Exim Bank, kwa kuchangamka vyema fursa za kibiashara zilizoko Visiwani Comoro. Aidha, natoa wito kwa Watanzania wengine wenye uwezo kuwekeza na kufanya biashara Comoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kukua kwa mahusiano kati yetu na Comoro na kuongezeka kwa biashara kati ya nchi mbili hizo, Serikali inakusudia kufungua Ubalozi Mdogo Visiwani Comoro, baadaye mwaka huu. Ubalozi Mdogo huo, utawasaidia kwa karibu zaidi wananchi wetu wanaofanya shughuli zao kati ya nchi yetu na Visiwa vya Comoro. Serikali ya Comoro, tayari imetupatia eneo lenye majengo matatu kwa ajili ya shughuli za Ubalozi. Mategemeo yangu ni kuwa, mchakato wa ufunguzi wa Ubalozi Mdogo wa Tanzania Visiwani Comoro, utaimarisha zaidi uhusiano wa nchi zetu mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Tanzania ipo katika mchakato wa kufungua Ofisi za Kibalozi katika mwaka huu wa fedha nchini Korea ya Kusini, Namibia, Uturuki, Uholanzi na Comoro ili kuendelea na utekelezaji wa Sera ya Diplomasia ya Kiuchumi, itakayoiwezesha nchi yetu kunufaika na fursa za uchumi, utalii na biashara, zitakazotokana na mahusiano baina ya nchi yetu na nchi hizo. Pamoja na nia hiyo, kikwazo kikubwa kinachokwamisha utekelezaji wa azma hii ni ufinyu wa bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu imeendelea na jukumu lake la kuratibu na kutoa huduma za Kitiifaki na Kikonseli. Aidha, mwongozo kuhusu uteuzi wa Wawakilishi wa Heshima na uendeshaji wa Konseli za Heshima umekamilika. Hivyo, Wizara imeanza mchakato wa uteuzi wa Wawakilishi wa Heshima kwa kutumia mwongozo huu mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Tanzania imepokea Mabalozi wapya wapatao ishirini na tano kutoka nchi za Nigeria, Namibia, Saharawi, Ubelgiji, Ujeruman, Cuba, Oman, Japan, Palestina, Uturuki, Korea ya Kusini, Columbia, Mauritius, Ethiopia, Senegal, Chile, Vietnam, Tunisia, Sierra Leone, Liberia, Cote d' Ivore, Uingereza, Indonesia, Hispania na Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoleza kwenye Hotuba ya Bajeti, kwa mwaka wa fedha 2008/2009, mabadiliko ya Muundo wa Wizara yangu, yamekuwa yaktikea kila inapobidi ili kufikia lengo la kuwa na muundo mzuri na unaoendana na wakati huu wa sayansi na teknolojia. Mabadiliko haya pia yanalenga kuboresha utendaji kazi na hatimaye kuongeza tija kwa Wafanyakazi wa Wizara yangu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo na uendelezaji wa watumishi katika Wizara, yamepewa kipaumbele ili kuwa na watumishi wenye uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa tija na kwa ufanisi mkubwa wakati wote. Aidha, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara ilipeleka watumishi ishirini kwa mafunzo ya muda mfupi na watano kwa mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na mafunzo hayo yanayogharamiwa na Serikali, mafunzo mengine kwa watumishi yamekuwa yaktilewa na kugharamiwa na nchi marafiki na Taasisi za Kimataifa. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na yale ya muda mfupi, kwa watumishi kwa kutumia fedha zetu wenyewe na ufadhili wa nchi marafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inaendelea kuwashirikisha wafanyakazi kupitia Baraza la Wafanyakazi ili kuelewa mapendekezo ya bajeti na malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha husika. Ni matarajio yangu kuwa, mukutano ujao wa Baraza la Wafanyakazi, utafanyika katika robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha, mara baada ya bajeti hii kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoiliarifu Bunge lako Tukufu mwaka jana, Wizara yangu ipo katika awamu ya pili ya kuimarisha mchakato wa mawasiliano na wadau wake. Sasa tovuti ya Wizara imeshaboreshw zaidi na inaweza kupatikana kwa kutumia anuani www.mfaic.go.tz. Aidha, zoezi la kuwianisha tovuti za Balozi zote za Tanzania, linaendelea kwa lengo la kuwapa watumiaji wote wa tovuti yetu, urahisi wa kupata taarifa za Balozi zetu zote za Tanzania katika tovuti moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha, Wizara inatarajia mabadiliko katika muundo wake. Mabadiliko hayo, yatalenga kuwa na Idara itakayoshughulikia masuala ya Watanzania waishio ughaibuni (*diaspora*); kuwa na Sehemu katika Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa itakayoshughulikia masuala ya Ukanda wa Maziwa Makuu; na pia kuimarisha Idara ya Mambo ya Nje, Zanzibar. Aidha, Wizara yangu itaendelea kuteua Wakurugenzi Wasaidizi katika Idara zinazohusika ili kuleta ufanisi zaidi katika utendaji kazi wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nafasi hizo za uteuzi, Wizara bado ina upungufu wa watumishi katika Ikama yake. Hivyo basi, Wizara inashirikiana na Taasisi husika, kuongeza watumishi wa taaluma na fani mbalimbali na pia kutoa mafunzo maalum kwa wale waliopo ili kuweza kukidhi mahitaji ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la majengo ya ofisi na makazi kwa ajili ya Balozi zetu nchi za nje bado ni changamoto kubwa. Mengi ya majengo yetu tuliyonayo, yanahitaji ukarabati mkubwa. Hivyo, ni matarajio yangu kwamba, Bunge lako Tukufu litaendelea kuidhinisha fedha kwenye Bajeti ya Maendeleo ya Wizara kwa ajili ya ununuzi, ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi wa Balozi zetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoelezwa katika taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2008/2009, Wizara tayari imeingia mkataba na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi ya Ubalozi wetu Jijini Nairobi, Kenya. Ujenzi huo utaanza kati ya mwezi Septemba na Oktoba 2009. Aidha, Wizara inaangalia uwezekano wa kuingia mikataba na Mifuko mingine ya Hifadhi za Jamii kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Ubalozi wa Maputo na baadaye majengo mengine huko Kigali, London na Abuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Wizara imeendelea kuratibu shughuli za uendeshaji wa Mahakama ya Afrika, kwa kusaidia mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa ofisi za kudumu kwa ajili ya matumizi ya Mahakama hiyo ili kuipa nchi yetu heshima inayostahili kama Mwenyeji wa Mahakama hii. Wizara iko katika hatua za mwisho za kuandaa tamko litakaloiwesha Tanzania kutambua mamlaka au uwezo wa Mahakama hii na hivyo kumwezesha mtu binafsi kupeleka malalamiko yake mbele ya Mahakama hiyo. Hata hivyo, mtu huyo ataweza kufanya hivyo pale tu ambapo itadhihirika kwamba, ameshindwa kupata haki zake kuitia mahakama zilizopo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Kujitathmini kwa Utawala Bora Barani Afrika (*African Peer Review Mechanism –APRM*), una lengo la kuzipatia nchi za Kiafrika fursa ya kujipima ili iwe njia ya kujua matatizo yao na kujirekebisha kwa madhumuni ya kuaminika, kukopesheka ama kusaidiwa na Jumuiya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Machi mwaka huu, Serikali yetu ilipokea ujumbe kutoka Umoja wa Afrika, ukiongozwa na Profesa Adebayo Adedeji, anayesimamia mpango huu kwa upande wa Tanzania. Lengo la ziara yake, lilikuwa ni kufuatilia hatua iliyofikiwa na Tanzania katika kutekeleza mchakato wa kujitathmini pamoja na kukutana na wadau wanaohusika na mchakato huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC), kimeendelea kufanya kazi vizuri. Kituo kimeendelea kuyaweka majengo yake na mazingira kwa ujumla katika hali ya kupendeza. Ukumbi wa Simba umeboreshwa na sasa una uwezo wa kuchukua watu 1,350 ikilinganishwa na watu 800 hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2008, jumla ya mikutano 172 imefanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC). Kati ya mikutano hiyo, 132 ilikuwa ya kimataifa na 40 ilikuwa ya kitaifa. Jumla ya wageni walioshiriki kwenye mikutano hiyo ni 34,948. Matarajio ya Kituo ni kuongeza idadi ya mikutano kila mwaka, kujitangaza na kutoa huduma bora zaidi kama kaulimbi ya Kituo inayosema kwamba, *We Bring the World to Tanzania*. Aidha, AICC imeanza mchakato wa ujenzi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Mjini Arusha, kitakacho julikana kwa jina la *International Conference Centre - Kilimanjaro*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Chuo cha Diplomasia kimeendelea kutoa mafunzo ya aina mbalimbali ya muda mfupi na mrefu, yakiwemo mafunzo elekezi katika nyanja za utandawazi, itifaki, uhusiano wa kimataifa na diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukipa Chuo sura ya Kitaifa na Kimataifa, Wizara ikishirikiana na Chuo chenyewe, imeanza matayarisho ya kutafuta eneo kubwa la ardhi huko Buma, katika Wilaya ya Bagamoyo, kwa ajili ya ujenzi wa chuo kipyä ili kukidhi mahitaji ya nyanja za kidiplomasia sasa na hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere, kinachotarajiwa kujengwa Jijini Dar es Salaam ni Mradi wa Serikali chini ya ufadhilli wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Mchakato wa ujenzi wa Kituo hicho ulianza kwa Serikali ya China kuwasilisha michoro ya awali ya ujenzi wa jengo hilo mwezi Januari 2009. Kufuatia hatua hiyo, Wizara yangu iliitisha vikao vya wadau muhimu katika ujenzi wa Kituo hicho ili kuipitia michoro ya wasanifu wa majengo (*China Architecture Design and Research Group-CAG*) kutoka China, kutoa maoni na kuwasilisha mapendekezo kwa CAG mnamo mwezi Machi, 2009 kama CAG walivyoomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya ujenzi wa Kituo hiki yanaendelea vyema. Kampuni ya Wasanifu Majengo nichini China (CAG), inaendelea na zoezi la kukamilisha michoro ya kina ya jengo (*Detailed Designs*) na watakapokuwa tayari, wataiwasilisha kwa Serikali ya China. Baada ya hapo, Serikali ya China itatangaza zabuni ya ujenzi wa Kituo hicho ili kumpata mkandarasi. Wizara yangu inaendelea kufuutilia zoezi hili kwa karibu ili kazi za ujenzi zianze mwezi Oktoba, 2009 kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nizungumzie suala la OIC; kama Bunge lako Tukufu na Watanzania wanavyofahamu, Wizara yangu ya Mambo ya Nje ndiye mratibu mkubwa wa mchakato wote wa ama kujiunga au kutokujunga na OIC.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kuwashukuru wale wote ambao wametuletea michango mbalimbali ya kimaandishi na ya mawazo, kuhusiana na mjadala huu wa iwapo tujiunge na OIC au hapana. Michango yote tulioletewa Wizarani tumeipokea, tumeithamini na tumeifanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Jumuia ya OIC kwa sasa inapita kwenye mabadiliko, yaani *Reforms*, yanayolenga kupata Jumuia Mpya, yenye sheria mpya, yenye kanuni mpya, yenye muundo mpya, yaani *Structure and Organization* na masharti mapya ya namna ya kujiunga katika Jumuia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mfumo huo mpya, vitatolewa vigezo na sifa mpya za nani anastahili kuwa mjumbe kamili, yaani *full member* na nani anastahili kuwa Mjumbe wa *Observer Status*. Kamati ya nchi nne, imeundwa na Baraza la Mawaziri wa OIC waliokutana mwezi mei mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii itamaliza kazi yake mwaka 2010 na itawasilisha mapendekezo ya mfumo na muundo mpya wa Jumuia ya OIC na sifa zake na kanuni zake mpya kwenye Kikao cha Baraza la Mawaziri kitakachokutana mwaka 2010 na watawasilisha taarifa hii kwa Kamati ya *Experts*, yaani *Experts working group* ya OIC ambayo itatoa taarifa yake mwaka 2011 kwa Baraza la OIC.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya hapo, Baraza hili litafikisha taarifa kamili kwa Viongozi wa OIC Duniani mwezi Mei mwaka 2012 ili kupitisha muundo, sheria na taratibu mpya ya namna ya kujiunga na OIC.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi ya Philipinnes iliomba kujiunga na OIC mapema mwaka huu, imekataliwa kwa maelezo kuwa Jumuia ya OIC inasubiri mabadiliko makubwa kwanza kabla ya kumkubalia mtu au nchi yoyote kujiunga na Jumuia hiyo. Baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu, pamoja na Watanzania, waelewe mabadiliko haya makubwa yanayolikabili Shirika la OIC.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba sasa, kutokana na mabadiliko hayo, Watanzania wausitishe mjadala huu kwa sababu hauwezi kuuendeleza mjadala wakati chombo chenyewe kinapitia mabadiliko makubwa ya mfumo. Narudia, Watanzania wote hatuwezi sasa kuendelea na mjadala wa namna ya kujiunga au kutokujiunga na Jumuia ya OIC wakati Chombo Chenyewe cha Jumuia hii kinapitia mfumo na mabadiliko makubwa katika kipindi cha miaka miwili ijayo

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiendelea na mjadala huu, maana yake ni kwamba ama mambo mengine tutakayokuwa tunayajadili yatakuwa yamepitwa na wakati au tutakuwa tunajadili jambo ambalo mwaka 2012 halitakuwepo. Tuvute subira na tuombeane turudi Bungeni hadi mwaka 2012, *Inshallah* tukirudi tuendelee na mjadala huu. Ninawaomba Watanzania wavute subira, haya siyo maneno ya Membe ni maneno ya Baraza la OIC, lililotutana Mjini Damascus Syria mwezi mei mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, itakuwa tayari kuwasilisha mbele ya Bunge hili na Mezani kwako Mheshimiwa Spika, Ripoti Maalumu ya Mabadiliko Makubwa ya Shirika la OIC, ambalo tulikuwa tumeanza mchakato wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niombe pesa. Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Wizara yangu ilipangiwa kutumia kiasi cha shillingi 69,405,738,700. Kati ya fedha hizo, shilingi 56,355,164,900 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida; shilingi 10,500,000,000 ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo na shilingi 2,550,573,800 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Balozi zake nje, ilitegemea kukusanya kiasi cha shilingi 11,028,003,000. Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2009, kiasi cha shilingi 11,097,724,950 kilikuwa kimekusanywa. Tunataraja kwamba, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2009, kiasi cha shilingi 12,106,609,036 kitakuwa kimekusanywa. Hili ni ongezeko la shilingi 1,078,606,036, sawa na ongezeko la asilimia kumi zaidi ya makadirio ya makusanyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tatizo la mgogoro wa uchumi duniani lisingekuwepo, huenda balozi zetu zingekusanya mapato zaidi, kutokana na kampeni mbalimbali zilizofanywa na Serikali katika kuvutia wawekezaji, watalii, wafanyabiashara na wageni wengine wa aina mbalimabali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2009, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 81,456,495,024 kutoka Hazina kama sehemu ya mgao wake wa bajeti. Kiasi hiki ni zaidi ya makadirio ya bajeti kwa shilingi 12,050,756,324, sawa na ongezeko la bajeti kwa asilimia 17. Ongezeko hili linatokana na kuporomoka kwa thamani ya sarafu yetu dhidi ya sarafu za kigeni hususan Dola ya Kimarekani, Pauni ya Uingereza, Euro ya Ulaya na sarafu nyinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko hili la Bajeti ya Wizara, linatokana na ukweli kwamba, Wizara yangu hulazimika kutumia zaidi ya asilimia 80 ya bajeti katika matumizi ya fedha za kigeni kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, pamoja na mambo mengine, Wizara yangu imepanga kutekeleza malengo makuu muhimu kulingana na Dira ya Taifa 2025, MKUKUTA, MKUZA, Malengo ya Milenia na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 kama ifuatavyo:-

- (i) Kuendelea kuiletea nchi yetu maslahi ya kiuchumi kwa kuwavutia wawekezaji wenye mitaji na teknolojia ya kisasa na watalii;
- (ii) Kuendeleza Sera ya Ujirani Mwema;
- (iii) Kushiriki katika kuimarisha Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Ukanda wa Maziwa Makuu (GLR), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Umoja wa Nchi za Afrika (AU), Umoja wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote (NAM) na Umoja wa Mataifa (UN);
- (iv) Kuitangaza nchi yetu na kuitetea heshima yake miongoni mwa Mataifa;
- (v) Kuendelea kudai mageuzi katika Umoja wa Mataifa kwa lengo la kuongeza sauti za nchi zinazoendelea;
- (vi) Kujikita katika Diplomasia ya Mikutano;
- (vii) Kuitambua Jumuiya ya Watanzania wanaoishi Ughaibuni na kuweka utaratibu utakaowawezesha kuchangia maendeleo ya Taifa lao; na
- (viii) Kujikita zaidi katika kuhakikisha mikataba yote ambayo Tanzania ni mwanachama inatekelezwa ipasavyo kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kutekeleza kikamilifu kazi zilizotajwa hapo juu, Wizara yangu imepangiwa kiasi cha shilingi 88,002,643,100 kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Kati ya fedha hizo, shilingi 63,917,282,800 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 20,269,113,100 ni kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, shilingi 3,816,247,200 ni kwa ajili ya mishahara. Katika bajeti ya matumizi ya kawaida ya Wizara, shilingi 1,000,000,000 ni kwa ajili ya

mchakato wa APRM, shilingi 2,000,000,000 ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na shilingi 1,306,690,000 ni kwa ajili ya fedha za mishahara na matumizi ya kawaida ya Chuo cha Diplomasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara yangu inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 9,863,298,000 kama maduhuli ya Serikali. Kwa maana ya utekelezaji wa Bajeti, kiasi hiki cha maduhuli tayari kimehesabiwa kama sehemu ya matumizi ya kawaida ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. WILSON M. MASILINGI (MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, inayoshughulikia mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawasilisha taarifa hii, napenda kuchukua nafasi hii, kukupongeza Naibu Spika binafsi, kwa kazi nzuri ambayo umekuwa unaifanya unapopata fursa ya kuwakilisha Bunge letu Nje ya Nchi katika shughuli za Mabunge ya Jumuiya za Madola na katika Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika. Umefanya kazi nzuri sana na mara nyingi unapokuwa nje, unapewa nafasi ya kuongoza kutokana na mchango wako mzuri unaoutoa na kuwakilisha Bunge letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuititia kwako, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Spika, kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, kuwakilisha Bunge letu katika Mabunge ya Nje na kazi anayoifanya akiwa Rais wa sasa wa CPA. Kusema kweli, mmetoa mchango mkubwa kuimarisha heshima ya Bunge letu na Kamati yetu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, yenye dhamana ya kuimarisha ushirikiano wa Bunge letu na Mabunge ya Nje. Kamati inaridhishwa na kazi nzuri mnayoifanya, tunawaombeni shime endeleeni kutuwakilisha vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na kuititia kwake, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanafanya kazi nzuri, iliyotujengea heshima kubwa nchi yetu na hata Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi juzi tu tumetoka Australia, tulikaribishwa ndani ya Bunge la Australia, jambo ambalo siyo la kawaida, mimi na Mheshimiwa Membe na Mheshimiwa Lazaro, viti vyetu viliwekwa ndani ya Ukumbi wa Bunge siyo Ukumbi Maalum wa Spika. Hiyo ni heshima kubwa ambayo wanasema kihistoria ilifanyika kwa kuheshimu mchango wa Mheshimiwa Membe kama Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuimarisha mashiririkiano na nchi za nje; hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia Wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini, kwa kunipa ushirikiano na kunivumilia muda wote ambao nimekuwa hapa. Namshukuru mke wangu mpandwa Marystella na watoto wetu, kwa kunivumilia muda wote ambao

nimekuwa mbali nao nikishughulika na mambo ya Bunge hapa. Nitaendelea kuwaenzi na kuwapa ushirikiano ili tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa na kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114(11), naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo, kwa Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ilikutana tarehe 01 Juni, 2009, kupitia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010. Mheshimiwa Bernad Kamilius Membe, Waziri wa Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Kimataifa, alieleza Kamati kuhusu Sera, Dira, Dhamira na Kaulimbiu ya Wizara. Aidha, Kamati ilielezwa utekelezaji wa majukumu ya Wizara, pamoja na utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao cha tarehe 1 Juni, 2009, Kamati ilielezwa vipaumbele vya Wizara vinavyohitaji mkakati madhubuti wa utekelezaji. Mionganini mwa vipaumbele hivyo ni ununuzi na ujenzi wa nyumba za Serikali katika Balozi zetu nje na kuongeza uwakilishi nje ya nchi. Jambo lingine lililotajwa kuwa kipaumbele ni kuimarisha njia za mawasiliano katika utendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Taarifa ya Wizara inaonesha kuwa, Serikali imefanikiwa kuimarisha uhusiano wa nchi yetu na Mataifa mengine Duniani, pamoja na Mashirika ya Kimataifa na Kikanda, kwa kiwango kikubwa. Tunaamini na kuendelea kuihimiza Serikali iendelee kuhakikisha kuwa, Tanzania ina mahusiano mazuri na Mataifa yote Duniani, pamoja Mashirika ya Kimataifa ya Kikanda, Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa.

Waheshimiwa Wabunge, mmeshuhudia hivi punde taarifa ya kina aliyowasilisha Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, jinsi ambavyo wamefanya kazi nzuri kuimarisha mashirikiano yetu na changamoto ambazo zinalikabili Bara la Afrika hasa kudumisha amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini na kuendelea kuihimiza Serikali iendelee kuhakikisha kwamba, Tanzania ina mahusiano mazuri na Mataifa yote Duniani, Mashirika ya Kimataifa ya Kikanda, Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana, zipo changamoto kadhaa zilizoelezwa kuathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Baadhi ya changamoto hizo ni:-

- (i) Uhaba wa rasilimali watu na fedha;
- (ii) Uhaba wa watumishi wanaokidhi mahitaji ya kukabiliana na changamoto ya Sera ya Diplomasia ya Uchumi;
- (iii) Maslahi duni ya watumishi wetu nje ya nchi; na

(iv) Nafasi na uwezo wa Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kupitia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2009/2010, Kamati hii ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali kwa kuzingatia dira na majukumu yaliyopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika Mwaka wa Fedha wa 2008/2009, Serikali imezingatia na kutekeleza ushauri wa Kamati kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, Serikali imezingatia ushauri kuhusu suala la ujenzi na ununuzi wa majengo kwa ajili ya Balozi zetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri yalionesha kuwa, Wizara imeandaa mpango wa miaka kumi na mitano wa kujenga na kununua kwa awamu, baadhi ya majengo ya Balozi zetu nje ya nchi. Kamati ilielezwa kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, imepanga kununua ghorofa (*floor*) mbili katika jengo moja, kwa ajili ya ofisi za Ubalozi, New York - Marekani. Tunaipongeza Serikali kwa Mpango huo mzuri na kusisitiza kuwa, Wizara hii iwezeshwe zaidi kibajeti ili kutekeleza vyema mpango wake mahususi, utakaosaidia kuongeza maduhuli ya Serikali na kupunguza gharama za uendeshaji wa Ofisi za Balozi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Waziri, sehemu kubwa ya ushauri na maoni ya Kamati ipo katika mchakato wa utekelezaji. Kwa mfano, kuhusu azma ya serikali kuitambua Jumuiya ya Watanzania wanaoishi ughaibuni (*Tanzanians in Diaspora*), Taarifa ya Waziri ilieleza kuwa, Wizara inaendelea na mchakato wa kuanzisha kitengo kitakachoratibu na kushughulikia masuala ya Watanzania wanaoishi ughaibuni. Aidha, ilielezwa kuwa kikosi kazi kinachohusisha wadau mbalimbali kimeundwa ili kutekeleza azma hiyo. Kamati iliambiwa kuwa mchakato huu utakamilika ndani ya kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwengine ambao upo kwenye mchakato ni kuhusu kuziba mapengo ya watumishi katika ofisi zetu za ubalozi. Mheshimiwa Waziri alieeleza Kamati kuwa, katika kutekeleza hoja hii, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, imetangaza nafasi za kazi 15 na kwamba mchakato wa kukamilisha ajira hizo unaendelea. Vile vile, tulielezwa kwamba, Wizara inakamilisha utaratibu wa kuteua Wawakilishi wa Heshima kutoa huduma katika sehemu ambazo hatuna ofisi za kibalozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kueleza Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Waziri alieeleza Kamati kuwa, malengo ya Wizara hii katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, pamoja na mambo mengine ni kutekeleza majukumu muhimu kulingana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005. Malengo hayo ni kama ifutavyo:-

(i) Kuendelea kuiletea nchi yetu maslahi ya kiuchumi kwa kuwavutia watalii na wawekezaji wenye mitaji na teknolojia ya kisasa kutoka nje;

(ii) Kuendeleza Sera ya Ujurani Mwema;

(iii) Kushiriki katika kuimarisha Jumuiya ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki (EAC), Ukanda wa Maziwa Makuu (GLR), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (

SADC), Umoja wa Nchi za Afrika (AU), Umoja wa Nchi Zisizofungamana na Upande wowote (NAM) na Umoja wa Mataifa (UN);

- (iv) Kuitangaza nchi yetu na kuitetea heshima yake miongoni mwa Mataifa;
- (v) Kuendelea kudai mageuzi katika Umoja wa Mataifa kwa lengo la kuongeza sauti za nchi zinazoendelea;
- (vi) Kujikita katika Diplomasia ya Mikutano;
- (vii) Kuitambua Jumuiya ya Watanzania wanaoishi ughaibuni (*Tanzaians in Diaspora*) na kuweka utaratibu utakaowawezesha kuchangia maendeleo ya Taifa lao; na
- (viii) Kujikita zaidi katika kuhakikisha kuwa mikataba yote ambayo Tanzania ni Mwanachama inatekelezwa ipasavyo kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa malengo mazuri yanayopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2009/2010. Kamati inashauri kuwa, utekelezaji wa malengo ya Wizara uendelee sambamba na mtiririko mzuri wa fedha kutoka Hazina ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa malengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri aliiarifu Kamati kuwa ili kutekeleza kikamilifu kazi zilizopangwa katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, imepangiwa kiasi cha shilingi 88,002,643,100. Kati ya fedha hizo, shilingi 63,917,282,800 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, shilingi 20,269,113,100 ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo. Kwa upande wa maduhuli, Kamati ilielezwa kuwa, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 9, 863,298,000 kama maduhuli ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilizingatia Taarifa ya Utekelezaji wa Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010 na kupitia kifungu kwa kifungu, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 34 la Wizara hii na kuyapitisha makadirio hayo ili yawasilishwe Bungeni kwa hatua zinazofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inayo maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

- (i) Kamati inaendelea kusisitiza kwamba Serikali ianzishe Kituo cha Kitaifa kitakachohusika na Ulinzi wa Maslahi ya Taifa (*The National Defence College*), ambacho moja kati ya majukumu yake itakuwa ni kuainisha maslahi ya Taifa, sambamba na kutoa ushauri kwa Watendaji Wakuu Serikalini. Aidha, Chombo hicho kitatoa mwongozo mzuri kuhusu maslahi ya Taifa katika Ushirikiano wa Kimataifa na kusaidia kujenga uhusiano mzuri baina ya Tanzania na nchi nyingine;
- (ii) Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF), liombwe kutoa fedha ya mkopo kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Jengo la Ubalozi wa Tanzania nchini Kenya.

Mheshimiwa Waziri amelitolea taarifa hili kwamba, tayari limekubalika na linatekelezwa na nimeshuhudia kwenye runinga, Mheshimiwa Rais akieleza kwamba, jengo

litakalojengwa Nairobi litakuwa refu na litaitwa Umoja House. Hongera sana na tufikishie pongezi kwa Mheshimiwa Rais, kwa kufanikisha hili.

(i) Tatizo la umiliki wa ardhi kwa Chuo cha Diplomasia kilichopo eneo la Kurasini lipatiwe ufumbuzi haraka kwa kutafuta eneo mbadala ambalo ni kubwa ili litumike katika ujenzi wa Chuo hicho, sambamba na kukiwezesha kuboresha mafunzo yake;

(ii) Serikali iendelee kuimarisha Mahusiano ya Kiuchumi na nchi ya China, Mashariki ya Kati (*Middle East*) na Mashariki ya Mbali (*Far East*) ili kutumia vyema fursa zilizopo katika mahusiano yetu hayo;

(iii) Serikali iendelee kutumia ofisi zetu za ubalozi nje ya nchi katika kuimarisha Diplomasia ya Uchumi ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wawekezaji katika nyanja ya Kilimo. Kaulimbiu ya kilimo mwaka huu ni Kilimo Kwanza, Utalii, Reli, Madini, Nishati na Bandari;

(iv) Serikali ione umuhimu wa Balozi zetu kuwezesha ili kuratibu ushiriki wa nchi yetu katika Maonesho ya Biashara yanayofanyika nje ya nchi;

(v) Serikali iendelee na msimamo wake wa kutaka uimarishaji wa ushirikiano wa kikanda kabla ya hatua ya kuwa na Serikali moja ya Afrika;

(vi) Ofisi zetu za Ubalozi nje ya nchi ziboreshe huduma zake kwa Watanzania wote na kujiimarisha kimtazamo ili kuwawezesha Watanzania wanaoishi ughaibuni (*Diaspora*), kushiriki kikamilifu katika kuchangia shughuli za kiuchumi na kijamii hapa nchini;

(vii) Serikali ihakikishe kuwa Ofisi zetu za Ubalozi nje ya nchi zinakuwa na takwimu za Watanzania wote wanaoishi katika nchi hizo; na

(viii) Serikali iboreshe utaratibu wa kupitia Mikataba ya Kimataifa iliyosainiwa ili kuongeza ufanisi katika uridhiaji na utekelezaji wa Mikataba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuhitimisha kwa kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa fursa hii muhimu ili niweze kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, inampongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhudi zake kubwa katika kudumisha mahusiano mazuri na nchi zote za Afrika Mashariki, Maziwa Makuu na Mataifa mengine Duniani. Rais Kikwete, amefanikiwa kwa kiasi kikubwa, kuendeleza uhusiano mzuri baina ya nchi yetu na Mashirika ya Kimataifa ikiwemo Umoja wa Mataifa. Tumesikia taarifa na heshima tuliyopewa, Rais wetu amekutana na Rais Barrack Obama, Raia wa Marekani, akiwa Rais wa kwanza kwenda Ikulu ya Marekani; si jambo dogo hili wengi wanakwenda wanaishia mjini tu. Mafanikio haya yameipatia nchi yetu heshima kubwa nje ya nchi. Kamati inaamini kuwa, Serikali ya Awamu ya Nne, chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, itaendelea kudumisha na kuimarisha heshima hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawashukuru Mheshimiwa Bernad Kamillius Membe, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Balozi Seif Iddi, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Ndugu Sethi Kamuhanda, Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara, Mabalozi na Watendaji wengine wa Wizara, kwa ushirikiano na utendaji makini wa majukumu yao. Aidha, tunashukuru kwa maandalizi mazuri ya taarifa zenye ufanuzi wa kina. Kamati inaridhishwa na kupongeza ushirikiano na uchapakazi wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wasaidizi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati yangu kwa ushirikiano, busara na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua kwa kina Bajeti ya Wizara hii. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Col. Mst. Saleh Farrah, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Hassan Kigwagilo, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Dokta John Samwel Malecela, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Col. Mst. Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Dokta Ibrahim Msabaha, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Thomas Mwang'onda, Mheshimiwa Brig. Jen. Mstaafu Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na Mheshimiwa Magalle Shibuda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, kwa msaada mkubwa kwa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawashukuru sana Makatibu wa Kamati; Ndugu Athuman Hussein na Ndugu Stella Mlambo, kwa kuihudumia vyema Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kama yalivyowasilishwa na mtoho hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa nitamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA): Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba nitoe maneno machache ya Utangulizi kabla ya kusoma hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia nafasi hii, kukupongeza wewe na wote wanaosimamia shughuli za Bunge hapa, kwa kazi yenu nzuri ambayo kwa kweli imeijengea sana heshima kubwa nchi yetu na Bunge letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba niishukuru Serikali, pamoja na kuwa muda mrefu imechelewa kufanya shughuli hiyo, lakini sasa imeonekana kipindi cha pili inajaribu kutenga pesa za maendeleo kwa Wizara hii, kitu ambacho kitasaidia sana katika kukamilisha majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, napenda niseme kama ifuatavyo:-

Napenda kutoa shukrani kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kwa kunipa fursa hii ili kutoa maoni ya Kambi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kifungu cha 99(7), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa neema na rehema, kwa kutujaalia afya njema na uzima. Aidha, nachukua fursa hii, kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Gando, kwa kuendelea kuniamini na kuniunga mkono kwa dhamana hii nzito waliyonipa ya kuwawakilisha katika chombo hiki nyeti.

Mheshimiwa Spika, pia natoa shukrani zangu za dhati kwa Viongozi wetu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi na Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Willibrod Slaa, Mbunge wa Karatu, kwa kutoa mwongozo sahihi kwa Kambi kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. Pia nawashukuru wenzetu wote katika Kambi ya Upinzani, kwa msaada na maelekezo mazuri waliyonipa wakati wa kuandaaa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kumshukuru sana Waziri wa Mambo ya Nje, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa ushirikiano wanaonipa wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya tatizo kuu linalorudisha nyuma maendeleo ya nchi nyingi ni kuwepo kwa ubadhirifu wa fedha wa hali ya juu. Ubadhirifu huo huonekana katika sura mbalimbali, zikiwemo masurufu yasiyorejeshwa, matumizi ya fedha bila ya kufuata utaratibu, matumizi ya fedha yasiyo na hati au maelezo ya kutosha, upotevu wa fedha, upotevu wa vifaa na matumizi ya fedha za umma kwa maslahi binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2008, iliyotolewa Machi, 2009, ipo tuhuma ya matumizi mabaya na ubadhirifu wa fedha katika baadhi ya Ofisi za Kibalozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano; jumla ya Balozi mbili zilipata hati za ukaguzi zisizoridhisha; Balozi nane hati za ukaguzi zenye mashaka; na Balozi 19 zilipewa hati inayoridhisha, lakini zenye masuala ya msisitizo. Balozi tatu tu za Riyadh-Saudi Arabia, Harare-Zimbabwe na Maputo-Msumbiji, ndizo zilizopata hati inayoridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ubalozi wetu nchini Marekani, Washington, ulifanya manunuzi ya huduma jumla ya Sh. 18,459,370 bila ya idhini ya Kamati ya Manunuzi. Kwa ujumla, ipungufu ni mwangi katika Balozi zetu, kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa ufupi tu, Balozi zilitumia fedha zaidi ya makisio yaliyoidhinishwa jumla ya Sh. 7,914,996,040.27.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuwa, hadi enzi hizi za ushindani mkubwa wa kidiplomasia, bado Wizara hii inaendelea kuathirika na tatizo la uajiri wa watumishi ambao

baada ya muda mfupi, huthibitisha upungufu mkubwa katika uwezo kama ilivyojitokeza katika Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, utashi na uzalendo wao katika kutekeleza wajibu wao wa kutafsiri, kutetea na kulinda maslahi yetu kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona hapa inawezekana kabisa, Balozi zetu nyingi zina upungufu wa wafanyakazi wenye kiwango sahihi cha uhasibu. Vinginevyo, tunamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufanuzi kuhusiana na upungufu huo kama tulivyoeleza hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tulishauri katika Hotuba yetu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwamba, nafasi za uwakilishi wa nchi yetu nje ya nchi, yaani Mabalozi, kuwa Bunge chombo kinachowakilisha wananchi, kipewe nafasi kubwa kwa utaratibu ambao tulieleza kwa undani, tunaendelea kusisitiza tena kuwa ufuatwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa, kwa kufanya hivyo, ile tabia na dhana ya umwenzetu itaachwa. Kwa hali halisi ya sasa ni wazi kuwa, wapo watendaji ambao uwezo wao wa kazi unatiliwa mashaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, imeonesha kuna malipo ya kutilia mashaka makubwa kwa huduma na manunuzi katika Wizara jumla ya Sh. 241,603,906.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iangalie kwa makini matumizi ya Wizara, kama tulivyosema hapo awali kuwa, Wizara hii ni kubwa na inatakiwa kuwa kioo cha Wizara nyingine kiutendaji. Hivyo basi, tunamtaka Mheshimiwa Waziri, alieleze Bunge hili ni kwa nini wale wanaotumia vibaya fedha za walipa kodi bila kufuata taratibu na kanuni wananyamazishwa? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya chanzo muhimu cha mapato ndani ya Wizara hii ni uuzaaji wa *Visa* kwa Wageni waingiao nchini. Mapato haya ni muhimu kwani husaidia kuiwezesha bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeamua kupunguza viwango vya ada ya *Visa* na kuwa na kiwango kimoja cha Dola 50, bila ya kuangalia kuwa wageni wanatoka nchi zipi. Kambi ya Upinzani ina uhakika kuwa, viwango vya *Visa* kwa nchi mbalimbali ni makubaliano baina ya nchi hizo. Aidha, mapato hayo ya *Visa* hutumiwa na Balozi zetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inahitaji kuambiwa kuwa badiliko hili litaipunguzia Serikali mapato kiasi gani na Balozi zitafidiwa vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelewa kuwa Tanzania imepata heshima kubwa kutokana na msimamo wake usiroyumba unaohusiana na suala zima la haki za binadamu, ambalo msingi wake uliwekwa na Baba wa Taifa, Marehemu Julius Kambarage Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na mtafaruku mkubwa na maoni tofauti juu ya uanzishwaji na utendaji wa Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Uhaliwa Kivita (ICC). Sasa hivi kuna mtafaruku mionganoni mwa wanachama, juu ya kukamatwa na kushtakiwa katika Mahakama hiyo kwa Rais Omar El- Bashir wa Sudan, kutokana na mauaji makubwa ya kikatili yaliyofanyika Darfur.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka kusikia msimamo wa Serikali kuhusiana na kukubaliana na kazi zitakazokuwa zinafanywa na Mahakama hiyo au inapingana na utendaji kazi wa Mahakama hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ina wasiwasu kuwa, pamoja na kuwa nchi za Bara letu zinapaswa kuheshimiwa kama nchi zeny mamlaka kamili, lakini tabia mbaya za baadhi ya viongozi wa nchi hizi za kusababisha uhalifu na udikteta kiasi cha kufikiri kuwa nchi wanazotawala ni mali yao, zisipokemewa kwa nguvu zote, basi madhara makubwa yanaweza kusambaa katika Bara lote hadi kwetu sisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imetia saini Tamko la Ulimwengu juu ya Haki za Binadamu (*Universal Declaration of Human Rights*), vile vile imeridhia mikataba mikubwa ya Kimataifa ya Haki za Binadamu. Hivyo basi, Tanzania ina jukumu la kuhakikisha kuwepo kwa misingi ya haki za binadamu kupitia mikataba ya Kitaifa na Kimataifa. Cha kushangaza ni kuwa, kumekuwepo na tofauti kubwa kati ya sera na utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mionganoni mwa haki ya msingi ya binadamu kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu, ni haki ya kuchagua na kuchaguliwa. Haki hii inavunjwa waziwazi tena kwa kiburi kikubwa hapa kwetu. Wananchi wengi wanakoseshwa kupiga kura katika chaguzi mbalimbali zinazosimamiwa na Tume ya Uchaguzi na hili linathibitishwa na vitendo vinavyofanyika hivi sasa Kisiwani Pemba katika kile kinachoitwa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wengi waliokwishafikia umri wa miaka kumi na minane na zaidi, hawakuandikishwa kupiga kura katika Jimbo la Konde na kwingineko. Hivi tunakwenda wapi; ni kweli nchi yetu inafuata na kutekeleza misingi ya kulinda haki za binadamu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Niabu Spika, umuhimu wa kuwashirikisha Watanzania walio nje ya nchi yetu katika masuala mbalimali ya maendeleo ya nchi ni suala ambalo linapaswa kutiliwa mkazo. Tunaamini kuwa tunapokuwa na mazingira mazuri na rasmi ya kuwashirikisha ndugu zetu hawa katika masuala ya kisiasa, kijamii na kiuchumi, tutakuwa si tu tunatekeleza jukumu la kuwapa haki yao walivyonyimwa kwa muda mrefu, lakini pia tunaongeza nguvu katika juhudhi za kufanikisha maendeleo ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha Jumuiya za Watanzania walioko nje ni hatua nzuri ya kuanzia, lakini pia ni wajibu wa Wizara hii kuhakikisha kuwa, wanajenga mazingira yanayohitajika kuwawezesha ndugu zetu hawa kutoa mchango wao kwa maendeleo ya Taifa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nyanja mbalimbali za kitaaluma, upo ushahidi kuwa, katika nchi jirani zenu wapo vijana wengi wa Tanzania ambao wanatoa huduma mbalimbali kama vile Uhndisi, Udaktari, Unesi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wote na wengine wengi ni hazina kubwa ambayo tunashindwa kuitumia ipasavyo, kutokana na utamaduni wetu wa kuogopa maamuzi mazito kama ambavyo unagubika mchakato wa uraia wa nchi mbili hapa nchini. Kuwa na sheria inayoruhusu kuwa na uraia wa nchi mbili, kutawezesha na kurahisisha ushiriki wa Watanzania waishio ughaibuni katika kulinda, kutetea na kujenga Taifa lao. Hivi kuna tatizo gani hasa linalokwamisha suala hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni muda mrefu sasa tokea suala ambalo Mheshimiwa Waziri sasa hivi ametuomba tulinyamazie la OIC lianze kuzungumzwa. Kambi ya Upinzani inapenda kujua ni hatua gani zimefikiwa na amezieleza lakini mimi hapa ningependa niseme kuwa, hili ndiyo tatizo la kusubiri jambo jema kwa muda mrefu, matokeo yake utastukia unakwama bila ya sababu za msingi. Mpaka sasa haijaamuliwa ama kujiunga Tanzania yenewe au Zanzibar kama sehemu ya nchi, ambayo ina matatizo makubwa ya kiuchumi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii iliahidi kuanzisha Mabalozi wa Hesima (*Honorary Councilors*), katika kanda na nchi mbalimbali ili kupunguza gharama za matumizi ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunaelewa jinsi nchi yetu ilivyo kubwa na namna tunavyokabiliwa na uchache wa fedha. Kwa msingi huo, kila juhudini inahitajika ya kupunguza matumizi. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inauliza, hadi sasa Waziri analieleza nini Bunge hili juu ya utekelezaji wa ahadi hiyo ingawa katika maelezo yake ametoa maelezo ya kiasi fulani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Diplomasia kimefanya kazi kubwa ya kuwaelimisha vijana na watumishi mbalimbali katika nchi yetu. Hata hivyo, bado haionekani kuwa Wizara inachukua juhudini za makusudi za kukipandisha hadhi Chuo hiki, pamoja na kelele nyingi ambazo Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama na watu wengine wanazopiga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inauliza kinachokwamisha ni nini hasa? Vyuo vikuu vyetu viro na vina uwezo na hadhi kubwa. Sasa ni wakati muafaka wa kukamilisha dhamira hii nzuri ili Chuo hiki kifanywe Tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na hivyo shahada zake ziweze kutambulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania iliridhia Azimio la Nchi Huru za Kiafrika la Kujifanya Tathmini Katika Sekta Mbalimbali za Kiutawala na Kiuchumi, yaani *Africa Peer Review Mechanism*. Mheshimiwa Rais aliteua Baraza la Uongozi la Taifa na wamekuwa wakisimamia zoezi la mchakato wa kujitathmini, lakini hadi sasa Baraza hilo halijazinduliwa na hilo ni sharti katika kujua uhalali wake na hata ripoti yake iwe na ithibati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato huu unaendelea vyema, pamoja na changamoto nyingi hususan za kutokupewa fedha kwa wakati, imepelekea hadi sasa taarifa hiyo kutokukamilika. Hivyo basi, nchi yetu ione umuhimu wa mpango huu kukamilika katika muda mfupi ujao, kwa kuwawezesha kadiri ya mahitaji yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inafahamu zoezi hili lina gharama kubwa, lakini ni matumaini ya Watanzania kwamba, kama kazi hii itafanywa kwa uadilifu na uwazi, itasaidia Taifa kujitambua tumetoka wapi, tumefika wapi na tunakwenda wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato huu utadhihirisha pia mafanikio na upungufu. Ni matumaini ya Kambi ya Upinzani kwamba, yale yote yatakayoonekana kama upungufu tuwe na utashi wa kisiasa wa kujisahihisha na kujipongeza pale tulipofanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaamini kwamba, tathmini hii haitafumbia macho kuyaona yale yote ambayo yanahatarisha umoja, mshikamano na muungano wetu na kutoa mapendekezo bora kwa ustawi wa Taifa letu. Tunaamini pia taarifa hii itakapokamilika, itakuwa wazi kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo na kwa sababu naamini Mheshimiwa Waziri atatoa majibu na Serikali itafuatilia, naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawaita wachangiaji, naomba niwatambue wageni ambao tunao ndani ya Bunge letu.

Kwanza, ninao wageni wa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernard Membe, ambao kwanza kabisa ni mpendwa mke wake Docas Membe, ambaye pia anao watu kutoka Jimboni kwake na Wilayani kwake. Yuko Mwenyekiti wa Chama, nafikiri Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Lindi, Bwana Ali Hassan Gwaja. Yupo Katibu wa Chama Wilayani huko, Ndugu Ahmed Nyama; yupo Bwana Issa Nyambala Mwenyekiti wa Jimbo la Mtama; yupo Bwana Athumani Ngoboko, Katibu wa Jimbo; yupo Bwana Said Matanje, Katibu Mwenezi Wilaya ya Lindi. Karibuni sana. Viongozi hawa wamefuatana na Makatibu Wenezi, pamoja na Makatibu wa Uchumi na Fedha wa Jimbo la Mtama. Karibuni sana, nadhani mnafanya kazi nzuri ya kukisimamia Chama cha Mapinduzi huko. (*Makofi*)

Halafu tuna maafisa 39 wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, wakiongozwa na Mabalozi wao, ambao ni Balozi Seti Kamhanda, Balozi Francis Malambugi, Balozi Degumja Taja, Balozi Alex Masinda, Balozi Radhia Msuya namfahamu sana, Balazo Mohamed Hamza na Balozi Herbert Mrango. Mabalozi wengine ambao hawajatambulishwa walikuwa nje sasa wamerudi nyumbani, lakini tunapokwenda safari huwa tunapata msaada mkubwa kwao popote wanapokuwa, nadhani hili halijatamkwa ni kweli tunawashukuru sana.

Wako pia wageni 34 wa Waziri wa Mambo ya Nje kutoka Jimbo la Mtama Lindi. Walikuwepo Waenezi wale halafu kuna wengine, nadhani watakuwa *Basement*, kwa sababu nafasi haitoshi.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Idd Azzan, Mbunge wa Kinondoni kutoka Ng'alue Charity Organization; naomba wasimame walipo. Wametajwa majina, yupo Ramadhani Juma, Peter Jacob Karunge, Asteria Herbert Kisanga, Fred Mbago na Maulid Kibarabara. (*Makofi*)

Halafu wapo wageni wa Mheshimiwa Eng. James Alex Msekela, ambao ni Diwani wa Kata ya Mabama, nadhani Jimbo la Tabora Kaskazini, anaitwa Kilugwe Tengeneza Chenji. Yuko wapi huyu; ahsante anatengeneza kabisa. (*Kicheko*)

Yuko Mwenyekiti wa Baraza la Milenia kule Tabora, kuna kijiji kimechaguliwa kuwa cha Milenia, Ndugu Jafari Kapona. Ahsante sana. Halafu yuko Mhandisi wa Mradi huo wa Milenia, Stanley Kayabo. Ahsante. Yuko Mratibu wa Maendeleo wa Mradi anaitwa Osanga Kasela; naye asimame. Halafu wapo Wajumbe wa Baraza la Kijiji hicho, nafikiri cha Milenia hebu wote wasimame wako wengi tu, kama wako ndani wasimame wote walipo. Kwa hiyo, hicho ni kijiji cha mfano, tunakisikia tu labda siku nyingine Kamati zetu ziende zikatembelee zikajifunze hiki Kijiji cha Milenia kikoje. Kipo Tabora katika Jimbo la Tabora Kaskazini. Kwa hiyo, Kamati zinazohusika, siku moja mkatembee mkaone.

Wageni 80 wa kikundi cha akina mama wajane, lakini hawajaniambia wametoka wapi. Hawa akina mama wajane wote walipo wasimame. Jamani wako 80 nadhani wanatoka sehemu mbalimbali. Karibuni sana, jipeni matumaini, Serikali na nchi yenu inawaangalia. Maisha ni kazi na ni kuhangaika, lakini bila kukata tamaa. Kukata tamaa kusiwepo, nawaomba sana na karibuni sana.

Halafu tunao wanafunzi 44 wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Huruma na walimu wao wanne kutoka Dodoma. Wanafunzi na walimu wasimame. Hii Huruma ni shule ya masister, wakati fulani mlishiriki katika kusimamia Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi; karibuni sana. (*Makofi*)

Halafu yupo Dkt. Leonidas Mshokorwa, yeye ni Katibu Mkuu wa Sekretarieti ya Muungano wa Vijana Barani Afrika, ofisi yake iko Algeria. Ndugu Mshokorwa karibu sana; amekuwepo huko miaka mingi na alikuwa Mjumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Vijana, ambapo sisi tulifanya naye kazi tukiwa Wajumbe wa Baraza hilo miaka hiyo. Karibu sana, tunafurahi kukuona. (*Makofi*)

Kuna wengine sijapewa majina yao, lakini naomba niwatambue hasa walio katika Gallery ya Spika; mnakaribishwa sana, maana wanaokaa kwenye Gallery ya Spika kwa kweli ni Wageni wa Spika. Kwa hiyo, nawakaribisha sana hata kama majina sinayo, naona kuna Masheikh pale. (*Makofi*)

Tunao wageni wa Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, nadhani ndiyo wataingia hapa; ni Ndugu Milisenti Obaso, *Country Director USAID*; karibu sana. Huyu mama ni mwenzetu, kwa hiyo, mambo mazuri. Kuna Rev. Dkt. Benjeman Nzimba, *Retired Archbishop of Kenya Anglican Church*. Ahsante karibuni sana. Kumbe nilikuwa nimewaruka tu. Yuko Canon Gideon Biamngisha, yeye anatoka Uganda; karibuni sana tumefurahi kuwaoneni. (*Makofi*)

Yuko Lediana Rwechungura, *HIV Aids Senior Advisor USAID*, anaishi na VVU. Wabunge wote mnamfahamu, kwa muda mwingi sana amekuwa na sisi hapa toka miaka ya nyuma kabisa alikuwa anafanya kazi ya kutuelimisha kuhusu mambo ya kupambana na UKIMWI. Yeye mwenyewe ni mwathirika na kwa taarifa yenu, miaka miwili iliyopita amepata twins, wana miaka kama miwili sasa ni wazima hawajaathirika na ni wajukuu zetu. Kwa hiyo, jamani kuishi na VVU siyo kwamba wewe ni *hopeless case*; amezaa watoto hawa akiwa na *HIV*, lakini ni wazima hawana maambukizi ya Virusi. Nasema hili kwa sababu yeye mwenyewe huwa anajitangaza hivyo, hana matatizo ya kuona aibu. Kwa hiyo, habari ya kunyanyapaa watu, kukata tamaa, haina msingi; huu ni ugonjwa unaoweza kuepukwa kwa namna yoyote ile. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Lediana karibu sana, nadhani tutaonana baada ya kikao hiki, kwa sababu ni rafiki yangu, sikujua kama upo.

Tunaye Sheikh Ruwuche, yeye ni Katibu wa Msikiti wa Nunge Dodoma; karibu sana. Halafu kuna Sheikh wa Bakwata Mkoa wa Tanga; majina yanafana na yeye ni Sheikh Ruwuche hivyo hivyo. Naona majina yote yanafanana; karibuni sana Masheikh. (*Makofi*)

Tunaye Rev. Nicolas Bernard Kimario, huyu ni wa *Evangelist Assemblies of God Tanzania*; na yeye pia anaishi na VVU. Karibuni sana. Hongera sana kwa kuweza kutupa moyo.

Kuna Evangelist Fedeli Mbiha, *Baptist*, yeye anatoka Kigoma naye pia anaishi na VVU. Ahsante sana karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, hawa wageni wetu leo ni wa kutupa matumaini hasa waliokaa katika *Speakers Lounge*. Wanatupa matumaini kwamba, watu wanaweza kuishi na matatizo hayo ilimradi wakiwa na matumaini.

Matangazo ya kazi; Mheshimiwa Estherina Kilasi, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, leo tarehe 18 Julai, 2009, baada ya kipindi cha Bunge kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi Namba 227. Hivyo, Wajumbe wote wanaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Kwaangw', yeche anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kuwa, leo tarehe 18 Julai, kutakuwa na Kikao cha Kamati kitakachofanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa (b), mara baada ya kuahirishwa kwa Kikao cha Bunge asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa matangazo. Wakati ule nilikuwa nimesema baada ya matangazo tutawaita watakaochangia. Tunao wachangiaji wetu; yupo Mheshimiwa Kidawa Salehe, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Riziki Omar Juma na Mheshimiwa Magale Shibuda.

MHE. KIDAWA HAMID SALEHE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ambayo iko Mezani hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kutoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwa bajeti nzuri waliyoandaa. Bajeti ambayo imekuwa na taarifa zote muhimu, ambazo Wabunge tunapaswa kuzielewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Nje ni Wizara muhimu sana kwa nchi yetu, kwa sababu ndio inayotunganisha nchi yetu na nchi nyingine zote za Ulimwengu, pamoja na Jumuiya za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ndiyo Wizara ambayo inaonesha taswira na mandhari ya nchi yetu ya Tanzania katika nchi za Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, Wizara hii inatakiwa ipewe mtazamo wa kipekee kibajeti, kwa sababu kama nilivyosema ni Wizara muhimu na vile vile imetoe viongozi wakubwa tu wa nchi. Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, ametokea katika Wizara hii na pia imetoe Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Mheshimiwa Rose Migiro. Hii ni Wizara muhimu, ambayo imeweka historia ya nchi yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hii ni lazima hadhi ya nchi yetu ionekane huko nje, Rais wetu anakubalika sana siyo tu ndani ya nchi lakini anakubalika nje ya nchi, kwa vigezo vyote ambavyo kwenye Hotuba ya Bajeti vimezungumzwa. Tumepata nafasi nzuri sana na tunapongeza kwa hilo, kwa kuwa Rais wetu amekuwa ni Rais wa kwanza kutoka Bara la Afrika, kualikwa na Rais Obama. Wamekaa pamoja wamezungumza, haijapata kutokea. Wengine wametuonea wivu wamelalamika, lakini ukweli ndivyo ulivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana ya kuonesha taswira ya nchi yetu, tuangalie vyema Balozi zetu kwa sababu ndizo zinazoonesha picha halisi ya nchi yetu. Balozi zilizokuwa nchi za nje, ndiyo Tanzania yenyewe ndani ya zile nchi. Viongozi wetu wanakubalika wakienda nje, lakini zikionekana zile Balozi ziko katika hali mbaya wale hujiuliza huyu ni Kiongozi wa Tanzania ile inayojulikana! Huyu ndiyo kiongozi ambaye tunamwona ni mwadilifu, mwenye demokrasia ya kutosha ndani ya nchi yake; kwa nini Ubalozi uko namna hii? Hii inatudhalilisha na kuonekana duni katika nchi za nje.

Nimeona kuna fedha zimetengwa, lakini hazitoshi kwa sababu kuna Balozi zaidi ya 20 nchi za nje ziko katika hali mbaya. Kuna Balozi nyingine zimepasuka, zina mipasuko mikubwa; yule mtoto mdogo ambaye hawesi kulinganisha mlango ni upi na mpasuko ni upi, anaweza akapita kwenye mpasuko akadhami ndiyo mlango wenyewe. Hizo ndiyo Balozi zetu. Nyumba za Mabalozi ni mbovu, Mabalozi wengine wanapata hata aibu kukaribisha wageni katika nyumba zao, wanaonekana labda Mabalozi wa Tanzania hawako *social* hawakaribishi watu; lakini anaangalia ni nyumba ipi ampeleke mgeni!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba sana mwaka ujao hizi fedha za maendeleo ziongezwe ili tuweze kukarabati Balozi zetu na tuweze kujenga nyumba za Balozi zetu, ambazo umiliki wake uwe ni wa Tanzania. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo upo na inawezekana tukijipanga vizuri katika kupanga bajeti yetu na tukitoa umuhimu wa shughuli hizo za kujenga Balozi zetu, hali ya Balozi zetu itabadilika.

Balozi zetu zimesambaa katika nchi mbalimbali za Ulimwengu, ingekuwa Ubalanzi uko nchi moja tungesema taswira ya Tanzania itaharibika kwa nchi moja tu, lakini zimesambaa katika Mabara yote. Tuna Balozi katika Nchi za *Asia*, *Europe*, Marekani na Afrika. Kwa hiyo, picha ya Tanzania inaharibika katika ulimwengu mzima. Kuna Balozi nyingine, kwa mfano, Ubalanzi wa Tokyo, wanaweza kufanya kazi zao wakati wa kiangazi tu, wakati wa mvua Ubalanzi unavuja, inabidi wafanye uswahili wa kuchukua mabeseni kukinga maji yanayomwagika kutoka juu. Siyo kitu kizuri!

Kuna nyumba zetu za Maputo tena ziko katika *prime area*, zinaona aibu zile nyumba zenye kwa sababu hazilingani na majengo yaliyokuwepo pale; majengo yote ni mazuri, lakini lile la kwetu linaonekana kama nyumba ya kawaida ya tembe, ambayo imejengwa pale. Kwa hiyo, mgeni anaiona haraka haraka na kuuliza hizi ndiyo nyumba za Ubalanzi wa Tanzania? Kungekuwa na uwezekanao wa kuweza kuzihamisha zile nyumba zikang'olewa zikapelekwa huko geto vijijini zikawa sawa sawa na zile nyingine, basi ingelikuwa ni bora zaidi kuliko pale zilipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tujitahidi na inawezekana kutengeneza Balozi zetu kwa kuzijenga upya, kuzikarabati na kujenga majengo mapya. Kujenga jengo jipya na ukarabati mkubwa siyo jambo la siku zote. Ukishaweka bajeti, ukijenga jengo basi linakuwa liko pale linadumu kwa muda mrefu, itabakia ukarabati mdogo mdogo ambao hautahitaji fedha nyingi. Kwa hiyo, tujifunge mkanda, tuijandae tuweke fedha za kutosha, tufanye ukarabati wa Balozi zetu. Kama si hivyo, tutaendelea kuaibika na kuwa duni na kumdhahilisha Rais wetu, Mawaziri wetu na Viongozi wetu, wanaotembelea nchi za nje. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nije katika Idara ya Mambo ya Nje kule Zanzibar. Kule Zanzibar tunayo Idara, tunaipongeza nayo inafanya kazi nzuri, lakini kuna mambo muhimu ambayo yanatatiza utendaji wao wa kazi. Kwa mfano, kuna upungufu wa watumishi wanaofika 10; kazi zimeongezeka utandawazi na utangazaji wa Tanzania yetu nchi za nje umeongeza; watu ambao wanapenda kutembelea Tanzania kutokana na amani iliyokuweko ndani ya nchi yetu wamekuwa wengi tu.

Sasa kukiwa na upungufu wa watendaji, ina maana wale wachache waliokuwepo wanabeba mzigo mkubwa kwa kuwafanya kazi wale ambao hawajaajiriwa. Kwa hiyo, tuangalie tatizo ni nini; kwa nini hatujiri? Hakuna watu ambao wako *qualified* kwa hizo nafasi au hatuna fedha ama mipango tu bado haijaka sawa ya kuruhusu kuajiri? Kwa hiyo, tuangalie kwa mapana yake ili kuweza kuajiri hawa watu na kuwapunguzia mzigo wale ambao wapo.

Vile vile kuna magari mawili tu kule; gari la Mkurugenzi na la pool, ambalo pia ndiyo wanalobebea wageni. Sasa wakifika wageni gari lile la kubebaa wageni ni bovu, lenyewe ni spana mkononi, liende kilomita moja lisimame ligongwe lifunguliwe halafu ndiyo liende tena. Gari hilo kweli utampakia mgeni; si ndiyo kujidhalilisha nilikokutaja mwanzo? Kwa hiyo, hebu tuangalie uwezekano, wakanunue magari mengine. Sasa hivi kinachofanyika, akitokea mgeni, Mkurugenzi anahama kwenye gari lake anampakia mgeni yeye anapanda kwenye lile gari bovu. Dereva aliyemchukua mgeni inabidi aende *speed* ndogo ndogo ili wafanane na lile gari bovu ili isiwe mgeni anafika anakopelekwa, mfano anapelekwa Ikulu, mwenyeji wake hajafika; itakuwa ni kichekesho. Kwa hiyo, inabidi waende mwendo wa jongoo ili waweze kufika pamoja.

Ni mambo madogo, lakini yanatuharabia, tuyaangalie hayo. Tutafute magari ya wageni yaliyo mazuri ili mgeni akifika afurahi, aseme Tanzania Zanzibar nimepata mapokezi mazuri kweli kweli. Aseme nimepatiwa yote ambayo mgeni anahitaji kupatiwa. Wasitoke tena na malalamiko na picha mbaya, wakaona wamedharauliwa wamepakiwa kwenye gari bovu. Haiwavutii mara nyine kurudi tena. Mgeni akija akaribishwe vizuri ili akienda kwao awe na hamu ya kurudi tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna jengo la ofisi, hii idara imekuwa na bahati mbaya, inahama hama kama mtoto wa paka; jengo walilokuwemo sasa hivi ni jengo la tatu, lakini nalo tumeazimwa na SMZ, tunashukuru kwa kuwa tumeazimwa, lakini nalo linahitaji ukarabati. Nataka kujua je, katika hizi shilingi 2.2 bilioni zilizotengwa katika matumizi ya maendeleo na sehemu ya kulikarabati lile jengo imo kama haimo ni kwa nini au mtalipangia lini kulikarabati? La msingi vile vile tuombe watu wa SMZ watupatiate kiwanja, lijengwe jengo la Idara ya Mambo ya Nje tu, tusiazimwe; jengo hilo liwe mali ya Wizara ya Mambo ya Nje. Mbona wengine wameweza, kuna Jengo la *BoT*, Mambo ya Ndani wana ofisi yao nzuri tu pale; kwa nini Wizara ya Mambo ya Nje ishindwe kufanya hivyo?

Kwa hiyo, nadhani Serikali haitashindwa, lakini kuwe na dhamira na jitihada ya kutafuta fedha za kujenga jengo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia katika matumizi ya kawaida, kifungu cha mafuta kwa Idara ya Mambo ya Nje Zanzibar, kimepunguzwa kwa asilimia 50 kulinganisha na bajeti ya mwaka jana 2008/2009. Najiuliza kulikoni kwa sababu kazi zinaongezeka, tumesema wageni wanakuja wengi, mambo muhimu mengi tu ya kufuatiliwa; sasa imekuwaje mwaka huu ipunguzwe kwa kiasi kile? Kweli kuna mtisikiko wa uchumi; lakini mbona kiasi kikubwa kimepunguzwa na wakati shughuli zinakua?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ambalo halina bajeti kabisa, ni suala la mawasiliano na taarifa, kifungu hiki kabisa hakikuwekewa fedha. Tunasema tupo kwenye karne ya 21 ya sayansi na teknolojia na mambo ya *internet*, mamabo ya *database*, mambo chungu nzima ya mawasiliano ambayo ni muhimu, sasa kwa nini hakikuwekewa pesa, tunataka turudi kule kule kufanya hesabu zetu kwa vidole? Mambo hayo yameshapitwa na

wakati. Kwa hiyo, suala la mawasiliano ni muhimu kama ilivyokuwa muhimu mambo mengine yote ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda nitoe pongezi kwa Balozi zetu huko nchi za nje, kwa kuitangaza vizuri Tanzania yetu, kwa kutusaidia kutafuta masoko ya mazao yetu. Kwa hali ngumu hiyo hiyo waliyonayo lakini wanajitahidi sana. Hivi sasa kuna matunda ambayo yanapendwa sana nchi za nje ukienda utayakuta kwenye hoteli mbalimbali kama vile makarakara, maparachichi ambayo kwa kwetu ni mazao mapya, lakini watu wanajitahidi sana kulima na hayo watutafutie masoko huko nje na sisi wanasiwa humu ndani tutajitahidi kuhamasisha watu wetu walime matunda hayo. Kwa kweli Mabalozi wanajitahidi sana na tutaendelea kuwatetea mpaka wapate nyumba nzuri, ofisi nzuri na nyumba nzuri za watumishi ili wafanye kazi zao kwa utulivu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nilipokuwa natangaza, naona nilisoma kwamba yule Miss Milisenti Obaso ni *Country Director USAID*, sasa sijui walipata wapi, mimi nasoma kama nilivyoletewa, kumbe wanasema ni Mkurugenzi Mkazi wa *Policy Health Initiative* na sio *USAID Director*.

Halafu nilisoma pia Kanoni Guidion Byamugisha kwamba ametoka Uganda, nimepewa maelezo zaidi kwamba yeze huyu ni kiongozi wa dini wa kwanza Afrika kutangaza kuishi na VVU. Kwa hiyo, alikuwa ni kiongozi wa dini wa kwanza aliyejitangaza kwamba yeze ameathirika.

Halafu kuna wageni sikuwatangaza wa Mheshimiwa Madeje, wao ni ndugu Joseph Mwaka, Naibu Kamanda wa UVVC Dodoma Mjini na Dkt. Peter Kapoka, Mhadhiri Mwandamizi *UDOM*, Chuo Kikuu cha Dodoma, ndugu David Mwaka, mfanyabiashara na ndugu Michael Clement mfanyabiashara. Wengine hawa nafikiri niliwatangaza jana walikuwa hawapo.

Tunaendelea na Mheshimiwa Lazaro Nyalundu halafu Mheshimiwa Riziki Omar ajiandae.

MHE. LAZARO S. NYALANDU: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii, kumpongeza kwa dhati, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, Bernard Membe, kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, nachukua nafasi hii, kuunga kabisa mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, kuhusiana na suala nyeti, ambalo limegusa watu wengi ndani ya Bunge hili na nje, suala la *OIC* kwamba kwa sasa lisiendelee kujadiliwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Waziri, nimpongeze pia, kuna viongozi hapa, yuko Mheshimiwa Waziri Mkuu...

NAIBU SPIKA: Nani unayemwambia, mimi ni Naibu Spika maana wewe unasema Naibu Waziri.

MHE. LAZARO S. NYALANDU: Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri naeleweka, Waziri Mkuu Pinda, viongozi wa dini mbalimbali za Kiislamu na za Kikristo, wameendelea

kutoa matamshi ambayo yanaendelea kuliweka hili suala sawa kwa sababu ni suala nyeti kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kunukuu kipengele kimoja muhimu sana cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika utangulizi, *page* ya 13 Nanukuu:-

“Kwa hiyo, basi, Katiba hii imetungwa na Bunge Maalum la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa niaba ya wananchi, kwa madhumuni ya kujenga jamii kama hiyo, na pia kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Tanzania inaongozwa na Serikali yenyewe kufuata misingi ya demokrasia, ujamaa na isiyokuwa na dini”. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndiyo ile iliyotajwa katika misingi ya utangulizi wa Katiba yetu. Serikali, kimsingi, kwa tafsiri hiyo, hairuhusiwi kabisa kuwa na dini lakini pia hairuhusiwi kusaidia uanzishwaji wa chombo chochote au mamlaka yoyote yenyewe misingi ya dini yoyote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hali kadhalika, Serikali chini ya kifungu hicho, itatakiwa kusimamia uhuru wa kuabudu na uhuru wa mtu kujiunga ama kujihusisha na dini au dhehebu lolote kwa kadri atakavyoona inafaa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, haitakuwa jambo la busara na itakuwa kukiuka, kwa mawazo yangu, misingi ya Katiba ya nchi hii, kuruhusu aina yoyote ya michakato inayohusu masuala ya dini moja dhidi ya dini zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lilipoibuka suala la *OIC* Zanzibar yaani Zanzibar kujiunga na *Organization of Islamic Countries*, Mwalimu Nyerere alisema hapana. Suala linalofanana na hili ni suala la uanzishwaji wa Mahakama za Kadhi au Mahakama za aina yoyote ambazo zinahusisha dini moja dhidi ya dini zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaweka sawa mfumo wa sheria na mfumo wa sheria huu unatakiwa kuwa mfumo wa sheria moja ambayo haitakuwa na *parallel legal systems* kwamba kuna sheria za Wahindu, kuna sheria za Wakristo, kuna sheria za Waislam, kuna sheria za Marasta Farian, kuna sheria za Wabudha na kadhalika. Nchi hii ina madhehebu yote niliyoyataja, nchi hii ina dina zote zile nilizozitaja na zile ambazo sijazitaja, wapo watu wengi Tanzania ambao wanawali katika zile dini zinazoitwa za asilia, Katiba inawapa uhuru kujiwekea miiko yao ndani ya dini zao wenyewe kadri watakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoa mfano, Uingereza inajitambulisha kwamba ni nchi ya Kianglikana, sio tu Kikristo, sehemu zingine wanasema wao ni nchi za Kikatoliki, Sweden inajitambulisha kwamba ni nchi ya Kilutheri wala sio nchi ya Kianglikana, wala sio nchi ya dhehebu lingine lolote la Kikristo. Saudi Arabia, ni nchi ya Kiislam, Israel ni nchi ya Kiyahudi, Tanzania haina dini “*a secular state*”. Nchi nyingine niliyotaka niitolee mfano ni *United State of America*, Marekani, haina dini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi ya Uingereza, ukioa mke wa pili, ni kosa la jinai na utafungwa kwa sababu wao wenzetu wameandamana na dini fulani iliyosema ufanye mambo fulani. Katika Saudi Arabia, muda mrefu sana wanawake walikuwa hawawezi kuendesha gari kwa sababu ya mila na desturi zao na dini zao. (Makofi)

WABUNGE FULANI: Ndiyoo!

MHE. LAZARO S. NYALANDU: Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema hapa ni kwamba, kwa sababu baadhi ya nchi zimeamua kuwa nchi za dini fulani, zimeendelea kumomonyoa uhuru wa watu na wananchi katika nchi zao. Baba wa Taifa alisema:-

“Nchi hii itakuwa ni nchi isiyo na dini yoyote isipokuwa watu wake, Watanzania, wadogo kwa wakubwa, walio Songea na walio Mtwara, wao wataruhusiwa kuwa na dini wanazozichagua wao kwa wakati wao wenyewe”. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi kujiunga na nchi za Kiislamu au na nchi za Kikristo, itakuwa ni kuvunja moja kwa moja Katiba na misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hoja kwamba tuwe kama mataifa mengine, tuwe kama Uganda, kwa sababu Uganda ni wajumbe wa *OIC*, tuwe kama Somalia, Chad, Sudan, Nigeria na kadhalika, utaratibu wa mila na desturi... (*Makofi*)

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu!

NAIBU SPIKA: Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Mudhihir!

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64(a), mzungumzaji hapa anasema wanawake wa Saudi Arabia, hawaendeshi gari kwa sababu ya mila zao na dini yao. Dini ya Kiislamu haimkatazi mwanamke kuendesha gari. Tunaomba afute kauli hiyo ili asitutie jazba Waislamu kwa kutusingizia mambo ambayo hatuna. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Nikiitisha *Hansard* na kusoma hakutaja dini, amesema dini zao. Nitaitisha *Hansard* sasa hivi maana sasa hivi niko *careful* sana na *Hansard*, maneno mnayosema, mwingine anahisi, kumbe hajataja. Italetwa *Hansard* sasa hivi, Katibu leta *Hansard* iliyosemwa hapa. Inawezekana alisema hivyo lakini nilivyomsikiliza mimi, ndiyo maana nilinyamaza hapa, kwa sababu alisema dini zao, sasa zifi hizo ndiyo sifahamu. Tutaleta *Hansard*, tunaendelea. (*Makofi*)

MHE. LAZARO S. NYALANDU: Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi ya Zambia, aliingia Rais anaitwa Chiluba, yeze ni Mkristo, jambo la kwanza alilolifanya, akatangaza Zambia itakuwa nchi ya Kikristo, ulikuwa ukiingia Zambia wakati wa Chiluba, unaambiwa jambo la kwanza andika jina lako la ukoo, unaandika Nyalandu. Jambo la pili, unaambiwa andika majina yako ya Kikristo, sasa yule ambaye sio Mkristo, yule ambaye hana dini kama hiyo, inakuwaje? Rais Chiluba yeze mwenyewe akaanza kuwasulubu wenzake, akamsulubu aliyekuwa Rais wa Kwanza, Mzee Kaunda, akamnyanyasa, wakamuua mtoto wake, mambo yakaendelea kuwa mabaya lakini leo tunapozungumza, yeze mwenyewe amefilisiwa na Mahakama Kuu ya nchi yake. Mambo kama haya, hayataitendei mema nchi kama Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nyingine nyingi zimeshindwa, kuna kesi maarufu ya Mama Mariam iliyofanyika Nigeria. Sehemu moja ya Nigeria iliruhusiwa kuwa na sheria za aina fulani, yule mama chini ya zile sheria akahukumiwa kuuawa kwa kupigwa mawe, dunia nzima ilipiga kelele kuokoa maisha ya yule mama. Pakistan katika miezi michache iliyopita, Serikali iliingia dili na Mkoa mmoja wakasema nyie bwana mpo wengi tunawaruhusu mfanye Sharia baada ya muda wakaona kwamba wamekosea wakaingia vitani. Hivi ninapozungumza, jeshi la Pakistan linaendelea kupambana na Wanamgambo wa Kitaleban kwa sababu walikuwa kilomita 100 kutoka Makao Makuu Islamabad, nchi hiyo iliingia

hatari, wale wenzetu walianza kuwakata watu ulimi, kuwakata mikono, kuwapiga mawe na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la dini, ni suala nyeti sana. Naomba nirudie, naomba niiambie Tanzania, suala la dini, ni suala nyeti sana. Nchi hii imekaa na watu wa dini zote siku zote tangu enzi za Mwalimu watu wasio na dini, walio na dini, wamekaa kwa amani kikaitwa kisiwa cha amani, watu wakasema tunapenda kwenda Tanzania tukaone, kwa sababu Tanzania ni mahali ambapo uhuru wa kweli upo. Walisema sentensi hii “*the house divided shall not stand*”. Dini au ukabila utaigawa nchi katika vipande vipande. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba yenyi misingi imara kama ya Tanzania, misingi hiyo inatikiswa unapotaja suala la ukabila, unapotaja suala la udini wa aina yoyote ile. Ukabila unaimaliza Kenya, lakini udini unainyemelea Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninakusudia kuleta Muswada, Hoja Binafsi katika Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kulitaka Bunge hili lenyewe kupiga marufuku Bunge kujadili masuala yanayohusu imani za dini yoyote ndani ya Bunge lako Tukufu na kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iendelee kulinda uhuru wa kila mtu, uhuru wa kila raia kuamini, kufanya chochote anachokitaka ili mradi tu asivunje sheria na kwamba fedha za walipa kodi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kamwe zisitumike ama kuinua ama kukandamiza dini ya aina yoyote ile dhidi ya dini zingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ya Tanzania ni baadhi ya nchi chache sana duniani, utakuta kwenye mtaa mmoja kuna Msikiti ambao unafuatana na Kanisa, baada ya Kanisa kunafuata *temple, temple* inafuatana na ofisi ya Mganga wa Kienyeji, hawa wote wanakaa salama na Waganga wa Kienyeji wana *practise* wanachokiamini, nchi hii imewatanza watu wote, imekaa salama na wako salama. Katika Iraq, waumini wa Shia hawakai mtaa mmoja na waumuni wa Suni ingawa wote wako katika dini moja. Ubaguzi wa aina yoyote utailetea nchi hii shida kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naonya juu ya mambo yafatayo; naonya juu ya wanasiwa kunyemelea kutaka kuidhinisha mambo ya dini yatungiwe Sheria humu ndani, naonya. Naonya juu ya mambo yafuatayo, naonya juu ya wakuu wa dini zote huko waliko kunyemeleanyemelea siasa na kutaka mambo ya kule yaje hapa kwenye siasa. Hali hii ikiruhusiwa, itaiondoa Tanzania tunayoifahamu “*a beautiful land that we call ours*” itaondoka. Tusiruhusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iendee huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema cha mwisho ni hiki, narudia pale pale alipoishia Mheshimiwa Waziri Membe. Tufute kabisa, tupige marufuku kujadili mambo ya *OIC, OIC* ni shirika lao huko, hatuna haja ya kusubiri sisi mpaka mwaka 2010 eti waamue nini kwenye shirika lao, Taifa letu lije lianze mchakato, hakuna mchakato hapa, Tanzania ni nchi isiyo na dini, kamwe haitakuwa na sababu kujadili iwe mwanachama wa nchi za Kiislamu au iwe mwanachama wa nchi za Kikristo au iwe mwanachama wa nchi za Kihindu, au iwe mwanachama wa nchi za Kiyahudi, nchi hii, ni nchi ya watu wote. Wananchi wote wa Tanzania, kitu ambacho wanaki-trust, wanakipenda, wanakisifu, ni mambo mawili muhimu, hatujui sisi rafiki yako ni wa kabilia gani na wala wa dini gani, tumekaa salama miaka nenda rudi, hili jambo la kuleta kujadiliana dini fulani humu ndani limetoka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwasihii kwa upendo Wabunge wenzangu, tuachane na jambo hili. Ninaomba tuyachie Makanisa, sisi wote pia ni waamini wa huko,

tuiachie Misikiti sisi wote tukienda huko ni waumini, wajadiliane mambo yao, wayapange, waendelee kutetea amani na mustakabali wa Taifa hili, miaka 100 ijayo wajukuu na vitukuu watayakumbuka mambo ambayo Bunge hili liliamua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kabisa, naomba nirudie kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na naomba haya ambayo nimeyasema yaingie katika udongo ulio mzuri, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Nashukuru, ahsante sana. Mheshimiwa Riziki Omar Juma halafu tutakuwa na mchagaji wetu wa mwisho, Ndugu Shibuda. Naona uhame hiyo *microphone* haisikiki vizuri.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia machache katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambayo ameiwasilisha muda mfupi iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uwezo na afya iliyonjema na kuweza kusimama hapa leo mbele ya Bunge lako hili, ili nami niweze kuchangia machache kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba niende moja kwa moja kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 14, kipengele namba 34 ambacho kinazungumzia kuhusu Mradi wa kusaidia Uchaguzi Mkuu Tanzania mwaka 2010. Malengo ya mradi hapa yaliyotajwa ni matano lakini naomba niseme kwamba Watanzania mara nyingi tumekuwa tukiandaa hotuba zetu nzuri, zinatuvutia sisi wenyewe na zinawavutia wananchi ambao wanatusikiliza au ambao wanazisoma lakini la kusikitisha ni kwamba mara nyingi tunakuwa sijui tunateleza kwa bahati mbaya au sijui inakuakuje lakini hatutembei katika maneno yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa *UNDP*, wametusaidia pesa kwa ajili ya kuimarisha uwezo wa kitaasisi, kiutawala na kiutendaji wa Tume ya Uchaguzi ya *ZEC* na *NEC* ili kuziwesha kupanga shughuli za kuandaa, kuendesha na kusimamia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 na malengo mengine ambayo nitayataja baadaye. Uchaguzi ambao umetajwa hapa na fedha ambazo tumepewa kwanza, ni kujandikisha kwa wapiga kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa masikitiko makubwa, naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri kwa ruhusa yako lakini kabla sijaendelea kuzungumza, niombe Mheshimiwa Waziri aende kwenye *site* kule Pemba, akaangalie hali halisi ya Uchaguzi unavyoendelea yaani daftari linavyoboreshwa halafu Mheshimiwa Waziri atajionea mwenyewe hizi fedha ambazo tumepewa jinsi zinavyotumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ni msimamizi mkuu wa matumizi na lengo la matumizi yanapotolewa lazima lifikiwe na kwa sababu hiyo tutapopanga mipango yetu na kuitumia fedha yetu kwa ajili ya malengo ambayo tunayatarajia, nadhani tutakuwa tumelinda heshima ya nchi yetu na tumefanya kazi vizuri na yale malengo tutayafikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zimetolewa kwa ajili ya uchaguzi, kutoa taaluma kwa wapiga kura, kusimamia vizuri uchaguzi, kutoa maelekezo mazuri, lakini hapa wiki iliyopita, tulikuwa tukijadili kwa kina sana, Wabunge wengi walichangia kuhusu namna ya daftari linavyoendelea kule Zanzibar, hizi fedha ni kwa ajili ya *NEC* na *ZEC*, je, *ZEC* ndivyo walivyoelekezwa kuzitumia fedha hizi vibaya? Naomba Waziri ye ye pamoja na

mwakilishi wa *UNDP* ambao wametoa hizi fedha, waende kwenye *site*, wakaangalie hali halisi ya mambo yanavyokwenda na namna fedha hizi zinavyotumiwa vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sisi tunakwenda kwenye uchaguzi, tunawataka wapiga kura, lakini wapiga kura tunawawekea vikwazo vikubwa sana ambavyo haviwezi kuwapa ile haki yao ya kupiga kura, unaponiambia mimi niende nikajiandikishe niwe mpiga kura, vijana ambao wamefikia umri wa kupiga kura wananyimwa na fedha hii inawahuju na wao wana haki ya kutumia fedha hii, je, atakayekuja kupiga kura na kumchagua kiongozi ambaye anamtaka ni nani ikiwa vijana ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa, ndiyo tunaowaachia mirathi yetu, hawaandikishwi? Watapiga kura vipi tukiwa tumewanyima haki yao ya kujiandikisha? Wale ni vijana ambao kwa sasa nathubutu kusema kwamba pengine *either* hawana vyama au kama wanavyo lakini maamuzi yao bado hatujayajua, kwa nini wanyimwe haki hii wakati maamuzi yao hatujayajua? Kila Jimbo, ukiwa unapunguza vijana wapatao 2000, vijana wale huwezi kujuu ni wa Chama gani, kuna vijana wengi wanaolalamika sasa hivi hata wa Chama Tawala, wamenyimwa hii haki kabisa, wako na wanapiga simu hapa hapa kwa viongozi wao kwamba jamani mbona tunanyimwa hii haki?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Karume juzi alipokuwa akizungumza na wahitimu wa Chuo cha Utalii, alisema kwamba kila ambaye ana haki ya kupata kitambulisho aende katika ofisi ya Mkurugenzi akapewe kitambulisho ili aweze kwenda kujiandikisha kuwa mpiga kura sasa je na haya maneno ya Rais Karume pia tunayapinga? Tunaachana nayo kule kwetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia hili si kwa bahati mbaya, nazungumzia hili kwa sababu katika kitabu chako umezungumzia masuala ya uchaguzi na fedha jinsi zinavyotolewa na namna zinavyotumika. Ni masikitiko yangu makubwa kwamba fedha hizi, nasema kwa uhakika, fedha hizi zinatumwiwa vibaya kwa sababu wale walengwa hatuwafikii. Je, hii taaluma ya kupiga kura atapewa nani ikiwa mimi ambaye unanitarajia nije nipige kura, unaninyima hiyo haki ya kupiga kura? Hii taaluma tutampa nani? Je, ikiwa mimi au wewe unanyimwa hii haki ya kuwa mpiga kura, je, utawala bora uko wapi hapa katika nchi yetu? Mheshimiwa Obama juzi alizungumza maneno nafikiri viongozi wote wameyasikia kwamba Waafrika ni lazima twende katika masuala ya utawala bora na utawala bora ni pamoja na kuheshimu demokrasia, demokrasia tunaipinda je, utawala bora utapatikana?

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa utawala bora haupo, ikiwa demokrasia haipo na demokrasia kwanza ni kumpa mtu haki ya kuchagua na kuchaguliwa na apewe uhuru wa kumchagua kiongozi anayemtaka, ikiwa mimi unanibana nisiweze kuchagua kwa imani tu kwamba labda mimi namtaka kiongozi wa upinzani, *are you sure* kwamba mimi nampigia kura kiongozi wa upinzani? Yule kijana unayemnyima, una hakika, pengine unakinyima fursa Chama Tawala kupata kura zake ambazo kwa uhakika, watazipata kwa fikira tu au mawazo potofu, kwa hiyo, hapa Watanzania tunaonekana hatuendi katika msingi ule wa utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema tutasaidia utoaji wa elimu kwa wapiga kura na kuhakikisha kwamba wapiga kura hasa wanawake, vijana, walemavu na makundi mengine yaliyotengwa na jamii yanapata haki zao za kupiga kura, tayari tumeshawanyima hiyo haki. Kwa maana hiyo, hiyo taaluma hatuwapi na hawapati na hata wakipata hiyo taaluma watakuwa hawana pa kuitumia kwa sababu haki ya kupiga kura hawana, kwa hivyo, fedha hizi zinapotea bure. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuvisaidia Vyama vya Siasa nchini na Asasi zisizo za Kiserikali kuchangia katika uwandikishaji wa wapiga kura, usimamizi madhubuti na utatuzi wa migogoro baada ya uchaguzi. Kwa nini kuwe na utatuzi wa migogoro baada ya uchaguzi kama uchaguzi utakuwa wa haki na huru? Kama demokrasia itaheshimiwa, hakutakuwa na migogoro, lakini migogoro inatokea kutokana na kwamba hatuheshimu haki za wapiga kura, hatuheshimu mawazo yao, hatuheshimu chaguo lao na hapa fedha zinaendelea kuteketea. Kwa hivyo, tunapofanya haya, migogoro itakuja na migogoro itakuwa haiishi milele Tanzania kwa sababu hatuheshimu haki za wananchi wetu, hatuheshimu mawazo yao, hatuheshimu chaguo lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoa mafunzo ya kuratibu shughuli za wasimamizi wa Kimataifa wa uchaguzi hususani kwa kuhakikisha kwamba hawapati matatizo yoyote katika kutekeleza majukumu yao ya usimamizi. Haya pia wakati mwingine yanakiukwa, sitaki niende *deep* zaidi lakini ukitaka, nitakufuata na nitakueleza mambo mengine ambayo najua haya pia hatuyaheshimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha uwezo wa vyombo vya habari vya Kitaifa na Kimaifa kwa kutoa habari za uchaguzi kwa wazi na kwa uwiano chanya. Sisi tunapokaribia uchaguzi katika Tanzania, mambo yanayooneeshwa kwenye vyombo vyetu vya habari, ni ya kutisha, zile nchi ambazo wamepigana, wamevurugana wakati wa uchaguzi na kuuwana na mambo mengine ndiyo tunayooneeshwa kwenye *television*, kwa hiyo, tunawatisha wapiga kura. Watu wengi wa vijijini wanaogopa vita, wanaogopa Askari, hivyo, watu wetu tunawatisha, hawawezi kukabiliana na uchaguzi kwa sababu ya kuwatisha, kwa nini tusiwaoneshe chaguzi zilizo haki na huru? Kwa nini tuwaoneshe chaguzi za ajabu ajabu au migogoro ya ajabu ajabu isiyokwisha? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nazungumzia hili kwa uchungu sana kwamba ebu Watanzania tujifunze kuheshimu demokrasia, ebu twendeni katika uchaguzi ulio haki na huru, siku zote tunahubiri umoja, amani na utulivu mbona tunauvuruga wenyewe? Iweje tuuvuruge wenyewe halafu tuseme oooh, yule anafanya hivi, twendeni katika uchaguzi, tuwapangeni watu waende wakajiandikishe katika daftari bila ya Askari Polisi, bila KM, bila ya Mgambo, bila ya Zimamoto, bila ya nani, tutakaposimama kwenye foleni kwa utulivu watu wataenda watajiandikisha na kila mwenye haki yake atapata, atapiga kura kwa usalama na amani. Hebu tujifunzeni Watanzania jamani, kwa nini tunang'ang'ania utaratibu huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Daftari la Wapiga Kura, mimi nazungumzia kifungu hiki tu, mimi nakwenda na mzee pale anataka kuijandikisha kupiga kura au anataka kupewa hiyo Zanzibar *ID* wanaita, anaambiya lete cheti cha kuzaliwa. Mheshimiwa, Mzee aliyeko kijijini, wa miaka 70 au 80, hebu niambieni kweli ana cheti cha kuzaliwa huyo au tunamnyima haki yake kwa makusudi? Hili ni tatizo, tuzitumie fedha ambazo tunapewa vizuri kama tulivoagizwa. Tumeomba pesa kwa ajili ya kutusaidia, kwa ajili ya masuala ya chaguzi, tusiziende kinyume na makubaliano, tufuate hotuba zetu, twende na vitendo katika maneno yetu, tusiandae maneno kinyume chake tukaenda na vitendo vingine, kinyume na maandiko yetu. Tuyaheshimu maandiko yetu Mheshimiwa Naibu Spika, walahi tutajenga demokrasia ya kweli na Watanzania tutaishi kwa amani, tutaishi kwa umoja na tutaishi kwa utulivu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naomba niseme kwamba, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa ruhusa yako, Wizara itoe vigezo ilivyoweka katika utekelezaji wa *Economic Diplomacy* na pia aniambie ni Balozi zipi zilizofanya vizuri na zipi zimefanya vibaya. Naomba tupate tathmini Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa mchango wako mzuri. Sasa nitamwita Mheshimiwa Magalle Shibuda, atafuatiwa na Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu. (*Makofi*)

MHE. MAGALLE J. SHIBUDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa hii ili nami niweze kuchangia.

Awali ya yote, nachukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watumishi na Watendaji wa wote wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje. Hii ni kwa juhudhi mbalimbali wanazotekeleza kwa maslahi ya nchi zetu.

Vile vile napenda kutumia fursa hii, kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kikwete, kwa juhudhi zake mbalimbali ambazo zimevezesha kunawilisha mahusiano ya Tanzania na ulimwengu mzima, nampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wahenga husema kwamba, ‘usione chaelea kimeundwa’. Amani ya Tanzania imeundwa na kufumwa na waasisi wetu Hayati Mheshimiwa Karume na Hayati Baba wa Taifa. Ninaomba sana tusiichezee. Wajibu wetu raia na viongozi wote, ni kuendeleza na kudumisha amani na mshikamano wa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa madhumuni ya kumbukumbu sahihi, napenda kusema kwamba, madhumuni ya matakwa ya Katiba ya nchi hii ambayo Wabunge sisi sote tumeapa kuilinda na kuitetea ni kuhakikisha kwamba Bunge hili haliwi chombo cha habari cha kufarakanisha jamii. Tunapozungumzia vyombo vya habari vinatuandika vibaya, vinatengua udhu na heshima mbele ya jamii, basi naomba na sisi Wabunge wote ambao kila asubuhi huwa tunakumbushwa na sala, hii ni kwa ajili ya kuhakikisha kama ulikuwa umetenguka fikira zako urejee kwa Mwenyezi Mungu kwamba uko kwa maslahi ya Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi ya amani na ujenzi wa mshikamano, utategemea maneno yanayotoka katika vinywa vyetu, je, ni ya kujenga amani na mshikamano au ya kufarakanisha au ya kuleta tafrani? Kwa hiyo, naomba sana tunapoumba maneno, tujihakiki kuhakikisha kwamba tuna dira sahihi kwa maslahi ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 28 ya Katiba, inasema kwamba matakwa ya kila raia ana wajibu wa kulinda na kuhifadhi na kudumisha uhuru, mamlaka, ardhi na umoja wa Taifa. Ibara ya 9, inahimiza Serikali itawezesha ujenzi wa Jamhuri ya Muungano kwa kufuata Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea na kwamba matumizi ya utajiri wa Taifa, yanatilia mkazo maendeleo ya wananchi na hasa zaidi yanaelekezwa katika jitihada za kuondosha umaskini, ujinga na maradhi. Sasa je, Wizara yetu ya Ushirikiano wa Kimataifa ina wajibu gani wa kuhakikisha kwamba wawekezaji na mikataba iliyopo Tanzania inaendeleza dhamira ya kujengwa Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea kama ilivyo katika matakwa ya Katiba yetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro mingi sana ipo katika makampuni yaliyokuja kuwekeza Tanzania na migogoro hiyo inasimamiwa hapa nchini, aidha, mwekezaji akiwa na malalamiko anakwenda kwenye Ubalozi wake, hivyo, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, inakuwa inaguswa moja kwa moja. Sasa Tanzania tuna mikataba ya mikosi, je, juhudhi zipo katika Wizara hii za kutengua mikataba hiyo kwa ushirikiano na Balozi na nchi mbalimbali ili kuhakikisha kwamba mikataba hiyo inasafishwa na hivyo rasilimali za Tanzania sasa tuweze kufaidika nazo kama matakwa ya Katiba yanavyosema?

Mheshimiwa Naibu Spika, ulimwengu tulionao huu, unaozungumziwa sasa, ni utandawazi. Je, utandawazi unaumba maono gani ya kusadikisha kwamba ushirikiano wa Tanzania na Kimataifa bado uko katika mwegemeo wa Katiba yetu yaani matakwa ya Katiba ya kujega Ujamaa na Kujitegemea? Au sasa tuumbe maneno mapya tuondoe maneno hayo katika Katiba ya nchi yetu!

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Marekani, baada ya kutetereka uchumi wa nchi yake, alikuwa na ujasiri wa kuhakikisha kwamba pesa za Serikali, pesa za umma wa Wamarekani, zinakwenda kujenga uchumi wa makampuni hayo ya kibepari ili yaendelee kushika hatamu za ubepari na kuongoza uchumi Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tulikuwa na bahati ya kushika hatamu za uchumi. Tilitaifisha mashamba mbalimbali, tukajenga viwanda vyote sasa hivi tumebinafsisha, je, bado mwegemeo wetu ni wa itikadi ya Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ama sasa tunaumba siasa na itikadi ambayo haijabainika kwa Watanzania? Naomba Mheshimiwa Waziri utusaidie kutufahamisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuko katika diplomasia ya uchumi, je, watumishi wa Wizara ya Mambo ya Nje, wanasadikishwa na kuthaminishwa na mafunzo gani waelewewe ujamaa na kujitegemea ili wanapokuwa nje wawe washenga wa kusadikisha imani ya ujamaa na kujitegemea wakati kwenye vyuo vyote tulishafuta? Je, huduma hiyo wanaipata wapi ili uzalendo wao uendelee kuwa na mwegemeo wa kutimiza matakwa yale ya Katiba?

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ilisema kwamba tumefaulu kushika hatamu zote za uchumi ziwe mikononi mwa Watanzania. Je, Wizara hii inawasadikisha nini Watanzania na inaonyesha ujasiri na ushupavu na ushujaa upi ambao uko chini ya nahodha, rafiki yangu, swahiba wangu, Mheshimiwa Bernard Membe, Mbunge, je, huko Umoja wa Mataifa mmewahi kwenda kusema kwamba pana nchi ambazo zinatunyonya? Idara ya Sheria ya Wizara yetu baada ya Mheshimiwa Rais kuunda Tume ya Jaji Mark Bomani kuhusu matatizo ya mikataba, mmeweza kwenda kulalamika Umoja wa Mataifa ili Tanzania iombe Umoja wa Taifa utusaidie? Kama Mahakama za Kimataifa zinakamata Marais wa Afrika kwamba walikuwa na tabia mbovu katika utawala pamoja na demokrasia, je, mikataba ya *Multinational* na au makampuni haya ya kibepari ambayo yanatunyonya na yanayotumia utandawazi kuwa mirija ya kibepari ya kuwanyonya Watanzania, ninyi mnasimamia vipi au mmelalamika wapi au mna juhudzi zipi ili rasilimali za Tanzania zisiendelee kunyonywa kwa mwegemeo wa kwamba tunajenga itifaki ya mahusiano? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tunategemea vipi tuondokane na kazi ya kuombaomba mikopo na misaada ikiwa mashirikiano yetu hivi sasa ni kujenga itifaki ya uhodari wa kwenda kuomba misaada lakini hatuna uhodari wa kutetea mikataba yetu? Ikiwa wale ambao wameihujumu nchi hii kwa mikataba mbovu, je, kwa nini nao wasipelekwe kwenye Mahakama ya Kimataifa, nao hao wakaadhibiwa ikiwa sisi tunaogopa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Katiba yetu, Ibara ya 9, inasema utajiri wa nchi utilie maendeleo ya nchi na kwamba uchumi usiwe katika mamlaka ya watu wachache, je, utandawazi huu unahimiza nini hivi sasa kwa Watanzania? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais aliunda Tume ya Mark Bomani, tukapata faida kubwa sana. Bado naendelea kusema, ushahidi ulioumbwa na Kamati ya Jaji Mark Bomani, nahimiza Wizara hii uutumie. Je, utandawazi unahimiza itikadi gani hasa hapa duniani hivi

sasa ili Tanzania tujiumbe upya katika mwegemeo wa siasa? Je, nchi ya China ambayo inahimiza ujamaa na kujitegemea, baada ya utandawazi imeacha ujamaa na kujitegemea au ina mwegemeo wa kuendeleza siasa hiyo? Je tunajifunza nini Watanzania kutokana na hali hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuwaasa Waheshimiwa Wabunge, tutumie maelezo ya kujenga hisia za jamii za misisimko ambapo tunakonga miyo yao, siyo tunajenga tafrani ndani ya miyo ya Watanzania. Naomba sana hilo tuliendeleze. Tusitumie lugha za kuumba mifarakano ya tafrani. Vilevile, naomba Bunge lisiwe malighafi ya hisia na visa dhidi ya jambo ambalo mtu hana utafiti na nguvu za hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili tusiwe na miteguko ya kutengua amani na umoja wa mshikamano. Wabunge tusiwe wana harakati wa madhebu, kwani Bunge si Msikiti wala Kanisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitobo kidogo huzamisha jahazi kwa maji yanayoingia. Kwa hiyo, napenda kutahadhirisha kwamba, ndo ndo za tafrani zitazamisha amani na umoja wa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lisiwe misumari ya majeneza ya kuzika amani na mshikamano wa Watanzania. Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, anapendwa na madhehebu yote na hakuna Kiongozi atakayetawala nchi hii kwa mwegemeo wa dhehebu moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo napenda kutangaza kwamba bila Rais Mwinyi, Mwislamu, nisingekuwa leo na dhamana za uongozi kwa sababu ndio ye ye aliendumba, ndiye alinitia unyago wa kisiasa. Wazee wa Zanzibar, wamekuwa kila siku nguzo yangu na asilimia kubwa ni Waislamu. Matendo yako, kama yanakubalika katika Msahafu na Biblia, wewe ni mja wa Mwenyezi Mungu na daima utapendwa na watu wote si maneno ya kubwatuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuachane na kauli za kuviza kwa hisia za amani za Watanzania. Bunge lina usanifu wa kusadikisha ama kubomoa umoja na mshikamano. Bunge hili ni chombo cha habari kinachoaminika sana na Watanzania. Sasa tusije na misisimko ya ujana. Najua ujana ni harakati, najua uzee ni maono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, rafiki wa majuto ni ujinga, naomba tujitahadhari, tusije tukawa na majuto. Viwango vya ujinga sio kwamba kama mtu akiwa na dhamana ya uongozi vinaondoka kwa sababu mtu haachani na vinasaba vya hulka na silka yake bali dhamana za uongozi, ni vipodozi vinavyopumbaza janaba la mtu mzima hovyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukumbusha tena, ujana ni harakati, uzee ni maono. Aidha, kila aliye na subra yuko na Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu atunusuru na mitihani, ahsanteni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nakutakia kila la kheri Mheshimiwa Membe. (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Sasa nitamwita Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu lakini ngoja kwanza, hapa mbele yetu, kuna wachezaji wa zamani wa Timu ya Taifa, wakiongozwa na

Kapteni wa zamani wa Timu hiyo, anaitwa Jella Mtagwa, yuko wapi Jella Mtagwa? Aah ndiyo huyo. Naomba ile Timu ya zamani wote wasimame. Karibuni sana, karibuni sana wamekuja kucheza na timu yetu ya Bunge leo jioni Uwanja wa Jamhuri. Basi mnakaribishwa kuwashangilia na kushangiliana wenyewe huko. (*Makofi*)

Haya nitamwita Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, nataka tupumzike kidogo kutokana na maneno mazito aliyotoa Mheshimiwa Shibuda. (*Kicheko*)

MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo na kama unavyosema, baada ya Mheshimiwa Shibuda unakuwa na machache sana ya kuzungumza. Lakini kabla ya kuendelea kuzungumza zaidi naomba kuunga hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuja mara ya kwanza kuwa Mbunge wa Jimbo la Bukene, nimekuwa Mjumbe wa Kamati ya *Foreign*, kwa hiyo, najuajua vitu vichache katika Wizara hii na ninajua kwamba kuna matatizo hayo ya nyumba na vitu vingine. Kwa hiyo na mimi ninapenda kuomba Wizara iwafikirie Mabalozi wetu katika Balozi mbalimbali waweze kuwa na hadhi inayostahili ya Kibalozi, wawapelekee mishahara yao mapema ili na wenyewe waweze kukaribisha watu maana wao ni kioo cha Tanzania wakiwa katika nchi hizo za mbali. Kwa hiyo, naomba wawe wanawapelekea na kuwasaidia kuwapa vitu yaani nyumba, makazi mazuri na mambo mengine kwa hadhi ya Ubalozi ili wakiweza kuita pale Tanzania, wajulikane kwamba hapo ni Tanzania kweli na mtu anajisikia kwamba ni Mtazania kwa sababu wanatutangazia nchi yetu vile vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kusisitiza kidogo tu kuhusu suala la Katiba. Katiba yetu, tulio hapa, tuitetee, tukianza kuivunja sisi wenyewe kama Viongozi, mimi nashindwa kuelewa wale tunaowaongoza itakuwaje. Kwa hiyo, nataka kusisitiza kama Katiba inavyosema, nchi hii haina dini. Nchi hii ni ya watu wote, wenyewe dini mbalimbali na makabila wengi. Tuna dini sisi wananchi, lakini nchi yetu haina dini. Ndiyo nataka kusisitiza hapo hapo kwa sababu tukianza kuzungumzia, tunataka kuingiza masuala mengine hapa ndani tunaungana na Serikali, tunaungana na Vyama vingine vyta kidini, maana yake tunaondoka kwenye Katiba yetu inavyosema kwamba nchi hii haina dini. Kama tunaondoka pale, tutaleta mifarakano isiyo ya lazima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tumeishi kwa amani kwa miaka yote mpaka wenzangu wameshasema tangu enzi za Mwalimu, tumeishi kwa amani, tumeishi Waislamu hapa Wakristo hapa, Wapagani pale na wa dini za Hindu na kadhalika. Mimi nakumbuka nilipokuwa mdogo nilikuwa nakaa karibu ya Wahindi wana dini yao, ile wanachoma moto wakifa, halafu vile vile nilikuwa nakaaa na Waislamu lakini tulikuwa tukichukua kuku kupeleka kwenda kuchinja kwa Mwislamu ili tuweze kula pale nyumbani lakini sisi wenyewe tukiwa Wakristo ile tulifanya kwa upendo kwamba tunataka tuwe na umoja wote hata kama sisi wenyewe tungeweza kuchinja pale lakini tulikuwa tunapeleka kwa mtu ambaye anaaminika na jamii yote ili atuchinjie yule kuku hata akipiga hodi mtu mwininge, kama unavyojua, mila na desturi za Mnyamwezi na Msukuma, akikukuta unakula kwanza hatakiwi kuzungumza na wewe anakula kwanza, anakaribia karibu, mnakula naye. Mkishamaliza kula ndiyo anakueleza shida iliyomleta na sababu ya mila na desturi hiyo ni kwa sababu pengine anaweza kuwa amekuja na shida ya msiba, kwa imani yake, kwa hiyo, akikuambia pale pale unaweza ukashindwa kula. Kwa hiyo, anaona kwanza ule naye halafu baada ya kula ndiyo akuambie. Sasa kama akishakuambia umesha kula kwa hiyo unagalagala unavyotaka, anguka lia unavyotaka, lakini umeshashiba. Kwa hiyo, tunafanya hivyo, ndiyo maana nasema tulikuwa tunapeleka kuku au mbuzi kwenye sikukuu, kwenye

nyumba ya jirani, ili wachinje kwa sababu anaweza kuingia mtu yeote nyumbani pale mfano Mwislamu, sasa akikuta umechinja kuku au ng'ombe, unakula pale, usipomwambia haina tatizo kwa sababu hajui lakini kwa sababu ya ujirani, kwa sababu ya upendo tulikuwa tunafanya hivyo ili na yeze ale kitu kilicho halali. Kutokana na hayo ndiyo maana nasema tumeishi vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuja tukatunga Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 na wengine wameoana dini mbalimbali, tumeoana makabila mbalimbali. Kulikuwa na makabila yaliyokuwa yanajulikana kuwa ni makali sana na mengine mapole sana katika mchanganyiko huo tumepata, hakuna mkali sana sasa hivi. Wote tuko mchanganyiko mzuri wa Mtanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukianza kuingiza vitu vingine nya kuweka hapa mambo ya dini, hata ikiwa ya Kikristo au hata ya Kiislamu, tutawagawa hawa wananchi tunaowaongoza, tutakuwa *source* au waanzilishi wa kuvunja amani hii tuliyonayo. Naomba kabisa ndugu zangu sisi kama viongozi hata ikisogezwa hii Sheria ipelekwe mwaka gani na mwaka gani, naomba tuache kufikiria vitu kama hivyo. Tufikirie amani hii kuwarithishe wajukuu zetu, vitukuu vyetu ili sura ile iendelee kuonekana ya Tanzania iliyo nchi ya amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanasema cha Kaizari mpe Kaizari cha Mungu mpe Mungu. Sasa hapa Kaizari ni Serikali. Sisi wote tunatakiwa kulipa kodi. Sisi wote tunatakiwa kufuata mambo yote ya dunia kama Serikali inavyotuvekea na Sheria tunazozitunga hapa, kwa ajili ya mwili wetu lakini ya Mungu ni kwa ajili ya Ufalme unaofuata yaani ya roho, kila mtu anatakiwa kuamini anachoamini. Kila mtu anatakiwa kufuata wa huko anakoamini na kila mtu anatakiwa kutoa mchango au fedha au kitu chochote, nguvu zake zote kwenye kile anachoamini huko. Kila pahali pana utaratibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema hivi, kama mimi, mimi ni Mkatoliki, kule kwangu kuna utaratibu wa tofauti. Kuna utaratibu wa Baraza la Walei, mimi nitafuata utaratibu wa Baraza la Walei kutoka chini, nitafuata, kama wanataka mchango, nitafanya hapo. Kuna utaratibu wa wanawake wa Wakatoliki wa WAWATA, nitakwenda nitafuata, watasema wanataka hela au wanataka kitu gani, nitashiriki na mambo yao katika utaratibu wao kama Katiba inavyosema, mradi hatuvunji Sheria. Kuna utaratibu wa kila kitu. Kuna utaratibu wa kusoma Seminari watoto wanaotaka kuwa Mapadre na kuendelea namna hiyo. Kule kwenye Seminari wale hawataki kuo, hawataki kuolewa. Kwa hiyo, wale wanakwenda kwenye Seminari wanasoma wanakuja kutufundisha dini na sisi tunawaamini na tunawaheshimu Mapadre. Sasa mimi nikiwa kwenye dini namheshimu Padre pamoja na Ubunge wangu lakini namheshimu Padre, Paroko na namheshimu kwa sababu ya utaratibu wa roho kwa sababu yeze anaangalia roho yangu. Naamini na Waislamu ni vile vile wana vikundi nya kwao nya wanawake, wana vikundi nya kwao katika Baraza la Walei sijui wanaita kitu gani, sifahamu. Sasa michango ya kule iwe huko huko na sisi huku huku na Angalikani nao hivyo hivyo na wale wa kwangu nyumbani kwangu kule kwenye Jimbo langu Waswezi kwa mfano, wengine hawana dini, huko huko tunakutana, tunakubaliana, tutaaamkia katika staili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi mimi nimekwenda kutoa Kombe langu la *Teddy Kasella-Bantu Cup* walikuwepo Waswezi. Tumefuatana na wenyeve nikawaamkia kwa staili inayotakiwa na nimecheza ile ngoma yao lakini *of course* na wenyeve katika staili yao lakini ni wapiga kura wangu, nimefanya vyote ambavyo walikuwa wananiomba. Sasa hiyo ni huko, kama mnawapa msaada wanaoutaka, ni kule kila mtu peke yake tusije tukaingiza kila mtu akaanza kuomba Mswezi anatakiwa tumpe hela na yeze aweze kuendesha biashara

dini yake kwa watu wake. Haya Mkristo sijui wa madhehebu gani naye vile vile, Mkatoliki, Mwangalikani, Mlutheri, Mpentekoste, kadhalika na kadhalika maana yake Wakristo wako wengi, kila mtu aombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba cha Kaizari tumpe Kaizari ambayo ni Serikali, ya kwetu yale ya roho kila mtu na roho yake na njia yake na utaratibu wake, tusiingize kwa Kaizari mambo ya roho kwa sababu kila kitu kina utaratibu wake. Ukishindwa kutunza kitu cha roho yako, unatengeneza tofali za nyumba ya baadaye huko, yawe ya kwako mwenyewe unayehusika, muumini wewe na viongozi wako wa dini yako lakini tusije tukaingiza huku, kuchukua kodi ya wananchi wa Tanzania maskini ambao hawana hata mlo mmoja wakati mwininge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba tusivunje Katiba. Katiba yetu inasema wazi kabisa, nchi hii haina dini ila sisi wenyewe tuna dini. Sisi tulio na dini tuna majukumu yetu kila mtu katika staili yake na anavyopenda yeye mwenyewe. Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Msemaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, hajaongea muda mrefu sana alikuwa anaumwa, karibu!

MHE. HAJI JUMA SEREWEJI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, kwanza niunge mkono hoja asilimia mia kwa mia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, niishukuru Ofisi ya Bunge, kwa kuniwezesha mimi kwenda kwenye matibabu huko *Delhi India Appolo Hospital* na niishukuru Wizara ya Afya pamoja na Madaktari wote walioota kibali ili niende huko. Vile vile niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mwanakwerekwe, kwa kunipa uongozi huu kwa sababu bila wao nisingefika huko. Kwa hivyo, nawashukuru sana na naahidi sitawaangusha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Mheshimiwa Kidawa hapa kwa vile alivyosema kwamba Mabalozî wetu walio nje lazima wawe na hadhi ya Kibalozi. Kwa sababu hivi sasa ukienda nchi yoyote tu ukitaja wewe unatoka Tanzania, basi wananchi wa kule huwa wanafurahia sana na wanafurahia kutokana na sifa za Tanzania, sifa ya mwanzo demokrasia, utawala bora, amani na utulivu. Sasa kama Mabalozî wetu watakuwa hawana sifa za Kibalozi kama nchi yetu inavyosifiwa itakuwa si vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nashukuru Ubalozi wa kule wanavyopokea wagonjwa ambao wanatoka huku, wanatushughulikia vizuri. Namshukuru ndugu yetu Makongoro ambaye saa 24 anapita na anatuangalia na anasikiliza matatizo yetu, pamoja na Maofisa wote wa kule pamoja na Balozi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitia kwako, ninaomba tu kama inawezekana pale *Delhi Airport* basi iwepo Ofisi hasa na itambulikane kwamba Ofisi ile ni ya Tanzania ambayo inapokea wageni kuliko ndugu yetu Makongoro pale au mhusika ye yeyote anayekwenda pale akawa anaanza kuhangaikahangaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitazungumza kidogo kuhusu vitambulisho vya Zanzibar. Mimi naunga mkono sana vitambulisho vya Zanzibar, vya ukaazi wa Zanzibar na naviunga mkono kwa sababu mbili, sababu ya mwanzo kabisa hakuna Chama chochote ambacho kitaingiza kijana aliyejewa chini ya miaka 18 kwenye uchaguzi. Kabla ya vitambulisho vile ilikuwa Vyama vya Upinzani vinalalamika kwamba CCM wanaingiza

vijana wa miaka 14 na Chama Tawala CCM vile vile wanalamika kwamba Vyama vya Upinzani wanaingiza vijana wa miaka 14 lakini hivi sasa vitambulisho vya Uzanzibar huwezi kukipata mpaka utimize miaka 18 na ukikipata kitambulisho kile cha miaka 18 wewe umeshakuwa na haki ya kupiga kura. Ndiyo maana Rais wa Zanzibar akawa anasema wananchi wote wapatiwe vitambulisho vile ili wakapige kura. Sasa ndio maana Vyama vya Upinzani vinaanza kulalamika havipatikani. Ni kweli havipatikani kama hujatimiza miaka 18, ukitimiza miaka 18 hakuna matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, hata wale ambao wamezaliwa Zanzibar, lakini wameandikisha uraia nchi ya nje, wakija Zanzibar hawatapiga kura zamani kulivyokuwa hakuna ukazi wa Uzanzibar, mtu aliye na uraia wa nchi ya nje akija pale anapiga kura. Sasa nafasi hiyo haipo kabisa na ndio maana Wapinzani wanalamika kwa sababu watu wao wengi wako nje. Tunaunga mkono vitambulisho vya Uzanzibar. (*Makofi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile natoa wito kwa Tanzania Bara pamoja na wananchi wa Jamhuri ya Muungano, mtuletee vitambulisho vyetu vya uraia wa Jamhuri ya Muungano kwa sababu hata sasa uchaguzi wa Jamhuri ya Muungano Tanzania Bara, itakuwa unavamiwa sana na waliokuwa sio raia wa Tanzania, lakini tukiwa na vitambulisho vya Uraia wa Utanzania, hataingia mtu wa Kenya, wa Uganda na ye yote yule na hapo vile vile Wapinzani watalalamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalosema mimi, Mpinzani kama Mpinzani, akikisifu Chama Tawala, kakuumiza; lakini ikiwa analia, ujue unakwenda sawa. Hivi sasa Zanzibar, Chama cha Mapinduzi, hatutathubutu kumuingiza kijana wa miaka 14, Chama cha CUF, CHADEMA, havitathubutu kumuingiza kijana wa miaka 14, kwa sababu ni lazima uende na kitambulisho cha Uzanzibari ambacho ni lazima ufile miaka 18. Sasa wenzetu wamezoea kuwavisha mabaibui watoto wa miaka saba, 14 na matiti ya vifuu pale, wakaandikishe kura; hayo yameshafutwa Zanzibar hayapo. Sisi tunaunga mkono na ndio maana Rais wa Zanzibar, akawa hana wasiwasi akasema kila mmoja aliyetimia miaka 18 aandikishwe. Juzi juzi tu wameambiwa kwamba waende kwa Mkurugenzi, waende pamoja na karatasi ya kuzaliwa ya miaka 18, huru watapata, sasa mnalamika nini? Ngoma droo. (*Makofi/Kicheko*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyosema, ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika kikao hiki, kwa hivyo, ninaunga mkono hoja 100/100, mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Mwanakwerekwe, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, huyu ni msemaji wetu wa mwisho. Wakati Mheshimiwa Nyalandu, anachangia hoja hii, alisema yafuatayo, nasoma *Hansard*.

“Mheshimiwa Naibu Spika, katika Nchi ya Uingereza, ukioa mke wa pili ni kosa la jinai na utafungwa, kwa sababu wao wenzetu wameandama na dini fulani ili yosema ufanye mambo fulani. Katika Saudi Arabia, muda mrefu sana wanawake walikuwa hawawezi kuendesha gari kwa sababu ya mila na desturi zao na dini zao.”

Mheshimiwa Mudhihir, akasimama kuhusu utaratibu akasema:-

“Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu. Kanuni ya 64 (a), mzungumzaji hapa anasema wanawake wa Saudi Arabia, hawaendeshi gari kwa sababu ya mila zao na dini yao. Dini ya Kiislamu haimkatazi mwanamke kuendesha gari. Tunaomba afute kauli hiyo ili asitutie jazba Waislamu kwa kutusizingizia mambo ambayo hatuna.”

Sasa nasoma maneno yangu niliyosema:-

“Nikiitisha Hansard na kusoma hakutaja dini, amesema dini zao. Nitaitisha Hansard sasa hivi. Sasa hivi niko careful sana na Hansard maneno yanayosemwa. Mwingine anahisi kumbe hajataja; italetwa Hansard sasa hivi. Katibu, leta Hansard iliyosemwa hapa. Inawezekana alisema hivyo, lakini nilivyomsikiliza mimi, ndiyo maana nilinyamaza hapa, kwa sababu alisema dini zao; sasa zipi hizo ndiyo sifahamu. Tutaleta Hansard, tuendelee.”

Maneno:-

“Katika Saudi Arabia, muda mrefu sana wanawake walikuwa hawawezi kuendesha gari kwa sababu ya mila na desturi za dini zao.”

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, niko sahihi. Mheshimiwa Mudhihir, nilivyosikia na *Hansard* inavyosema ni hivi. Kwa hiyo, haikuwepo kwamba ni hisia ya dini fulani, tunaendelea. (*Makofi*)

Sasa namwita Naibu Waziri Wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Waheshimiwa Wabunge, siku hizi *Hansard* inatoka dakika ile ile na tunataka kuhusu utaratibu, maneno, tutakuwa tunasoma *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Waziri au atasema Waziri tu peke yake? Mheshimiwa Naibu Waziri, kujibu hoja, tayari tumefikia wakati. Vipi! Hamko tayari?

Leo ni Jumamosi, hakuna namna, ndio maana inabidi, kama hamwezi kusikiliza kwa makini, ndio basi tena, ndio hivyo tena. Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri. Ndio maana inabidi, dhamana ni yako, wakikusaidia ni bahati yako. Sasa Wataalamu kama mna majibu, wakati Naibu Waziri anajibu, hayo muandalieni Waziri yaje sasa hivi. Siku hizi hatuahirishi kikao, tunaenda tu. Dhamana ni ya Waziri. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uzima na afya njema na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kutoa mchango wangu kwenye hoja iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Aidha, ninapenda kuwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Kitope, kwa ushirikiano na msaada wanaonipa katika juhudzi zangu za kuwatumikia kwa nia ya kuwaletaa maendeleo. Nawaahidi kuwa nitaendelea kwa nguvu zangu zote, kuwatumikia kwa mujibu wa Ilani yetu ya Mwaka 2005/2010. Naomba wazidi kuniunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kumshukuru kwa dhafi Waziri wangu, Mheshimiwa Bernard Kamilius Membe, kwa ushirikiano na msaada mkubwa anaonipa katika kuniongoza vema ili niweze kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi. Namwomba aendelee kunipa ushirikiano na msaada huo, kwani ushirikiano, msaada na uongozi wake ni muhimu sana kwangu.

Pia ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliota michango yao kwenye hoja hii. Michango yao tunaithamini sana kwani nina hakika lengo lake ni kuimarisha ufanisi na utendaji wetu wa kazi katika Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa muda niliopewa, kama ifuatavyo; hoja zilikuwa nyingi, kwa hivyo kwa muda mchache niliopewa, nitajibu zile ambazo nitaweza kuzijibu kwa sasa na Mheshimiwa Waziri, atakuja kuendelea nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Castor Ligallama, ameshauri kwamba tuwe na Ofisi za Balozi katika nchi za Mashariki ya Mbali, kama vile Indonesia, Vietnam, Thailand, ili kupata zana za kilimo, *power tillers* na kadhalika, ambapo nchi hizi huwa zinatoa vifaa hivi ambavyo ni rahisi na pia ni rahisi kutumia. Nimshukuru sana Mheshimiwa Ligallama, kwa mchango wake huu. Wizara inatambua umuhimu wa kuwa na uwakilishi katika nchi hizo. Kwa sasa, kwa vile hali ya fedha hairuhusu kuwa na Balozi kamili, Wizara yangu inafanya kila linalowezekana ili kuwa na Mabalozi wa Heshima, katika nchi hizo. Tunajaribu sana kuteua Mabalozi hawa wa Heshima kwa mujibu wa vigezo tulivyonavyo na Wizara yangu imeanza kuweka Kamati maalum ambayo itakuwa chini ya uongozi wa Naibu Waziri, kwa ajili ya kushughulikia mambo haya ya Mabalozi wa Heshima, katika nchi ambazo hatuwezi kupeleka Balozi kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Sevelina Mwijage, anasema je, Wizara ina habari ya kero wanazopata Watanzania wanapoomba Visa? Tunazo habari kwamba Watanzania wanapata taabu sana wakati wanapokwenda kuomba Visa, kwa mfano katika Ubalozi wa Uingereza au Ubalozi wa Marekani na Balozi nyingine. Mimi mara kwa mara huwa ninajaribu sana kuingilia kati ili kero hizo ziweze kupungua lakini tunavyojua kila nchi ina taratibu zake na mara nyingi utoaji wa Visa ni ridhaa pia ya nchi husika, kwa hivyo, sio busara sana kwa nchi yangu kuingilia. Lakini tutajitahidi kwa kadiri tunavyowenza kuwatetea Watanzania waweze kuondokana na usumbufu huo, waweze kupata Visa kwa urahisi na kwa haraka kadiri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, anasema baadhi ya Balozi kuingilia kati au kutoa kauli kwa mambo yetu ya ndani, hasa kwenye uchaguzi mdogo wa Tarime, je, hali hii ndio kawaida ya uzushi wa utumishi wa Mabalozi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Mabalozi waliopo nchini hapa, hawapaswi kuingilia mambo ya ndani ya nchi yetu na hasa pale chaguzi zinapofanyika. Mabalozi ni wawakilishi wa nchi zao na kazi yao kubwa ni kuimariswa uhusiano kati ya nchi zao na Tanzania, wakiashaanza kuingilia mambo ambayo hayawahuusu ndani ya nchi yetu, ina maana wanavunja ule utamaduni wa kazi zao walizoletewa hapa kufanya. Kwa hivyo, Mabalozi wanapokwenda Mikoani, wanapaswa kwanza kuiarifu Wizara, kujua kwamba wanakwenda Mikoani kufanya kazi moja, mbili, tatu. Nia kubwa kwanza ni kujua wanakwenda kufanya nini na pili ni kwa usalama wao wenyewe kwa sababu tunapopata taarifa ni lazima tuwaarifu viongozi wa Mkoa anaokwenda ili waweze kuwalinda wasipate madhara yoyote, kule anakokwenda. Kwa hiyo, kwa ufupi ni kwamba Mabalozi hawatakiwi na hawaruhusiwi kwa mujibu wa Sheria za Diplomasia, kuingilia mambo ya ndani ya nchi ambazo wanafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, amesema kwamba, wafanyakazi wa Wizara wengi wanatoka upande wa Tanzania Bara, ukilinganisha na wachache wanaofanya kazi na Balozi kutoka upande wa pili wa Muungano. Ninapenda niseme tu kwamba Wizara yangu inachukua kila juhudhi kuhakikisha kwamba kuna uwiano kati ya wafanyakazi ndani ya Wizara, kutoka Zanzibar na kutoka Tanzania Bara. Vile vile kuna uwiano wa wafanyakazi kutoka Tanzania na kutoka Tanzania Visiwani/Tanzania

Zanzibar kule katika Balozi zetu. Kwa hivyo, juhudhi tunazichukua kuhakikisha kwamba uwiano huo unafanyika. Tutajitahidi sana wakati tunapopata nafasi ya kuajiri kiasi kinachofaa kiweze kuajiriwa kutoka upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Omari Kwaangw', anasema Serikali ichukue tahadhari ya kufuatilia nyendo za wafadhili ili mradi wa kusaidia uchaguzi mkuu wa 2010 utumike kudumisha utengamano. Namshukuru tena Mheshimiwa Kwaangw', kwa ushauri wake. Kama tulivyosema katika hotuba, tutawaomba na kuwatahadharisha Wafadhili wa mradi wa uchaguzi wazingatie Sheria na Kanuni za uwazi na tutaendelea kuwakumbusha na kila inapolazimu kutoa taarifa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Omari Kwaangw' amesema Serikali itekeleze mpango wa *Rescue Package*, ya shilingi trilioni 1.7 kwa ulinzi na taarifa ya utekelezaji iletwe Bungeni mara mbili kwa mwaka. Tunamshukuru Mheshimiwa Kwaangw' kwa ushauri wake na kwa niaba ya Wizara zinazohusika na utekelezaji wa *Rescue Package*, ninaahidi kwamba Serikali itakuwa wazi kabisa katika hili na italeta taarifa ya utekelezaji Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, anazungumzia juu ya nyumba za Balozi wa Zambia au *Tanzania House*. Nyumba hii ni moja ya vitega uchumi, lakini iko katika hali mbaya. Serikali bado haijachukua hatua zozote za kuikarabati. Serikali ina mpango maalum wa ujenzi, ununuzi na ukarabati wa nyumba zake katika nchi za nje. Kila inapowezekana na fedha zinaporuhusu, tutajitahidi sana kukarabati nyumba zetu na tunajua kabisa nyumba zetu ziko katika hali mbaya na dhaifu, tutajitahidi kurekebisha hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, ametuambia Balozi zetu nje ziwe na watumishi wenyе taaluma za biashara na utalii. Hilo tunalifahamu na sasa kila tunapopelea watumishi wetu nje, tunapelea mtumishi katika Balozi fulani na taaluma inayohitajika pale. Kwa hivyo, kama anahitajika mtumishi wa taaluma ya mambo ya utalii, tunapelea mwenye taaluma hiyo. Tunahitaji mtumishi mwenye taaluma ya uchumi, tunapelea mtumishi wa aina hiyo. Kwa hivyo, hilo linazingatiwa sana na Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, anasema Balozi zetu zimepata hati zisizoridhisha za ukaguzi na baadhi ya Balozi kutumia zaidi ya bajeti zilizopangwa. Ni kweli, Wizara imechukua hatua za kuwataka wote wenyе hesabu zenye kasoro, kutoa maelezo. Hivi sasa kila Ubalozi unawajibika moja kwa moja kwa CAG. Zamani walikuwa wanajificha kwenye mgongo wa Wizara, sasa wenyewe ndio wanawajibika. Wizara yangu inafuatilia utekelezaji wa matumizi hayo ya fedha, lakini wenyewe wanawajibika na pale ambapo ubalozi haufanyi vizuri katika matumizi ya fedha, watawajibika wao wenyewe. Matumizi ya ziada ya bajeti mara nyingi yanatokana na kupanda kwa sarafu za nchi wenyе wanazotumia. Tatizo hili tunalishughulikia pamoja na wenzetu wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Khalifa, ameuliza tena sababu ya matumizi ya ziada kwenye baadhi ya Balozi, ni kwamba baadhi ya vifungu vya bajeti hutengewa fedha pungufuli kuliko mahitaji, kuongezeka kwa thamani ya sarafu, kama nilivyooleza na kushuka kwa thamani ya sarafu ya Tanzania dhidi ya thamni ya sarafu ya nchi zile ambazo Balozi yetu ipo. Hizi ni baadhi ya sababu anmbazo zinasababisha matumizi kuzidi kuliko bajeti ilivytengewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Godfrey Zambi, anasema anaupongeza uamuzi wa kipeleka Wanajeshi wetu Darfur na anashauri wakienda huko wafuate maadili ya kijeshi. Tunamshukuru kwa ushauri huo na kwa kawaida Jeshi letu ni zuri, linapokwenda mahali popote pale, linafuata maadili ya nchi zilizopo. Kwa hivyo, tunakushukuru sana na hilo tunalitia maanani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada zifanyike katika kuboresha huduma katika Balozi zetu. Tunashukuru sana ushauri huo na jitihada zinafanyika kila tunapokuwa na rasilimali fedha na watu zaidi, tutaendelea kuboresha huduma katika Balozi zetu. Tunataka Balozi zetu zifanye kazi vizuri na ziawakilishe Watanzania vizuri kule waliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Shally Raymond, Ubalozi wa Tanzania New Delhi, kupatiwa gari jipya kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa. Suala hili tayari limeshashughulikiwa na Wizara ya Afya imekwishanuna gari lipo na labda karibu litaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Castor Ligallama, ameshauri tuwe na Ofisi za Balozi katika nchi za Mashariki ya Mbali, mfano Indonesia. Nafikiri hili nimeshalijibu na kama nilivyosema, juhudu tunazichukua kila inapowezekana ili Balozi zetu zifanye kazi vizuri pale ambapo hatuwezi kipeleka Mabalozi kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge ambao wametoa michango yao kwa kuzungumza na maandishi. Nianze na kuwatambua wale waliochangia kwa kuzungumza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimtambue Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Khalifa, Mheshimiwa Kidawa, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Riziki, Mheshimiwa Magalle Shibuda, Mheshimiwa Teddy Kasela-Bantu na Mheshimiwa Haji Juma Sereweji. Namtakia afya njema sana Mheshimiwa Sereweji na ninashukuru amepata matibabu mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatambue pia waliochangia kwa maandishi nao ni Mheshimiwa Aziza Sleyum, Mheshimiwa Dokta James Msekela, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Sevelina Mwijage, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Mheshimiwa Omari Kwaangw', Mheshimiwa Mtutura Abdallah, Mheshimiwa Lucy Fidelis, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Rajab Hamad, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Gaudence Cassian, Mheshimiwa Dokta Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Ritta Mlaki, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Mwadini Abbas, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Hemmed Mohammed, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Hassan Rajab, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Omar Mzee, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Mohammed Abdulaziz, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula na Mheshimiwa, dada yangu, Anne Kilango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende tena kwa namna ya pekee, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa ushauri wao, kwa mawazo yao na kwa michango yao mizuri sana waliyoitoa katika Wizara hii. Wazungumzaji walikuwa nane, lakini waliota kwa njia ya maandishi ni 42. Inaonesha ni jinsi gani Waheshimiwa Wabunge, wanavyokuwa na hamu ya kuchangia kwenye Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kutokana na mambo muhimu na mazito yanayoendeshwa na Wizara. Ni dhahiri sitaweza kujibu maswali yote 42, kwanza wengine wameweka maswali kama manne katika kila ombi, kwa hiyo yako zaidi ya 100 na mtanisamehe na ninadhani mtanionea huruma kwamba sitaweza kujibui maswali yote.

NAIBU SPIKA: Na una dakika 30 tu.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nitayajibu kwa vikundi tu na kwa mpigo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, lipo kundi la Waheshimiwa Wabunge wanaozungumzia suala la hali mbaya ya fedha kwenye Balozi zetu. Naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kusisitiza kwamba ipo haja ya bajeti hasa ya maendeleo kuongezwa ili kuweza kuyakamilisha majengo yetu kwenye Balozi zetu, lakini pia kuweza kuwalipa watumishi wetu vizuri na hivyo kujenga hadhi ya Taifa letu huko duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwamba katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, Serikali ilituanzia na *development budget*, hela ya maendeleo ya shilingi bilioni 10 na sasa tunakaribia shilingi bilioni 20. Ni matumaini yangu mwakani huenda itakuwa shilingi bilioni 40 na kwa kufanya hivyo tutakuwa tunajijengea heshima yetu nje kwa Balozi mpya tunazotaka kufungua, Balozi zilizochakaa na malipo mazuri kwa watumishi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wenzetu waliozungumzia suala la Darfur na kushikwa kwa Jenerali Bashir. Ninapenda niseme tena kwamba Tanzania sio kwamba inakataa au inaunga mkono hujuma za Kimataifa, mauaji ya Kimataifa au maonezi ya Kimataifa au *torture* zozote zile zinazotokea katika Taifa. Tulichosema sisi Tanzania pamoja na Afrika, ni kwamba muda uliopangwa kutekeleza hili, utaleta fujo zaidi Sudan kuliko amani. Muda uliopangwa kumkamata Bashir, utahatarisha zaidi maisha ya vijana wetu wanaokwenda kulinda amani Darfur, kuliko vinginevyo. Kwa hiyo, kwa mtazamo wa busara hizo kwamba Tanzania inapeleka vijana wake na tunetaka Sudan iwe ya amani, hatudhani kwamba kumkamata Jenerali Bashir, ambaye ana Jeshi sasa hivi la kulinda bandari, la kulinda viwanja vya ndege, la kusindikiza mizigo yetu kutoka *Port of Sudan* kwenda Darfur, tulidhani kwamba si kitendo cha busara sasa katika kipindi hiki ambacho tunapeleka vijana wetu Darfur, kumkamata Kiongozi yule ambaye uongozi wake ni wa kijeshi na tukategemea vijana wale na mizigo yao kufika salama Darfur. Kwa hiyo, ni suala la *timing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wengine wamezungumzia suala la mikataba, ndugu yangu John Shibuda, mikataba ya Kiamataifa na Wizara inafanya nini katika hili? Ni jambo zuri kweli kwamba tunapokabiliwa na matatizo ya Kimataifa na hasa katika upande wa Mikataba ya Kimataifa, Serikali inao wajibu wa kufanya kila linalowezekana kutatua matatizo hayo kwa kutumia vyombo vya Kimataifa. Sasa viro vyombo vingi sana vya Kimataifa vinavyoshughulikia migogoro mbalimbali na ni dhahiri kwamba pale tunapopata maombi, kama Wizara au kama Serikali, sisi Wizara ya Mambo ya Nje, jukumu letu ni kupeleka kwenye Wizara ya Sheria na Wizara ya Sheria kuititia kwa Wataalamu wake,

wanalipeleka suala hili katika ngazi za Kimataifa zinazohusika na urekebishaji wa migogoro ya kibashara na migogoro ya Kiusalama. Kwa hiyo, jukumu la Wizara yangu ni kupokea, jukumu la Wizara ya Afya ni kuipoleka na kwa Watanzania, ni kwenda kutolea ushahidi na kuyamaliza mambo haya. Tunathamini mchango huo na tutaendelea kupeana taarifa kila tutakapokuwa tunaomba kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la matangenezo na hili nilitaka kulisemea, la Mheshimiwa Felix Mrema kule Arusha. Tuna nyumba nyingi sana kule, tuna nyumba karibu 360 ambazo zinamiliwi na Wizara ya Mambo ya Nje kuitia *AICC*. Taarifa niliyonayo ni kwamba urekebishaji wa nyumba hizi unafanyika na mpaka sasa hivi nyumba 104, tayari zimeshashughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kwamba, katika Bajeti hii tukishapata pesa kwa sababu ya ufinyu wa fedha tutatenga kiasi fulani cha fedha ili kusaidia kukamilisha ukarabati wa nyumba nyingi pale Arusha. Tukipata pesa nyingine tutakarabati zile nyumba na ikiwezekana kuziweka katika hali nzuri sana ambayo nadhani itamsaidia Mheshimiwa Felix Mrema katika harakati zake za kuwaweka watu wake katika hali nzuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa pia na wenzetu kwamba ni vizuri na huyu ni Mheshimiwa Dkt.Chrisant Mzindakaya kwamba ni vizuri tukawa na uhusiano mzuri wa Kibalozi katika nchi za Asia ambapo tunaweza kufaidika zaidi katika shughuli za maendeleo ya kisiasa, ni kweli kabisa tunafungua ukanda mpya wa mahusiano ya Kimataifa na tunadhani nchi za Asia ni mionganoni mwa nchi ambazo zitaisaidia sana nchi yetu. Wengine wengi wamezungumzia suala la amani katika nchi kuheshimu Katiba na wananchi au Serikali yetu kuwa *a secular state* yaani nchi isiyofungamana na dini yoyote. Ningependa kukazia mambo mawili; kwanza Serikali hii itaendelea kuwa *a secular state*, Serikali itaendelea kuwa *a secular state* wala haitakuwa na dini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ambalo ningependa mtege masikio ya dakika moja tu kunielewa, tatizo moja tulilonalo kwenye *OIC* ni kwamba kwa mujibu wa Katiba iliyotambuliwa na *UN members* au wanachama wa *OIC* lazima ziwe Serikali *inter-governmental organization* hapa ndipo tunapopata matatizo, naomba nirudie tena hapo, sio kwamba Serikali inakusudia eti kuhamza kutoka *secularism* na kujiingiza kwenye dini hapana, tatizo ni kwamba mtu akianzisha *OIC* pekee kama walivyofanya wa Zanzibar mwaka 1963 wala hawakuihusisha Serikali walikataliwa kwa sababu Katiba wanatambua *OIC inter-governmental organization* ni kikundi cha Serikali, Serikali lazima itoe kibali hapo ndipo mnapotukamata mashingo, kwamba ukitaka kuingia kule hapana kwenda peke yako *it is an inter-governmental organization* lakini *that say it baada ya kuyasema hayo haina maana kwamba Serikali hii itahama from secularism* kwenda kukumbatia dini moja hata kidogo tumebanwa tu na visheria vyenyewe na maombezi yangu ni kwamba huko wanakofanyia *review* suala la *inter-governmentalism* hili suala la kuwalazimisha dunia nzima kwamba uingiaji wa kwenye chombo hiki lazima uwe wa Serikali, tunadhani watalifanyia *review* hilo ndugu zangu mnielewe hilo *inter-governmentalism* kwamba yaani wewe kikundi peke yako au wewe mtu peke yako huwezi kujiunga si Zanzibar walijaribu si wakanyamazishwa sasa *this is a contradiction* kwamba tumeamua kuwa *a secular state*, yetu unaambiwa kama watu wanataka kujiunga hii wewe lazima utoe kibali hapo ndipo tulipo na naomba Watanzania mnielewe hilo na ndiyo maana tunasema pia lazima *tolerance* ya kuelimishana, *tolerance* ya kupeana mawazo, *tolerance* ya kutokutumia jazba ili tuelewane twende, *but this country will remain a secular state*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho tumeulizwa maswali mengi sana hapa kuhusu uteuzi wa mabalozi, wanawake washirikishwe katika uteuzi wa mabalozi na mimi nasema tutajitahidi kwa kadiri ya uwezo wetu akinamama wengi mteuliwe katika nafasi za mabalozi. Lakini mwenye ridhaa ya mwisho ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara yangu ni kuweka mapendekezo na ahadi kutoa mapendekezo haya na mtege masikio maana tu ziko nafasi nyingi zaidi ya kumi na sita zinakuja kwa vyovyyote vile akinamama watawekwa katika orodha ya mabalozi ambao tunataka tukateuwe hatutawasahau kwa hilo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ndiyo tunakupigia kengele ya kwanza bado.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naweza kwenda kwa zile nyeti zingine hapa kuna suala la pesa za uchaguzi ambazo ni milioni 23 zilizotolewa na *UNDP* pamoja na *donors* wengine kwa ajili ya uchaguzi Tanzania. Sasa niseme kwamba pesa hizi wabia wa kwanza, watu wa kwanza watakaozipata hizi pesa ni *NEC*, *then National Electro Commission* pamoja na *ZEC*. *ZEC* nadhani wameomba karibu bilioni 6 na karibu bilioni zaidi ya 15 ni *NEC* na nyingine zitakuwa zinasaidia utengenezaji wa makabrasha kama vile maboksi ya kura na vitu vinginevyo. Jukumu letu sisi kama Wizara ni kufanya mambo mawili, la kwanza kuhakikisha kwamba matumizi ya pesa hizi zinakuwa kwa njia ya uwazi, tujue nani kapewa na amepewa kiasi gani.

Lakini la pili kujihakikishia tu kwamba pesa hizi zinatumwi vizuri ili baada ya miaka mitano tuweze kusaidiwa zaidi hilo tutalifanya, ni matumaini yetu na tunaimani na *ZEC*, tunaimani na *NEC* kwamba pesa zitakazotolewa na wafadhili katika hili zitatumwi vizuri, muda ukinuruhusu niko tayari kwenda Pemba, kwenda kujihakikishia lakini wakati wa uchaguzi kwenye *IQ* zile nione kama mambo yanaenda vizuri lakini ni matumaini yetu kwamba vyombo hivi vitafanya kazi yake vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeulizwa maswali nini jukumu la Wizara ya Mambo ya Nje katika Ushirikiano wa Kimataifa kwenye nchi za jirani za maziwa makuu, tunazoshughuli mbili tu; kwanza ni kudumisha ujirani mwema na nchi zote zinazotuzunguka, hili ni jukumu la msingi na jukumu la kihistoria na pili, ni suala zima la kulinda usalama, kutetea ulinzi wetu, kuhakikisha kwamba kwenye nchi hizo tunakuwa na mabalozi wetu, tunakuwa na watu wetu, wanashughulikia usalama wa mipaka na kuhakikisha kwamba wakati wote wahalifu wa upande mmoja hawaingii upande wa pili na kufanya vituko au wahalifu wa upande wetu hawakimbilii nchi zingine kama kichaka chao kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Katiba na Sheria hilo ndiyo jukumu na changamoto kubwa sana ya nchi yetu katika ukanda wa maziwa makuu. (*Makofi*)

Pia kama jukumu letu sisi Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ni kushughulikia migogoro ambayo inawakumbuka kila mara wenzetu wa kwenye maziwa makuu. Sasa hivi tunashughulikia suala la *DRC* na kutatua migogoro ya *DRC* kati ya Serikali na *CNDP* ningependa kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Rais Mstaafo Benjamini Mkapa, ambaye amekubali kuingia kwenye Kamati ya Usuluhishi wa mgogoro wa *DRC* na wamefanya kazi nzuri sana pamoja na Olusiga Obasanjo, ningetaka kutumia nafasi hii kwa namna ya pekee kumpongeza sana kwa ushiriki wake kwenye migogoro hii na sio *DRC* peke yake ameshiriki pale Kenya na kama mnavyoona mwaka jana tulipata matunda ya kufanikisha haya yote yanatokana na sera yetu ya ujirani mwema sera yetu ya mambo nje ambayo nguzo moja ni kutatua migogoro na tuna hazina za kujivunia tuna viongozi wenye uzoefu mzuri watu kama wakina Benjamini Mkapa wanatusaidia kuifanya kazi hii. (*Makofi*)

Kuna suala la deni la Dkt. Rwebugira wa *Kigoma Health Centre* na huyu ni afisa wa Ubalozi wa Zaire, ningependa kulitaarifu Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge wa mkoa Kigoma kwamba Wizara yangu imeandika barua miezi miwili iliyopita ya kuutaka ubalozi mama wa Dar es Salaam umwamishe na umuondoe mtu huyu arudi kwa. Lakini pamoja na barua ile tumeweka na tumesema kwamba deni ambalo lipo kwenye *health* au kituo cha afya cha Kigoma linalipwa lote. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tunataka kufanya mambo mawili na tutafuatia na tutatoa taarifa hapa aondoke na pesa zilipwe na huyu Dkt.Rwebangira, sasa mwezi uliopita na tulipata suala hili tulijaribu kucheki Kigoma pale hayupo sasa hatuna uhakika kama ameshakwenda kwao au amefichama mahali, lakini kama ananisikia barua ameshaletewa na Balozi ameshaandikiwa aende kwao, lakini pesa hizi ubalozi umeahidi kulipa na tutahakikisha wanazilipa. (*Makofi*)

Sasa hadhi ya Chuo cha Diplomasia pia imeletwa na Kambi ya Upinzani pamoja na baadhi ya watu waliochangia na kwamba ombi hapa ni je, tunaweza kukishirikisha yaani ikawa *credited* kwenye Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Sisi kama Wizara tunakusudia kukipa hadhi kubwa sana Chuo cha Diplomasia lakini sio tu Chuo cha Diplomasia kwa kushirikiana na Serikali ya Finland, mwaka huu wa fedha wa 2009/2010 mipango ya kuanzisha chuo maalum kinachoitwa cha uongozi na *strategic development* na maendeleo cha pekee katika Kanda yetu ya Afrika kitaanzishwa na Serikali mbili ya Tanzania na Finland, narudia Chuo cha Uongozi na cha maendeleo peke katika ukanda wetu wa Afrika kitajengwa Dar es Salaam kwa kushirikiana na Serikali ya Finland ikiwa kama ni matokeo ya mchakato uliokuwa unajulikana kama *Helsinki process* baada ya *Helsinki process* kufanya kazi zake zote hizo Serikali hizi mbili sasa imeamua kutengeneza chuo kitakachofanana na Diplomasia lakini hakitakuwa kile cha Diplomasia ili kuweza tu kuwapatia wananchi wengi fursa za kusoma na ni kweli moja ya lengo ya vyuo vyote ni kuvipa utambulizi (*accreditation*) kutambuliwa na Chuo Kikuu ili mwanafunzi atakayekwenda kusoma Chuo cha Diplomasia au kwenye chuo kipyä cha uongozi na maendeleo akimaliza pale, kile cheti atakachokipata kimwezeshe kuendelea na masomo ya Chuo Kikuu popote duniani hili ndiyo linaombwa na hili tutalikusudia kulifanya hili. (*Makofi*)

Lakini pia tumepewa jambo lingine, kwamba kuna baadhi ya Balozi, Balozi ya Uingereza na Marekani ya kutolea *visa* nje ya nchi yetu hasa Nairobi na hivyo kuleta usumbusu kwa wananchi wetu. Kilio hiki tumekipokea na ningependa kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tutaendelea na mazungumzo na wenzetu wa Uingereza na wa Marekani ili badala ya Watanzania kusumbuka na kwenda Nairobi au kupeleka hati zao Nairobi za kupata *visa* za kuingia kwenye nchi hizo shughuli hizi zifanyikie pale pale Dar es Salaam ili kuondoa usumbufu wanaoupata Watanzania katika shughuli zao za kusafiri wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Sasa Mheshimiwa John Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi anasema wananchi wa Comoro kutaka kuijunga na Tanzania sasa si kweli kwamba Jamhuri ya Comoro inataka kuijunga na Tanzania mkitaka tuwashawishi wanaweza lakini bado hawajasema wanapenda. Tulichokifanya Watanzania ni kwamba baada ya ukombozi wa visiwa vile sasa hivi tunawaomba Watanzania watumie kila rasilimali na nashukuru waandishi wa habari walilieleza hili mwanzoni kwamba baada ya kuwakomboa na sasa wako huru visiwa nya Comoro wanaiangalia Tanzania kama ni nchi peke ambayo wanaweza wakafanya kila aina ya biashara, biashara halali, kila aina ya biashara kwa hiyo nawaomba Watanzania tuchangamkie suala hili tulipe uzito jambo hili twendeni tukafungue biashara mabenki ili tupate soko la kuuza biashara zetu, tusiwaache tu tukiwaacha tu ipo nchi itakwenda kufanya

uwekezaji Comoro wakati sisi ndiyo tuliomwaga damu yetu pale na tuliohangai katika mambo ya uokoaji. Naomba Watanzania wote wa mikoa yote hasa Mtwara, Lindi, Dar es Salaam, Tanga kote huko twendeni Comoro tukafanye biashara na sehemu ya kuwekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho suala la ndege ya Yemen ambayo ilipata ajali kwenye visiwa vya Comoro. Tumeulizwa pia kwamba ushiriki wetu wa Tanzania na watu wamefanya nini. Ni kweli kabisa kwamba, ndege ya *Yemenair* ilipopata ajali kwenye visiwa vya Comoro ilikuwa na abiria 153 abiria 152 wakafariki, lakini kwa maajabu ya Mwenyezi Mungu malaika msichana wa miaka 14 peke ndiyo aliyedondoshwa pale kwenye visiwa vya Comoro na baada ya pale kwa kipindi cha siku tisa kuanzia tarehe 30 Juni hadi tarehe 7 Julai hakukupatikana maiti ya aina yoyote wala mabaki ya ndege, jambo ambalo liliwasumbua wananchi wa Comoro na wananchi wa Yemen kutaka kujua ni nini kilichotokea kwa ndege yao ambayo haionekani, hakuna mabaki mengine mbali ya kumkuta msichana yule akiyelekeea kwenye kipande kimoja cha ndege pale kwa hiyo, walikuwa kwenye majuto makubwa sana lakini baada ya siku saba maiti 25 ndiyo zikaibuka kwenye upande wa pwani yetu kwenye kisiwa cha Mafia na Kilwa.

Sasa kitendo kile kilileta faraja lakini Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kaomba Wizara, Ofisi ya Waziri Mkuu iunde *the National Task Force* ikiongozwa na Jeneral Shimbo wa JWTZ na kikosi kile kilifanya kazi nzuri sana ya kuokoa maiti vipande vyote vya ndege vingi sana vya ndege kuvilete kwenye mji wa Dar es Salaam lakini Yemen ikatuma timu yake ya *engineers* na madaktari, Ufaransa ikatuma timu ya *engineers* na madaktari pamoja na ndege za kutafuta maiti, Comoro yenyewe ikatuma *experts* wa DNA madaktari pamoja na timu zake, lakini na wote hawa wakaingizwa kwenye *National Task Force* wakaunda kikosi cha nchi nne ili kuanza kupata maiti, kuzitambua maiti pamoja na vipande vya ile ndege *operation* hii imekamilika kidogo lakini bado inaendelea kama nilivyo sema maiti 25 zimepatikana na asubuhi hii wamesema zimeonekana maiti mbili bahari bado hazijachomolewa lakini zitakwenda kuchukuliwa. Ni wataalam hawa lazima wazitambue kujua kila maiti hata kama umepatikana mguu au mfupa ijulikane mfupa na mguu huu ni wa nani na kwa sababu ya utaalam ulioko duniani sasa *DNA test* tunadhani kwamba baada ya wiki mbili tutaelewa kila kipande kilichopatikana na cha binadamu gani. Ni kwa njia hiyo tu, kwa njia hiyo tu ndiyo Serikali yetu inaweza kuruhusu ndege na maiti hizi kuondoka kwenye nchi inazozihusu ambayo ni Ufaransa na Comoro, zikazikwe. Kwa sababu hatuwezi kuzisafirisha bila ya kuwa na *death certificates* na bila ya kuwa na *identity* kwamba huyu tunayemsafirisha ni nani maana isije ikatokea kwamba ni Mtanzania alikuwa anatoka Kilwa kwenda Mafia akaanguka pale njia halafu tukajumuisha maiti kwenda Comoro. Kwa hiyo, uangalifu huu tunaufanya kwa uangalifu mkubwa sana.

Lakini ningependa tena kuchukua nafasi hii kuwapongeza, kupongeza uongozi wa Wilaya ya Mafia na wananchi wa Mafia kwa kushiriki kikamilifu sana katika kutambua na kutoa taarifa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ili kusaidia kuokoa maiti hizi na pamoja na hayo nasema tena naishukuru Kamati ya Taifa kwa kazi nzuri ambayo wamefanya vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napata hapa sahihisho moja huyu Dkt.Rwebangira ni daktari aliyekuwa anatoa huduma za afya anayedaiwa ni *council general* wa Ubalozi wa Kidemokrasi wa Kongo, na huyu *council general* ndiyo tumemwandikia barua na huyu Dkt.Rwebangira ndiyo huyo daktari aliyekuwa anatoa huduma za afya, kwa hiyo hili tutalishughulikia katika Wizara. Nadhani dakika zimebaki kumi.

NAIBU SPIKA: Mnapigiwa kengele ya kwanza halafu...

WAZIRI WA MAMBO YA NJE YA USHIRIKIANO WA KIAMTAIFA:

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya yote haya na baada ya kukiri kwamba zipo hoja nyingi sana za ushauri ambazo tutazizingatia kama Wizara, ningependa tena nisisitize kwamba michango hii yote hii tunaithamini sana, hamna haja ya kushika shilingi yangu tutaishughulikia kwa ukamilifu sana ili tuweze kwenda mbele na tunashukuru sana kwa michango ambayo inaimarisha na inachoimarishe sana watu wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

Kif. 1001 – *Administration and General* Sh. 5,056,516,300

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru *sub vote 1001, item 210100* nilipokuwa nachangia kwa kusema nilimuomba Mheshimiwa Waziri kuitia kwako kwamba angekwenda kule katika *site* akaangalia *situation* ya daftari namna linavyooendeshwa. Kwa bahati Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, atakwenda wakati wa uchaguzi; uchaguzi ni *process*, kama hujapata walioandikishwa kwenye daftari huwezi ukawapata wapigakura. Sasa ni sawa na kupika chakula usikiangalie kama kimeiva, kimetokea chumvi au vipi, ukaenda wakati wa kula tu, kitakuwa hakina ladha hata kama kimeharibika kitakuwa hakina maana.

Namwomba Mheshimiwa Waziri, angalau wao watoe agizo halisi la wale wanaohusika na lile suala ambao wana haki ya kuandikishwa kwa mujibu wa sheria basi waandikishwe au aende namwomba Waziri sasa hivi aende akakutane na wale ambao wana haki kisheria na wananyimwa hii haki ili hizi fedha ziweze kutumika vizuri. Nakushukuru. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba njibui kama ifuatavyo; kwamba Serikali itaomba nchi nzima kuzingatia sheria za uandikishwaji na sheria za upigwaji kura. Tunaomba kanuni na sheria zote hizo kote nchini inapofika wakati wa uchaguzi zifuatwe; kama hiyo haitoshi nitajitahidi kupata siku moja kabla ya uchaguzi kuandama na dada yangu kwenda kujionea hali hiyo.

MWENYEKITI: Mtaenda nchi nzima?

MHE. FELIX C. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru *subvote 1001 - mshahara wa Waziri*. Sina nia ya kuchukua mshahara wa Waziri, lakini kwanza nimshukuru yeche kwa kutimiza ahadi aliyoitoa mwaka jana ya kuja kukutana na wapangaji wa nyumba za AICC kule Arusha, lakini bahati mbaya baada ya kikao kile, yale yaliyotokea na majibu yake

kufafanua mchango wangu wa maandishi leo hapa, bado hayaniridhishi mimi wala sidhani kama yatawaridhisha wale wapangaji wa nyumba za *AICC* Arusha.

Kwa sababu hoja ya kimsingi ilikuwa ni hoja ya pango, ambalo lilitozwa kiwango kikubwa kuliko inavyoweza kubebeka na dhana ya zile nyumba ilikuwa inaenda kwa hawa wa kima cha chini na kati; na toka mwanzo ilikuwa ni kutoza pango linalooana na mishahara yao. Sasa kuja kuigeuza leo hii na kuifanya ioane na soko, kwanza ni makosa na nafikiri sio dhana ya *Corporate Mission* ya *AICC*, ambayo ni *Conference Tourism*. Hii shughuli ya kukodisha nyumba kwa ajili ya hawa wa kima cha chini na kati hawawezi wakaifanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Waziri hawezি akafanya kama alivyofanya mwenzake Waziri wa Ardhi, kuiagiza *AICC* ihakikishe kwamba vile viwango vya pango vinaoana na dhana nzima ya pango kwa hawa wa kima cha chini na kati, yaani iwe inabebeka kama Waziri wa Ardhi alivyotoa maagizo kwa Bodi ya *National Housing*?

MWENYEKITI: Mheshimiwa swali moja tu.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Mheshimiwa Felix Mrema hilo lingine nitakujibia lakini nilijibu hili moja. Ni kweli kabisa kwamba kiwango cha chini cha upangishaji wa nyumba za *AICC* kwa wale watu wa kima cha chini na katikati zilikuwa zimepandishwa. Taarifa ya awali ambayo ilifanyiwa kazi na Wizara ilikuwa inadai kwamba baadhi ya wapangaji nazungumzia sio wote walikuwa wajanja wa kupangisha zile nyumba kwa watu wengine wa nje, kwa hiyo *inspection* zilipokuwa zinafanywa na wenzetu wa *AICC* wanagundua mpangaji wa pale amempangisha mwenzake na huyu mwenzake ndiyo anamlipa huyu kiasi kikubwa halafu kiasi kidogo ndiyo anailipa *AICC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *AICC* ilipogundua hilo ndipo wakaona kwamba pengine sasa ni vyema tukaenda na bei ya soko. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Felix Mrema, madhali sasa mmelisema tena na kwa kuwa suala hili, naona bado hujaridhika nalo, nitatengeneza timu yangu iende tena Arusha ikafanye utafiti katika nyumba hizi 366 kama itabainika kwamba wapangaji wote ni wa *AICC* tena wa kule Soweto na wanaolipa kiasi chao kama kinavyotakiwa, basi nitatoa mapendekezo ya kufuata mkondo wa ardhi ya malipo yale yafanane na kiwango chao wanachokipokea. (*Makofi*)

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho cha 1001. Katika mchango wangu wa maandishi, nimeeleza kilio cha siku nyingi cha watu wa Lindi na kwa bahati nzuri, wako pale juu; kuhusu kurejeshewa mjusi au *Dinosaur* aliyeoporwa wakati wa Ukoloni wa Ujerumani mwaka 1918. Shirika la *UNESCO*, lilitoa amri kwamba wote waliopora mali hizi warudishe baada ya Ukoloni lakini mpaka hii leo huyu mjusi hajarudishwa Lindi. Wizara yetu ya Mambo ya Nje, ilipewa jukumu hili ili ifanye kila njia ya kuwasiliana na *UNESCO* na wengine wanaohusika ili mjusi wa Lindi arudishwe. Sasa hivi anawanufaisha sana Wajerumani, pale Berlin wanapata dola milioni tano kwa mwezi, kwa ajili ya watalii wanaokuja kumwangalia. Dudu lenyewe ni kubwa, sawa na jumba letu hili. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Aah! Eeeh!

MHE. RAYNALD A. MROPE: Ndiyo ametoka pale Tendeguru; sasa tunataka kujuua na kuiuliza Serikali jamani mmeifikia wapi? Watu wa Lindi wanamtaka huyo *Dinosaur*

wao na hata sisi Watanzania wote tunamlilia tuje tumwone na shughuli za utalii zitaongezeka sana kama atarudi yule *Dinosaur*.

MWENYEKITI: Sasa inakuwa kuna Waziri wa Maliasili na Utalii, unaweza kutusaidia kama liko sawa sawa na jumba hili; kwa kweli unatakiwa kuthibitisha. (*Kicheko*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje....

MWENYEKITI: Ni Serikali.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Kwa niaba ya Serikali, naomba nijibu kama ifuatavyo: Ni kweli kwamba, kwa sasa hivi mawasiliano tumeyafanya na tuko katika maandalizi mbalimbali, lakini mjusi huyo ni mkubwa sana, maandalizi ya kuweza kumleta ni makubwa mno na yana gharama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, urefu wa huyo mjusi ni sawa sawa na kujenga kama ghorofa tatu ndiyo anaweza akasimama na hiyo inatakiwa maandalizi, tukimleta hivi hivi kienyeji tutashindwa mahali pa kumuweka. Pia ni kazi kubwa sana, kwa sababu inatakiwa tumvunje vunje ile mifupa upya, ndiyo tupakie kwenye maboksi halafu aundwe tena upya, ni kazi na inahitaji utaalamu na inahitaji pesa na muda pia. Tunaendelea na mawasiliano, kuangalia tutapatajje faida au tumrudishe kulekule tuwe tunalipwa sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa majibu mazuri lakini naomba nitoe nyongeza. Nilikwenda Ujerumani mwezi wa nane mwaka jana na kweli nimeshuhudia urefu wa mjusi yule ni mita 22 upana na mita 14 kwenda juu. Kwa hiyo, anatisha na ni kweli aliposafirishwa mjusi yule kutoka Lindi mwaka 1918/1919 kama anavyosema Waziri, alikuwa amevunjwa vunjwa lakini kule baadaye akaunganishwa. (*Makofi*)

Sasa mchakato wa kwanza ni huo kwamba, namna ya kulibeba jitulile na kulipeleka Lindi iko kazi; kuna maandalizi ya *UNESCO* yanayohitajika. Mchakato uliopo sasa ambao tutauwasilisha katika Wizara ya Maliasili na Utalii ni wa nchi ya Ethiopia, Addis Ababa, ambayo ilishiriki kurejesha minara yao inayoitwa Oblisk, ilivyoirejesha kutoka Italy ni mkubwa kweli kweli, ile Kamati ya Kimataifa ya Addis Ababa tumekwishiandikia barua ya kueleza mchakato mzima, kwa sababu mchakato huo kama alivyosema Waziri, unahitaji pia tupatiwe pesa kutoka Shirika la *UNESCO*. Sasa mchakato ule ni lazima uwe na Kamati ya Kitaifa, ni lazima wananchi waelimishwe na wakubali, lazima waandishi wa habari walitangaze na Bunge Tukufu lipitishe, likishapitisha hilo, haya masuala ya utawala sasa ndiyo yatakapoanza kufanya kazi.

Kwa hiyo, napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunasubiri sasa Kamati ya Addis Ababa iliyokuwa inaongozwa na Waziri wa Utamaduni, atakapofika Tanzania na kukutana na uongozi, mchato huu utakwenda na utawahuishaa Wabunge wanaotoka Lindi na Wabunge wengine. Kamati itaundwa, italetwa hoja kwenye Bungeni na tuone namna ya kumbeba, kama waliweza kumbeba mwaka 1918 kumpeleka Ujerumani wakati teknolojia ilikuwa ya chini, hatuoni sababu gani teknolojia ya sasa hivi ilivyoikuwa *advance washindwe* kumtoa kule kumrudisha Lindi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Unataka kusema mniamrudisha Lindi au mniamrudisha Tanzania? Tunaendelea na Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu, nilikuwa nimeongelea suala zima la ujenzi wa Ubalozi wetu kule Addis Ababa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba, Addis Ababa ni Makao Makuu ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika na hivyo kunafanyika mikutano mingi sana ya Kimataifa. Serikali ya Ethiopia ilitoa viwanja mbalimbali kwa Balozi mbalimbali, lakini ukiangalia ni kwamba, Balozi nyingi zimeshajenga isipokuwa Ubalozi wa Tanzania haujajenga na hivyo kiwanja kile kimebakia kuwa dampo na inavyoolekea, inawezekana mamlaka ya Ethiopia kukichukua kama Serikali ya Tanzania haitajenga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri; ni lini watatoa fedha kwa ajili ya ujenzi? (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Lyimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nikiri kwamba, Addis Ababa tuna Ubalozi pale umejengwa vizuri sana, lakini kama anavyosema Mheshimiwa Susan Lyimo ni kwamba, kweli tunacho kiwanja kikubwa ambacho tulipewa na Serikali ya Ethiopia, kujenga ubalozi wetu mzuri; na ni kweli pia kwamba, wenzetu wengine wameshaanza kujenga pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutohana na ufinyu wa Bajeti na ninashukuru Waheshimiwa Wabunge mmeliona hilo, tulishindwa kujenga kiwanja kile. Tulichokifanya katika kipindi hiki cha mwaka 2008/2009 na 2009/2010 nikipata hela hizi, tumeagiza sasa tujenge fensi kwamba kuzungusha kiwanja kile ili kiwanja kile kisiwe dampo, halafu mwakani mkituungeza kidogo kwa vyovytote vile ujenzi utaanza kama unavyoanza ujenzi wa Nairobi mwezi Septemba mwaka huu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Rosemary Kirigini.

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Na mimi sina haja na mshahara wa Waziri isipokuwa napenda kupata ufanuzi wa suala ambalo linanitia wasiwaso kidogo.

Kwa kuwa Tanzania ni nchi ambayo inaheshimu sana misingi iliyowekwa na Umoja wa Mataifa wa kuhusiana na masuala mazima ya haki za binadamu, na kwa kuwa muda mrefu sasa kumekuwepo na vitendo vinavyoikiuka misingi hii ya haki za binadamu kwa mfano mauaji ya albino na unyanyasaji uliokithiri dhidi ya wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu Waziri aniondolee wasiwaso wangu, je, Umoja wa Mataifa unasemaje kuhusiana na kitendo hiki na nini nafasi ya Tanzania kama nchi kwenye *International System*?

MWENYEKITI: Yaani wanatuonaje sasa? Mheshimiwa Waziri majibu tafadhali.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilijibu swali la Mheshimiwa Rosemary Kirigini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kama mwanachama wa Umoja wa Mataifa unazingatia misingi yote ya haki za binadamu kama ulivyoandikwa kwenye chata ya Umoja wa Mataifa. Mwaka jana mwezi wa tisa Serikali ya Tanzania ilitia saini kwenye Umoja wa Mataifa mkataba wa kukataza maonevu mbalimbali ya watu amba wana ulemavu mbalimbali kama albino, watu wasioona na watu wengine ukiwemo uonevu wa *gender* mbalimbali kama za akinamama. Tuliweka saini mkataba ule tukiiionyesha Jumuiya ya Kimataifa kwamba Tanzania inajali na kwamba Tanzania inafuata misingi ya kuthamini Haki za Binadamu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, jukumu langu kama Wizara ni kuhakikisha kwamba mikataba hii ya Kimataifa inayoitaka Tanzania kuheshimu haki za binadamu tunaitekeleza. Sasa Wizara zinazobaki kazi yake ni kujaribu kufuatilia kuona tunaendelea kwa kiasi gani. Napenda kumhakikishia tu Mheshimiwa Rosemary Kirigini kwamba, *record* yetu katika *Human Rights Charter* kwa kweli ni nzuri, kama tunao upungufu ni kidogo sana na sisi Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje tutaendelea kushikamana na wenzetu kuhakikisha haki za binadamu zinapatikana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Nzanzugwanko!

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, mimi langu dogo tu kwani sikusudii kuchukua mshahara wa Waziri kwanza mshahara wenyeve mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo dogo tu, heshima ya Taifa letu yaani heshima ya Tanzania duniani na Afrika kwa ujumla imekuwa ni kutetea wanyonge, watu wanaokandamizwa duniani kote na huo ndio msingi wa mwanzo kabisa aliouacha Mwalimu Nyerere. Lakini leo hii nchi yetu tunashuhudia maangamizi mengi ya raia na nchi yetu haisemi chochote kwa mfano tuna mauaji yametokea huko Gaza, Zimbabwe, Kenya na kadhalika. Mbali na hizi juhudzi za kimya kimya za kidiplomasia, je, sera yetu ya nje ya msingi aliyoiacha Mwalimu imebadilika?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu ndugu yangu na rafiki yangu Mheshimiwa Daniel Nzanzugwanko, kwa swali lake zuri linalotetea wanyonge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera za Rais au Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere za kutetea wanyonge hazijabadilika na hazitalabika. Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na jitihada zake za kusemea utetezi wa wanyonge pia tunapata nafasi ya kutoa *statements* nzuri na kali kwa wale wote wanaosababisha hali ya wanyonge kuwa duni. Mapema mwaka huu baada ya Israel au Jeshi la Israel kulisakama sana eneo la *West Bank* kule Gaza kwa upande wa Hamas na kufanya vitendo vikali tulitoa tamko la kuilaani Serikali ya Israel, kwa kitendo cha unyanyasaji na mauaji waliyoyafanya *West Bank*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoa pia kauli kwenye Umoja wa Mataifa na kwenye nchi huru za Afrika mwezi uliopita na wiki mbili zilizopita kutetea wanyonge wa Palestina

ambao wanakandamizwa pamoja na Taifa la Israel. Tumetoa pia kauli ya wazi na ningependa kurudia mbele ya Bunge lako Tukufu kuhusu Western Sahara, watu wa Polisario ambao wanakandamizwa na ni wanyonge ambao Mwalimu alikuwa anawatetea, tumeomba wenzetu wa Morocco kuzingatia mazunguzo yanayoendelea sasa hivi chini ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa chini ya kifungu namba 1871 ambacho kimeteua *mediators* au wasuluhishi wa kusuruhisha mgogoro kati ya *Western Sahara* na Serikali ya Morocco. Serikali ya Tanzania kila inapopata nafasi ya kutoa kauli za kutetea wanyonge imekuwa inafanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo. (*Makofi*)

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi pia sina nia ya kuchukua mshahara wa kaka yangu Mheshimiwa Bernard Membe bali nataka kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia nilikuwa nimeuliza kwamba kumekuwa na malalamiko kwa wafanyakazi au maafisa wanaofanya kazi katika Ofisi za Balozi zetu kutohara na kwamba wanakuwa wakilipwa mishahara yao inayolingana na hali halisi ya mishahara ya huku nyumbani pamoja na hayo kunakuwa na *allowances* lakini zinalingana na hali halisi ya huku nyumbani. Lakini ukiangalia nchi wanazoishi uchumi wao unakuwa uko juu sana, kwa mtu unayemlipa hapa dola 500 yeeye atakuwa anapata hela nyingi lakini mfano ukimlipa mtu dola 500 ambaye yuko Uingereza ni sawa na paundi 200 ambazo ni hela ya matumizi ya wiki moja tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri naomba ufanuzi kama kutakuwa na *review* kwa ajili ya wafanyakazi wale ili waweze kuwakilisha vizuri nchi yetu na maisha yao yalete taswira nzuri kwa nchi yetu. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu hoja ya Mheshimiwa Martha Mlata kama ifuatavyo:-

Kwanza namshukuru sana kwa kuonyesha kujali hali nzuri ya maafisa wetu wa naofanya kazi ubalozini. Sasa ni kweli kwamba, maafisa wetu wanaoishi nchi za nje, mbali ya mshahara wao, wana kitu kinachoitwa *foreign service allowance* na tayari Wizara kupitia Mkutano wa Mabalozi wote uliofanyika Zanzibar mwezi Machi, 2008, walipitia utaratibu mpya wa kuona namna ya kuongeza *foreign service allowance* kwa watumishi wake wanaoishi nje ili *foreign service* zile zilingane na maisha ya kule wanakoishi na siyo huku walikotoka. Pia tumeangalia pia mambo kadhaa kama vile nyumba zao, afya, Elimu wanayoitoa kwa watoto wao na kadhalika haya yote yanahitaji pesa kutoka Serikalini ili watu wetu waweze kuishi vizuri kule nje na wafanye kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba katika pesa tulizozionba mwaka huu pamoja na hizo zitakazokuja miaka ijayo suala la kuthamini maisha ya watumishi wetu wanaoishi katika Ubalozi limepata kipaumbele na ni matumaini yangu kwamba hali hii itanza kuwa nzuri mara baada ya bajeti hii kuitishwa. (*Makofi*)

MHE. DKT. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, na mimi sina zaidi ila nataka ufanuzi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu nimeweka hisia na mashaka makubwa kuhusu hali ilivyo Somalia, maharamia hawa ambao wameshafikisha kiwango cha kuteka meli 42 wapo kwa sababu Serikali ya Somalia ni Serikali ambayo haina nguvu. Pili,

vitendo nya hawa vimekwishadhihirika wazi kwamba wanashirikiana na *Al-Qaida* na kwa hiyo ikiwa hawa watu wenye siasa kali wataitawala Somalia huu ndiyo utakuwa mwanzo wa vurugu katika Afrika nzima.

Je, kwa kuwa Serikali yetu inaushawishi mkubwa, haioni kwamba ingeweza kuweka ushawishi mkubwa ili Serikali zinazohusika zisaidie sasa kuliko kungoja Serikali hii ikiondolewa madarakani?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu hoja ya Mheshimiwa Mzindakaya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba Somalia Waingereza wanasema *is a failed state*, yaani ni nchi ambayo imepoteza hadhi yake ya Utaifa na imefanya hivyo kutokana na vita vinavyoendelea nya wenye kwa wenye, inayohatarishwa kuondolewa pia kwa Serikali ya sasa iliyoko madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki mbili zilizopita tukiwa Libya kwenye kikao cha wakuu wa nchi za Afrika pale ajenda ya Somalia ilijitokeza kwa maeleo hayo hayo na kwa misingi hii hii ambayo kaka yangu Mheshimiwa Mzindakaya anaisema. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeungana na nchi huru za Afrika kulaani sana maharamia na hasa wale wanaotoka kwenye *Al Qaida* kujiunga katika vurugu inayoendelea Somalia na hivyo kuhatarisha amani na usalama wa sehemu yote hii ya Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa kwenye mkutano na viongozi wa nchi huru za Afrika ambayo Rais Jakaya Kikwete alihudhuria, kilichojiteza pale ni kwamba zipo nchi jirani zinazoizunguka Somalia na hasa nchi moja inayodaiwa kushiriki kuunga mkono hawa waasi wa Somalia katika kuindoa Serikali ile. Mheshimiwa Rais Kikwete aliendewa na Somalia kuombwa asaidie lakini pia aliombwa na Eritrea asaidie kwa sababu hali ya usalama kule ni tete sana. Mheshimiwa Rais ameniagiza niwate wenzangu kutoka Somalia na Elitre kuja Dar es Salaam na wamethibitisha kuja wiki ya kwanza ya Agosti, 2009 ili kufanya mazungumzo yenye nia ya kujaribu kutatua migogoro hii inayoikabili Somalia. Somalia ina matatizo makubwa sana na Tanzania itajitahidi, tukishapata taarifa ile kuifanyia kazi. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ikilazimika kwamba tuongeze muda nitatumia kifungu cha 104 (1) kuongeza dakika thelathini. Lakini kwa sasa tunaendelea.

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*.....Sh. 617,516,100

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1003 - *Foreign Affairs Office Zanzibar*.....Sh. 277,003,000

MHE. KIDAWA HAMID SALEHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nataka ufanuzi tu katika kifungu kidogo 2203300 - *Fuel, Oils and Lubricants* inakwenda sambamba na kifungu kidogo 221200 - *Communication and Information*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilimtaka Mheshimiwa Waziri atueleze ni sababu zipi hasa zilizofanya Bajeti ya mafuta ikapungua kwa kiasi

kikubwa sana ukilinganisha na Bajeti ya mwaka jana na ilhali kazi zipo nyingi tu za kufanya. Lakini na kwenye *communication* hakuna hata senti moja, kwa hiyo *activity* hii itafanyikaje?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kidawa tumekuachia kile cha kwanza, Mheshimiwa Waziri umekiona?

MHE. KIDAWA HAMID SALEHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kifungu 220300.

MWENYEKITI: Ni *Fuel, Oils and Lubricants*, ilitoka kwenye shilingi milioni 20 ikaenda kwenye shilingi milioni 10.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe kama ifuatavyo:-

Mheshimia Mwenyekiti, kuanzia mwezi Juni, 2008 hadi Mei, 2009 tatizo la mafuta duniani lilijitokeza sana na hivyo kupandisha bei ya mafuta na bei ya chakula, hayo ni maeneo mawili ambayo yaliathirika. Kutokana na hali hii ni dhahiri kwamba hatua za mwanzo tulizokuwa tumezichukua ni kujaribu kutafuta ufumbuzi wa kupunguza supply yaani supply ya mafuta kutokana na ongezeko la bei.

Kwa hiyo, si Zanzibar peke yake ukiangalia kwenye vifungu vingi tumepunguza sana matumizi ya mafuta. Lakini baada ya kuyasema hayo tulizingatia pia kama alivyosema Mheshimiwa Kidawa hakukuwa na gari yaani walikuwa na gari moja tu na tunajitahidi kutafuta magari kwa kituo cha Zanzibar, pale tutakapopata gari jipya la Zanzibar kutumiwa na Mkurugenzi, gari ambalo halitatumia mafuta sana, gari ambalo litakuwa *economic* na tutapata katika kipindi nadhani cha mwaka huu tutajitahidi kwa kadri ya uwezo wetu tukipata ongezeko hili kusaidia kuiwezesha Ofisi yetu ya Zanzibar kumudu maisha yake na sisi *head quarter* pale watakakwama tutawasaidia. (*Makofifi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1004 - <i>Policy and Planning</i>	Sh. 449,346,800
Kif. 1005 - <i>International Cooperation</i>	Sh. 1,288,463,100
Kif. 1006 - <i>Europe and America</i>	Sh. 291,525,400
Kif. 1007 - <i>Asia and Australia</i>	Sh. 295,907,900
Kif. 1008 - <i>Africa</i>	Sh. 2,692,857,700
Kif. 1009 - <i>Regional Cooperation</i>	Sh. 2,692,857,700
Kif. 1010 - <i>Protocol</i>	Sh. 14,204,049,600
Kif. 1011 - <i>Legal Service</i>	Sh. 2,122,414,600
Kif. 1012 - <i>Information, Education and Communication</i>	Sh. 108,449,400
Kif. 1013 - <i>Middle East Division</i>	Sh. 208,208,400
Kif. 1014 - <i>Internal Audit Unity</i>	Sh. 30,064,876,500

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Programu 20 - Diplomacy and Missions

Kif. 2001 - *Embassy of Tanzania – Addis Ababa*.....Sh. 1,037,726,000

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uafanuzi kidogo kuhusu ubalozi wetu wa Addis Ababa. Mimi nilikwenda Addis Ababa...

MWENYEKITI: Kifungu tafadhali!

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 230 Programu 20 *sub vote 2001* kifungu kidogo cha 230400, *repair of vehicles and transportation equipments* chini kabisa *three but one*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri umeona?

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilibahatika kwenda Addis Ababa na Balozi wetu pale akanipokea na gari yake ya Benz iliyokuwa imechakaa na ambayo ina miaka na tukasafiri kwenda kwenye mpaka wa Djibout gari ile ikachemsha tukiwa kwenye mpaka wa Djibout. Sasa nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba hizi fedha naona milioni mbili ni za kwenda ku-*repair* gari ile ile au Ubalozi wetu Addis Ababa mmeshampelekea gari jipya? Lile gari kwa kweli lilinichafulia hata nguo. Naomba maelezo! (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Kwamba zinatosha kununulia gari jipya au ndiyo nini hapo?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nzanzugwanko kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti gari lile hataliona tena na wala halipo, Balozi ana Benzi nzuri ambayo nimeitumia wiki tatu zilizopita hujawahi kuona. Lakini mbali na hayo pia katika kipindi chetu cha Uenyekiti na kwa kuondoa aibu hizi tulinunua pia gari aina ya kombi kwa ajili ya wafanyakazi wetu. Hizi hela milioni 2,400,000 anazoziona hapa ni kwa ajili ya oil na kurekebisha rekebisha gari zuri ambalo tunalo pale.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2002 - *Embassy of Tanzania - Berlin*Sh. 1,391,888,700
Kif. 2003 - *Embassy of Tanzania – Cairo*Sh. 55,998,500

(*Vifungu vilivyonotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2004 - *Embassy of Tanzania Kinshasa*Sh. 706,281,000

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu kidogo 220400 - *Medical Supplies and Services*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika ka-*sub item* hako utaona kwamba hakuna fedha kwa ajili ya masuala ya afya. Sasa naomba kuhoji je, wafanyakazi katika ubalozi wetu kule Kinshasa wanapougua wanatibiwa kwa kasma ipi?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali hilo lililoulizwa na Mheshimiwa Susan Lyimo kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge, mtaona pale kwenye maeneo kadhaa inapofika kwenye masuala kama hayo unaweza ukakuta hata sifuri. Haina maana kwamba watumishi wetu hawatibibi, kinachotokea ni kwamba kwa *convenience* tu ya *accounting*, hivyo vifungu vinajitokeza hata ukiona *zero* kule sasa Makao Makuu tunapoandikiwa barua kinapokuwa na dharura ya watu kuhitaji matibabu basi Makao Makuu ina utaratibu wa kuchukua *vote* fulani na kujaribu kuweka hiyo *emergence* kwa ajili ya kufanya matibabu kwa wenzetu wanaoishi kwenye Balozi zile.

Kwa hiyo, na wengine wanatibiwa halafu baadaye wanatuletea bili Makao Makuu na sisi tunalipa lakini tulishindwa kuweka viwango maalum vyta matibabu kwa sababu mtu hujui uweke kiwango gani kitakachotosheleza lakini Makao Makuu siku zote ina take care hatujawahi kupata lalamiko lolote linalotokana na watu kushindwa kupata matibabu katika ubalozi.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

kif. 2005 - *High Commission of Tanzania - Abuja*Sh. 752,961,800

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu kidogo 221100 - *Travel out of Country*. Wana pesa sifuri, sasa kama Ubalozu huu wa Abuja uko nje ya Tanzania na hakuna fedha za kusafiria kwenda nje, ni utaratibu gani utakatotumika kuweza kupata pesa ya kusafiria kwenda nje wakati hawana fedha hata kidogo?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, kama ifuatavyo:-

Katika kubana matumizi ya kuhakikisha kwamba, Balozi zetu hazitumii hela vibaya basi hela za aina hii za *travel* maana yake hapa *travelling* ni kwamba Ubalozu wetu Nigeria unaweza ukawa na nchi kama tano hivi zinazoizunguka Nigeria ambazo Ubalozu wetu umekuwa *credited*. Baada ya kupata usoefu wa siku nyingi tukaona kwamba kifungu hiki ukipeleka pesa zinakwisha katika kipindi cha mwezi mmoja au miwili kwa sababu watu watasafiri tu na kwa hiyo, *control* yake iko *head quarters*. Nakushukuru sana Mheshimiwa Ponsiano Nyami umeliuliza hili; *control* ya *fund* hii tunaiweka *head quarters*, lakini pale tunapoona baada ya miezi mitatu au baada ya miezi sita Balozi sasa atasafiri kwenda kwenye *areas of accreditation* yaani nchi ambazo ametakiwa kufanya vile basi sisi ndiyo tunampelekea pesa na posho ili asafiri. Lakini tukipeleka tu kwamba hili ndiyo fungu la usafiri tumepata usoefu mgumu huko nyuma kifungu kile kinatumika wakati wote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maana yake ndiyo hiyo lakini pale inapobidi kusafiri tunawasafirisha.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2006 - *High Commission of Tanzania -London*.....Sh.1,437,802,600

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu kidogo 220300 - *Fuel, Oils, Lubricants*. Ukiangalia kifungu kile wamepewa shilingi 323,100/= tu na huu ni ubalozi wetu kule Uingereza, hasa tukizingatia kwamba bei za mafuta

na maisha kwa ujumla ziko juu. Sasa pamoja na kwamba, Waziri amesema ni kubana matumizi, nadhani kwa kweli shilingi 323,100 ni fedha kidogo sana kwa ajili ya mafuta kwa mwaka mzima katika ubalozi wetu kule Uingereza. Naomba ufanuzi.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Susan Lyimo kama ifuatavyo:-

Kwa bahati nzuri zipo baadhi ya balozi zetu ambazo maduhuli au *allowances* zingine zinatokana na mauzo ya *visa* na sisi kama Wizara, tunatoa kibali kwa balozi zetu zile ambazo zinapokea hela za kutosha za viza kumudu tatizo ambalo Mheshimiwa Suzan Lyimo, analisema la kupata mafuta. Kwa hiyo, hili lina *take care* tunapokuwa na nchi kama Uingereza ambako tunapata fedha za *visa* za kutosha basi tatizo hili tunalitolea kibali ili waweze kumudu, na hadi sasa hatujawahi kupata tatizo hili. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2007 - *High Commission of Tanzania - Lusaka*.....Sh.832,190,400

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2008 - *Embassy of Tanzania - Maputo*.....Sh. 897,831,100

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub vote* 2008, kifungu kidogo 221400 *Hospitality Supplies and Services*, naomba ufanuzi. Kumekuwa na ongezeko kubwa sana kutoka shilingi 9,470,000 mpaka shilingi 33,814,400 fedha za *hospitality*, ni jambo gani ambalo limeongezeka kiasi cha kuleta ongezeko kubwa kiasi hiki.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu ndugu yangu Mtutura kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili limetokana na malimbikizo na madeni ya nyuma katika kifungu cha *Hospitality and Services* na kwa hiyo mara baada ya kuona kwamba kuna umuhimu sasa wa kulipa madeni ya nyuma, ndiyo ikawa *compounded* hapa ili tuweze kulipa madeni yote ya muda wa miaka isiyopungua mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2009 - *Embassy of Tanzania - Moscow*.....Sh.1,187,960,600

Kif. 2010 - *High Commission of Tanzania - New Delhi*.....Sh.1,410,970,800

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2011 - *Permanent Mission to the UN - New York*.....Sh. 2,788,216,000

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Subvote* 2011 kifungu 221400 *Hospitality Supplies and Services*. Napenda kufahamu ni

sababu zipi zilizofanya ofisi hii ambayo ni ofisi yetu kule Umoja wa Mataifa, iweze kuondolewa kifungu hiki ikizingatiwa kwamba, miaka miwili mfululizo iliyopita ofisi hii imekuwa ikipatiwa fedha katika kifungu hiki. Sababu zipi zimefanya kifungu hiki kiondolewe na ofisi hii muhimu ipate sifuri?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu hoja ya Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi yetu ya New York ni moja kati ya ofisi chache sana katika Balozi zetu ambazo ziko *busy* na kifungu hiki cha *hospitality* yaani ukaribishaji wageni pamoja na *services* ni kikubwa sana. Kwa hiyo, kilichotokea ni kwamba Makao Makuu kwa busara zake imeamua kwamba ni vizuri kifungu hiki cha *Hospitality Supplies* na *Services* tukikamate sisi *head quarters* ili pale inapobidi na viongozi wanapokwenda kule, tuwe tunawapelekea fedha kwa sababu ukipeleka fedha katika kifungu hiki zikakaa pale, kila siku inaweza kuwa ni *hospitality* na *services*. Kwa hiyo, katika kuminya matumizi haya tunabana kwanza sisi, halafu wakituandikia Katibu Mkuu pamoja na *CPE* ndio wanajaribu kupeleka fedha za kifungu hiki.

MWENYEKITI: Kwa hiyo inavyoonekana katika Wizara hii, vifungu tofauti vina sera tofauti tofauti, maanake tumeona mahali pengine maelezo hayakulingana.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2012 - *High Commission of Tanzania - Ottawa* Sh.1,115,712,700

MHE. KIDAWA HAMID SALEHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu 221400 inahusina na *Hospitality Supplies and Services*. Nataka Mheshimiwa Waziri labda atueleweshe, kila tunapokuta *zero*, je, maelezo yake aliyoyaeleza sasa hivi kwa swali la Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o ndiyo yako sahihi? Kwa sababu kuna sehemu nyingi tu ambapo kuna *zero* lakini katika Embassies nyingine tayari kuna fedha.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu kwa mpigo sasa. Ni kwamba, hivi vifungu Waheshimiwa Wabunge mnavyoviona vimewekewa sifuri sifuri haina maana kwamba Balozi hizi hazipati fedha. Hii ni njia ambayo tunashauriwa na Mkaguzi Mkuu ya ku-control finances.

Kwa hiyo, niseme hivi, *hospitality* ni fungu la fedha ambalo unalitumia kukaribisha wageni kwamba, unapata kiasi fulani cha fedha unakitumia kukaribishia wageni nyumbani au ofisini. Tunachojifunza kwa usoefu ni kwamba ukipeleka fungu hili, baada ya mwezi mmoja unaombwa tena, tunaomba tena fedha, wageni safari hii walikuwa wengi mno kwa hiyo tuleteeni fedha. Sasa busara ya Mkaguzi Mkuu na ofisi wanasesma, ni vizuri vifungu vya aina hii ambavyo vina ushawishi maana hukosi wageni na ukitaka kuwa na wageni kila siku unaweza kuwa nao, ukitaka kuwa na mgeni kila baada ya mwezi mmoja unaweza kufanya hivyo, ukitaka kuwa na wageni kila baada ya miezi Sita, unaweza kufanya hivyo. Ukiwa na hela ushawishi wa kualika wageni kila siku upo hasa kwenye hizi Balozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *headquarters* yaani makao yetu makuu tukasema hizi hela ambazo ni za *hospitality* na *services* hata huku kama zikionyesha *zero*, makao makuu ina-take care, na mara nyingi mabalozi wanachofanya ni kueleza kuwa safari hii

anakuja mgeni fulani au tuna wageni kadhaa safari hii, akishawaorodhesha hivyo Makao Makuu sasa inamatumia pesa kwa ajili ya kukidhi mahitaji hayo. Tumeona utaratibu huo ni mzuri zaidi kuliko kupeleka tu pesa za *hospitality and services* kwenye balozi zetu kwani zinatumika kwa haraka sana na tunalazimika kulipia mara nyingi.

MWENYEKITI: Ndiyo, swali ni kwamba kuna Balozi ambazo inabidi zipate fedha za kifungu hicho kutoka makao makuu na nyingine zinapelekewa kwa sababu kwenye kifungu hicho kuna wengine wanazo pesa katika kifungu hicho. Swali ni hilo. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu lake ni dogo tu, ni kwamba katika Balozi zile ambazo hazikuwa na *hospitality and services* na watu wakaziheshimu zile *votes* bila kutumia na tusiwe na malimbikizo ya madeni unakuta kunakuwa na pesa zinazobakia pale. Sehemu zingine tumelazimika kulipa madeni na hapa inajionesha *zero* na tunawaambia wewe mpaka utakapopata wageni na utueleze ndiyo tukaletea pesa, kama unajiamini vizuri tunakupa hela pale.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2013 - <i>Embassy of Tanzania - Paris</i>	Sh.1,943,798,200
Kif. 2014 - <i>Embassy of Tanzania - Beijing</i>	Sh.1,074,423,600
Kif. 2015 - <i>Embassy of Tanzania -Rome</i>	Sh.1,751,839,800
Kif. 2016 - <i>Embassy of Tanzania -Stockholm</i>	Sh.1,116,569,600
Kif. 2017 - <i>Embassy of Tanzania - Tokyo</i>	Sh.1,372,142,700
Kif. 2018 - <i>Embassy of Tanzania -Washington</i>	Sh.1,853,856,700
Kif. 2019 - <i>Embassy of Tanzania -Brussels</i>	Sh.1,408,904,700
Kif. 2020 - <i>Permanent Mission to the UN - Geneva</i>	Sh.1,920,301,100
Kif. 2021 - <i>Embassy of Tanzania - Kampala</i>	Sh. 740,171,400
Kif. 2022 - <i>High Commission of Tanzania - Harare</i>	Sh. 854,613,100
Kif. 2023 - <i>Embassy of Tanzania - Nairobi</i>	Sh. 1,599,304,300
Kif. 2024 - <i>Embassy of Tanzania - Riyadh</i>	Sh. 890,120,600
Kif. 2025 - <i>Embassy of Tanzania - Pretoria</i>	Sh. 1,168,465,500
Kif. 2026 - <i>Embassy of Tanzania - Kigali</i>	Sh. 628,438,700
Kif. 2027 - <i>Embassy of Tanzania - Abu-Dhabi</i>	Sh. 1,220,059,000
Kif. 2028 - <i>Embassy of Tanzania - Bujumbura</i>	Sh. 732,443,400
Kif. 2029 - <i>Embassy of Tanzania - The Hague</i>	Sh. 687,355,500
Kif. 2030 - <i>Embassy of Tanzania - Lilongwe</i>	Sh. 662,927,800
Kif. 2031 - <i>High Commission of Tanzania - Brasilia</i>	Sh. 960,177,400
Kif. 2032 - <i>High Commission of Tanzania - Kuala Lumpur</i> ...Sh.	969,197,800

(*Vifungu vilivytajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

Kif. 1004 - <i>Policy and Planning</i>	Sh. 20,269,113,100
--	--------------------

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko hapo hapo *subvote* 104, kifungu 6391 - *Acquisition, Expansion and Rehabilitation of Mission*. Ubalozi wetu wa Addis Ababa, nilisikia maelezo yaliyotolewa kwamba ule uwanja...

MWENYEKITI: Ngoja kwanza, kimendikwa wapi Addis Ababa? Kifungu tumekiona; *acquisition, expansion and rehabilitation of mission; ni mission gani ndiyo swali lenyewe?* Wewe unauliza nini?

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wangu wa swali *nili-assume ni missions* ambazo ziko ndani ya *foreign services*. Sasa nilikuwa nataka kuulizia kuhusu *mission* yetu ya Addis Ababa.

MWENYEKITI: Uliza hizi fedha ni kwa ajili ya nini? Unataka iwe ni *mission*, hawakusema ni *missions*, ambayo ingekuwa inakubalika. Hii ni hela kwa ajili ya kitu gani? Naomba ulize swali lako namna hiyo; umenielewa? Tunauliza hivyo, kwa sababu yeye hawezi kuingiza Addis Ababa hapa, sisi hatujaiona ndiyo maana tunauliza hizi ni za kazi gani?

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, au katika kifungu hicho ni pamoja na *expansion* ya Ubalozi wetu wa Addis Ababa, ambao ulikuwa unazingatia kujenga Kituo cha Kiswahili ili tuweze kuuza Kiswahili kama bidhaa katika MakaoMakuu ya AU? Ndiyo ulikuwa msingi wa swali langu. Naomba ufanuzi kama hiyo *mission* maana yake ni pamoja na Addis Ababa?

MWENYEKITI: Sawasawa hilo ndiyo swali. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo *mission* ni pamoja na Addis Ababa. Kuhusu ujenzi wa Kituo cha Kiswahili, pesa za ujenzi wa Kituo cha Kiswahili zilikwishatolewa na ujenzi huo umeshaanza kwenye Makao Makuu ya AU pale Addis Ababa. Kwa hiyo, sisi kama Tanzania, hatuhitaji tena kutoa mchango wa pesa za ujenzi wa kituo kile.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

TAARIFA

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi, imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa Mwaka 2009/2010, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, Makadirio haya sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(Makadirio ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka 2009/2010 yalipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, imepitishiwa fedha zake kihalali na kama walivyosema Wabunge, tunaomba kila hela ndogo itumike kama inavyopaswa, kwa manufaa ya nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge, kubwa ambalo nimefikiri tumejifunza na naomba niseme, Bunge ni kitu kimoja muhimu sana katika nchi yoyote; na kwa hiyo, Wabunge wake wanaposema kweli uwe umehesabu maneno yako mdomoni, kwa sababu neno lako moja ni bomu; ni kweli kabisa, kwa waliochangia wengi wana lugha hapa rahisi rahisi, lakini nchi nydingi zimepigana vita kutokana na maneno haya haya. Tuna lugha nydingi rahisi sana, mtu anafikiri anazungumza *for funny* tu, lakini kuna maneno mazito yanatokea humu ndani. Kwa hiyo, nafikiri Waheshimiwa Wabunge, mjue kabisa mkiwa hapa, mnawakilisha nchi nzima na mnawakilisha Dunia na wala siyo kwamba unamwambia Spika tu; unauambia Ulimwengu mzima, tuwe waangalifu na maneno yetu. Tunapoapishwa, tunapewa Katiba na kila kitu, watakaolinda nchi hii ni Wabunge na watakaoipotosha nchi hii ni Wabunge. Kwa hiyo, jamani kauli zetu nydingine, mtu uwe unajiuliza kwanza. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hawa waandishi wa habari hawa wanapokwenda kuandika, wao wanaandika kwa lengo la kuuza magazeti. Nao pia ni hatari, lakini hatari zao ukizikanusha ndani ya Bunge, wewe utasikilizwa vizuri zaidi kuliko wao. Kwa hiyo, ninafikiri tuwe waangalifu sana, maana wengine tunajifunza hapa. Mimi ninawaambia nimetoka Kigali, kilichotokea ni sababu ya maneno haya haya ya kupita ovyo ovyo. Tumetoka Kigali kwa vita iliyotokea kule, mauaji ya halaiki (*genocide*). Unalala chumbani na mke wako, lakini kwa sababu ni kabilia lingine, unamchinja akiwa kitandani. Ndivyo ilivyotokea, mtoto uliyezaa wanadai mtoto hata kama amezaliwa na kabilia lingine, lakini damu yake ndiyo hiyo hiyo ya huyo mtu mwingine, wanamchinja naye.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo ni vitu vidogovidogo tu, ooh! udini, ukabila, nini! Kwanza kabisa, mtu anayesimamia katika maeneo haya ni mtu aliyefilisika. Yeyote anayesimamia kwenye maeneo ya ukabila, udini na ubaguzi mwingine ni mionganoni mwa wale waliofilisika katika vichwa vyao na hawana kazi nydingine isipokuwa kufurahia kuleta fujo. Kwa hiyo, mimi nasema haya tuyazingatie na sisi wengine hatuyapendi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nina jambo lingine; tukiwa Bungeni ninaomba kila mtu awe huru; Wabunge muwe huru na Mawaziri wawe huru, kwa sababu hapa ni pande mbili; Wabunge wanaailiza Serikali na Serikali inapaswa kujibu. Msichukue kama ni *vendetta* ya mtu na mtu. Inaanza kuonekana tabia hapa, mtu akisimama akisema inaonekana kama anamwandama mtu fulani; si sahihi! Tuzungumze, Kiti kiko hapa kwa ajili ya *ku-control* kama huyu anakwenda *out of order* ama yuko sahihi, mkimaliza hapa shikaneni mikono tembeeni, ongeeni. Humwandami mtu na hoja zako na ndiyo maana tuna Kanuni za kusema, usiseme uongo wala usimwonee mtu, ukibainika unapata adhabu *including kufukuzwa* katika Bunge. Kwa hiyo, unapojadili hapa uwe huru kabisa, lakini usichukue suala *personally* kabisa, mtu anakuwa *touched* kabisa. Wewe unayejadili usimhusishe mtu, kama unamjadili Waziri ni ile Ofisi yake siyo mtu, naona inaanza kujengeka tabia mtu anambana Waziri, tutaharibikiwa na Bunge litakosa heshima yake. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, *lobbying fine*, lakini na wewe unayefikiria kuwa *lobbed* pia utumie akili yako kuwa hiki anacho-*lobby* kina-sense or what? Kama wewe mtu anaku-

lobby halafu unakwenda tu anavyotaka huyo anaye ku-*lobby*; nao pia ni upuuzi! Kwa hiyo, nasema tuheshimu. (*Makofit*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nina matangazo machache: Mheshimiwa Shellukindo, Mwenyekiti wa ile *club* ya wenzetu wanaolenga shabaha, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa, kesho tarehe 19, Julai, kutakuwa na zoezi la kulenga shabaha huko Makutupora. Usafiri wa kuwapeleka Waheshimiwa Wabunge utakuwepo katika Ofisi za Bunge, nafikiri kuanzia saa mbili asubuhi. Kwa hiyo, wale wataalamu wa kulenga shabaha wajiandae.

Tangazo lingine linatoka Ofisi ya Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Wabunge, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, leo tarehe 18, Julai, kutakuwa na burudani ya Waheshimiwa Wabunge, kwa hisani ya NMB kama ifuatavyo:-

Kuanzia saa tisa mpira wa miguu na mpira wa pete na washindani wetu watakuwepo pale. Kwa hiyo, ninawatakia kila la kheri timu yetu muweze kushinda. Tangazo la pili, kuanzia saa mbili usiku, kutakuwa na tafrija kwenye Viwanja vya Bunge, Jengo la Utawala. Bendi itakayotumbuiza ni Saki Star na Mgeni Rasmi ni Mheshimiwa Waziri Mkuu. Vilevile kesho tarehe 19, Julai, Siku ya Jumapili, kutakuwa na mchezo wa kirafiki kati ya Timu ya Mpira wa Miguu ya Bunge na Timu ya Albino United kutoka Dar es Salaam, mchezo huo utaanza saa 10.30. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kushangilia shughuli hizi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana kwa kazi tuliyofanya wiki nzima. Tumekuwa na kazi nzuri, Waheshimiwa Wabunge mnajua namna ya kuuliza maswali kwenye vifungu, kwa kweli mnauliza vizuri sana na kama nilivyosema kuhusu namna ya kujibu maswali, Waheshimiwa Mawaziri wameendelea kuandika majibu mafupi. Kwa hiyo, nadhani tunakwenda vizuri na hapo tutakuwa na Bunge lenye uchangamfu.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatakie *weekend* njema na burudani zote hizi, halafu tuonane Siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi, hapa hapa Bungeni.

(*Saa 01.20 mchana Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 20 Julai, 2009 Saa Tatu Asubuhi*)

